

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini na Nane - Tarehe 27 Juni, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):

Utekelezaji wa Taarifa ya Ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of the Local Government Authorities for the year ended 30th June, 2012).*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):

Taarifa ya Majumuisho ya Mpango Mkakati wa kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Wizara, Idara za Serikali na Mikoa (*Vol. I na II*) kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali leo na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na atakayetuulizia swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Joseph Machali, tunafurahi kukuona ukiwa na afya nzuri.

Na. 478

Kero za Polisi kwa Wananchi – Kasulu

MHE. MOSES J. MACHALI aliuliza:-

Je, ni lini Waziri atatembelea Jimbo la Kasulu Mjini kuwasikiliza wananchi juu ya kero wanazopata dhidi ya Jeshi la Polisi kuwanyanyasa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kujibu swali, naomba nimpe pole Mheshimiwa Machali kwa masahibu yaliyompata. Namwomba kwa Mungu amjalie apone haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, nipo tayari kutembelea Jimbo la Kasulu Mjini kwa ajili ya kuwasikiliza wananchi juu ya kero wanazopata dhidi ya Jeshi la Polisi kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa mara tu baada ya kikao hiki tuonane ili tupange ratiba na utaratibu wa ziara hiyo. Naomba kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, kutembelea sehemu hizi hii ni sehemu kubwa ya kazi niliyopewa na niko tayari kuitekeleza kwa faida ya Watanzania popote walipo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, naomba niishukuru Serikali na hasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuhakikisha kuwa wamesimamia kesi moja, ambayo

ilikuwa ni ya mauaji ambayo yalifanywa na Jeshi la Polisi, baadhi ya askari ambao siyo waadilifu ambapo majuzi haki imetendeka chini ya Mahakama Kuu Kanda ya Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la kuweza kumwuliza Mheshimiwa Waziri, mwaka jana moja ya manyanyaso ambayo wananchi wa Jimbo la Kasulu Mjini na Wilaya ya Kasulu ambayo wanakabiliana nayo ni suala la kupigwa hadi kupoteza maisha na baadhi ya askari wasiokuwa waadilifu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba mwaka jana kuna mtu mmoja pia alipigwa na askari akapoteza maisha kwa sababu raia alikuwa anamdai pesa askari. Sasa nataka kujua, kwa kuwa suala hili nimeshalifikisha mpaka kwenu, mwanzoni ilionekana ile kesi wameitupilia mbali, na mtu kapoteza maisha na kuna ushahidi mpaka wa picha, kama kesi ambayo nimesema mwanzoni kuwa, walikuwa wanaizungusha naomba kupata kauli ya Serikali.

Mwananchi aliyepigwa na askari wawili katika Kijiji cha Elushingo, Wilaya ya Kasulu na kupoteza maisha, Wizara yako iko tayari kutupatia watu kutoka Ofisi ya *DCI* haraka au mapema iwezekavyo, kama walivyofanya kwa watu wengine ili kusudi upelelezi uweze kuanza upya na hatimaye tuone askari wale ambao wamefanya mauaji ambayo wanatuhumiwa kufanya mauaji, wanachukuliwa hatua kama askari wengine kwa sababu hata wale wengine mambo yalikuwa yanakwenda ndivyo sivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Wizara iko tayari kutuma wapelelezi katika kesi hii ya mauaji na si hii tu popote ambapo kuna kesi za namna hii tuko tayari kufanya wajibu wetu ili kuhakikisha kwamba, mtu anapewa haki anayostahili.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona ili niulize swali moja la nyongeza. Miongoni kwa sababu zinazolifanya Jeshi la Polisi kujihusisha na rushwa na kuwafanya wananchi kuwa mtaji wao hususani vijana wetu wanaoendesha bodaboda ni mafao yao kutokulipwa kwa wakati na Jeshi la Polisi linadai zaidi ya bilioni 28. Naomba nifahamu, ni kwa nini Serikali

isilipe hili deni la Polisi kwa wakati ili kuepusha adha kwa wananchi wetu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi haina nia ya kumdhulumu askari yeyote na inatambua bila shaka kwamba, utendaji wa askari yeyote unategemea kiasi gani anatumzwa na anapewa haki zake au pengine anapata motisha katika kazi anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilionalo ambalo ni la msingi ni kwamba, mahitaji yetu ya kazi za kawaida ni makubwa kuliko bajeti tunayoipata, kwa vyovyote kutakuwa na malimbikizo. Pamoja na hivyo, Serikali inachukua jitihada kubwa na malimbikizo yaliyopo yanafanyiwa uhakiki na tunategemea yataendelea kulipwa. Tatizo ni kwamba kazi inapohitaji askari aende, hakuna utaratibu wa kutakiwa aseme posho iko wapi wakati haipo.

Mheshimiwa Spika, inabidi aifanye baada ya kurudi ndiyo aje aulize. Tunawashukuru askari kwa kutuelewa, lakini jitihada tutazichukua pamoja na Wabunge mtusaisdie ili bajeti ya utendaji wa Jeshi la Polisi uongezeke na kazi zifanywe ili huduma za Kipolisi zifike kwa wananchi wote kama inavyotakiwa.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa hali ya ulinzi sasa hivi nchini siyo nzuri na kwa kuwa mikoa mingi inakabiliwa na upungufu wa magari hasa ya *patrol*. Je, Serikali kutokana na hali hii iko tayari kupeleka magari Mikoani angalau moja moja ili kuimarisha hali ya ulinzi nchini?

SPIKA: Msianze kulibadilisha hili swali, maana sasa naona mnalibadilisha mara mafao, mara sijui magari, swali la msingi halikuwa hivi. Sio mradi Polisi basi ndio muwe mnauliza vyovyote, hapana. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, tunatambua upungufu wa magari na vitendea kazi vingine unaolikumba Jeshi la Polisi Mikoa yote nchini. Pia tunajua ni kiasi gani askari wetu hawatimizi malengo waliyonayo kwa wakati kutokana na hili na wakati mwingine hata huduma zao zinachelewa

hata wakati wa dharura, jitihada tunazo kubwa sana za kutaka wote waweze kupata vitendea kazi. Katika kulithibitisha hilo, hata katika bajeti tuliyonayo mwaka huu tulijaribu kuomba ziada ili tuweze kuyashughulikia masuala hayo, lakini hatukuweza kufanikiwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hivyo tuna mipango ambayo iko nje ya bajeti tunaendelea kuifanya na ni matumaini yetu kuwa magari yatakuja na askari watapata katika Mikoa yote ya Tanzania. Kwa sasa tumejaribu kupata pikipiki na tumezisambaza ili nazo zisaidie katika ulinzi wa nchi hii.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nimuulize Waziri wa Mambo ya Ndani, wakati nachangia Wizara ya Mifugo nilieleza kuwa katika Jimbo la Muleba Kaskazini na hasa Kata ya Rutoro kunahitajika maridhiano kutokana na chuki iliyojengeka kati ya Jeshi la Polisi na wananchi. Kwa kuwa kuna wananchi wameonewa na viongozi wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Kagera hawataki kuwasikiliza wananchi. Je, Mheshimiwa Waziri mtakubali kuchukua askari waadilifu kutoka Makao Makuu ili wakasikilize mgogoro wa sasa ambapo Polisi wanawabambikia watu kesi ambazo hawahusiki nazo ili mpate kauli kutoka kwa wananchi wenyewe? (*Makofi*)

SPIKA: Itabidi nifunge hili swali. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, itabidi nisiendeleo kwa sababu mna *mislead*.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, kuna baadhi ya maeneo kuna migogoro kati ya wananchi na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, tunachukua hatua hasa kwa kutumia *task force* kuzunguka ili kuhakikisha kuwa migogoro hii pale iliposhindikana kutatuliwa Kimkoa, tunaishughulikia na kuimaliza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni moja katika majukumu ambayo tutayafanya na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutapeleka Maafisa na Washauri ili wahakikishe kuwa hili tatizo linafikia kikomo.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Swali la msingi linazungumzia Waziri kutembelea Majimbo, sisi

Tunduru hatuna matatizo ya wananchi kunyanyaswa na Polisi, isipokuwa Polisi wana matatizo ya mazingira magumu ya kikazi. Je, Waziri atakuwa tayari kutembelea Jimbo la Tunduru ambalo halijatembelewa kwa muda mrefu sana na Waziri wa Mambo ya Ndani ili waende kubaini matatizo mbalimbali yanayowakabili Polisi wetu wa Wilaya ya Tunduru?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa jumla nafahamu kuwa, kuna matatizo katika Wilaya zote za Kipolisi ikiwemo Wilaya ya Mheshimiwa Mbunge. Pamoja na hayo, nafikiri nikubaliane naye kuwa, tupate muda twende kule ili tuone hasa kule kuna matatizo gani ili tuweze kuyashughulikia kwa karibu, kama ilivyo kwani baada ya kuyaona na kujua, tunaweza tukawa na weledi zaidi wa kuyashughulikia.

SPIKA: Ahsante sasa tuendeleo na swali linalofuata, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha atauliza, kwa niaba yake Mheshimiwa Desderius Mipata!

Na. 479

Uhaba wa Samaki katika Ziwa Rukwa

MHE. DESDERIUS J. MIPATA (K.n.y. MHE. IGNAS A. MALOCHA)
aliuliza:-

Ziwa Rukwa ni chanzo kikubwa cha ajira kutokana na shughuli za uvuvi wa samaki, lakini kwa sasa ziwa hilo linakabiliwa na uhaba mkubwa wa samaki:

- (a) Je, nini kinasababisha uhaba mkubwa wa samaki?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa Ziwa hilo linapata samaki kama zamani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (*TAFIRI*), ilifanya utafiti katika Ziwa Rukwa ili kubaini sababu za kupungua samaki katika ziwa hilo. Utafiti huo ulibaini kuwa sababu hizo ni pamoja na:-

- (1) Uharibifu wa mazingira ikiwemo uharibifu wa mazalia ya samaki;
- (2) Uvuvi haramu na matumizi ya nyenzo haramu, yakiwemo matumizi ya nyavu zenye matundu madogo;
- (3) Shughuli za kibinadamu zikiwemo kilimo, mifugo, uchimbaji madini na ukataji miti ovyo;
- (4) Ziwa kujaa udongo (*siltation*) na kupungua kwa kiasi cha maji ziwani;
- (5) Uvunaji wa samaki wachanga;
- (6) Uvuvi uliozidi kiasi cha Ziwa kuweza kustahimili; na
- (7) Uchafuzi wa maji ya Ziwa unaosababishwa na kemikali za madini; wachimbaji wanapoosha madini na maji hayo machafu huingia ziwani.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kunusuru hali ya uvuvi katika Ziwa Rukwa, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Kufanya doria za mara kwa mara ili kukomesha uvuvi haramu na uharibifu wa mazalia ya samaki. Kuanzia 2010 hadi 2013, doria zilizofanyika zilisaidia kukamatwa kwa makokoro 105, nyavu zenye macho madogo 67, mitumbwi 28 na mahema matatu.

Pia kutoa elimu ya mazingira na athari za uvuvi haramu kwa kutumia mikutano, redio, luninga na machapisho mbalimbali.

Kuanzishwa vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (*BMUs*) ambavyo katika jitihada hizo vikundi kumi vimeundwa (vitano Chunya na vitano Mbozi). Aidha, Halmashauri zinazopakana na Ziwa Rukwa zinashauriwa kuandaa Sheria Ndogo za Kufunga Shughuli za Uvuvi na kufungua kwa kipindi maalum ili kuruhusu samaki kuzaliana.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa tafiti zinaonesha katika miaka 50 ijayo kama jitihada za makusudi hazitachukuliwa kunusuru Ziwa Rukwa litatoweka. Je, Serikali ina utaratibu gani na ina mpango gani maalum na wa haraka wa kuwezesha kulinusuru Ziwa hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi wengi wanaoishi kandokando ya Maziwa yetu ni maskini sana na wanapolazimika kutumia nyenzo haramu katika uvunaji wa samaki ni katika hali ya kujikimu tu kwa sababu ya umaskini wao. Je, Serikali ina mpango gani endelevu na wa kudumu kuhakikisha wanapewa mikopo ili waondokane na uvunaji haramu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema, naomba nikubaliane naye kwamba, jitihada zisipochukuliwa Ziwa Rukwa lipo katika hatari kwa sababu, kwanza, ni kwa mazingira ya Ziwa lenyewe kwamba, ni Ziwa ambalo lina mito 11 inayopeleka maji kwenye Ziwa, lakini hakuna *outlet*, halitoi maji kupeleka popote. Kwa hiyo, maji yanapungua kwa njia mbili, yale yanayozama ardhini, lakini pia *evaporation* ipo juu kwa sababu ipo katika eneo la bonde la ufa.

Mheshimiwa Spika, lakini mipango ya Serikali ipo, tayari kuna Mradi wa Mazingira unaogusa Ziwa Tanganyika na kufika hadi Ziwa Rukwa. Lengo lake kuu ni kuhakikisha kwamba, moja mazingira yatatunzwa, lakini pili hamasa ya watu iongezeke na wao wenyewe wafahamu kwamba, kuendelea na baadhi ya shughuli za kiuchumi

ni kuzamisha ziwa hilo ambalo pia ni muhimu sana kwa maisha na *livelihood* za watu wanaozunguka ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina mipango ya kujaribu kuunda vikundi katika maeneo hayo ambapo vikundi vilivyopo vitaimarishwa. Pia tunatarajia kwamba, mikopo itaweza kupatikana kwa ajili ya vikundi hivyo kuweza kuvua kwa namna endelevu, lakini pia kuna mipango ya kuendeleza *aquaculture* katika eneo hilo ili badala ya watu kuendelea kuona kwamba, ni lazima wavue katika maji ya asili, watu pia waanze kujenga madimbwi yao na kufuga samaki kwa sababu hii itaondoa msongamano wa uvuvi katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge; mikopo hivi sasa tayari inapatikana hasa katika benki ya *TIB* na tunatarajia kwa njia ya ruzuku, kwa fedha tuliyoongezewa, baadhi ya vikundi katika eneo hilo vitawezeshwa ili viweze kushikamana, wavue vizuri zaidi, lakini pia waanze kilimo cha samaki na hata hivyo pia waendeleo kuwa ni watunzaji wa mazingira katika eneo hilo. (*Makofi*)

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Tatizo la uhaba wa samaki katika Maziwa Makuu ni tatizo ambalo linazidi kuongezeka likihusisha vilevile Ziwa Victoria na tayari kuna mawazo ya mpango wa kuvuna kwa nyakati.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Wizara iliwasilisha hapa mpango wa kuendeleza sekta ya uvuvi katika nchi yetu, lakini hakuna hatua ambazo zinajionesha za dhahiri ambazo zinatekelezwa mpaka sasa. Naomba Waziri atueleze ni lini hasa mpango huu utaanza kutekelezwa ili maeneo yetu yaliyostahili kwa masuala ya uvuvi yaweze kufanya ufugaji wa samaki? Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Nawaomba mliosimama muulize maswali mafupi ili kusudi wote mpate nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema kwamba, katika maeneo

mengi ya Maziwa yetu ikiwemo Ziwa Victoria kiasi cha samaki kinazidi kupungua kwa sababu ya uvuvi unaofanyika bila kuzingatia uwezo wa Ziwa.

Mheshimiwa Spika, pia ni kweli kama Wizara tuliwasilisha mpango hapa, lakini Mheshimiwa Mbunge naye atakuwa shahidi kwamba, mpango huo kwa sababu ya ufinyu wa bajeti haukuweza kupatiwa rasilimali. Mwaka huu tu ndiyo kumekuwepo na nyongeza ya fedha ya bilioni 20. Katika hizo bilioni 20 zilizoongezwa, kiasi kitakwenda katika kuhakikisha kwamba mpango huo utatekelezwa na Ziwa Victoria litakuwa ni moja kati ya Maziwa yatakayonufaika na mpango huo wa kuendeleza Sekta ya Uvuvi.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hali ya *Lake Rukwa* ni sawasawa na *Lake Tanganyika*. *Lake Tanganyika* kila mwaka linapungua si chini ya mita moja ya maji. Kila mara wanazungumzia mikakati na mipango ya kwenda kule Congo kwa mazungumzo, waliandika hata katika bajeti ya mwaka uliopita kwamba, mazungumzo yanafanywa na Serikali ya DRC-Congo, Burundi, Zambia na sisi Tanganyika ili kupunguza Mto Lukuga kutoa maji kwenda Congo kama zamani. Je, mikakati hiyo ya mazungumzo imefikia wapi ili kupunguza maji yasitoroke zaidi kutoka Ziwa Tanganyika?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Ziwa Tanganyika kweli ni moja kati ya Maziwa ambayo hayakupata kipaumbele huko nyuma, lakini kwa sasa kuna miradi kadhaa inayoendelea Ziwa Tanganyika ikiwemo Mradi unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Mradi huu ni wa Mazingira, lakini kwa uhakika utakuwa na fursa ya kuboresha hasa *habitat* ya samaki katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya mipango inayoendelea, miundombinu inaendelezwa katika Ziwa Tanganyika ikiwemo mialo minne inayojengwa katika Ziwa hilo. Katika nyongeza pia ya pesa tulizopata, boti zinanunuliwa hasa kwa ajili ya vikundi vya uvuvi vinavyozunguka eneo hilo ili kuhakikisha kwamba, watavua kwa namna iliyo bora zaidi na kwa namna ya kibiashara. Vile vile tunatarajia kwamba vikundi hivi pia vitakuwa ndiyo walinzi wa kwanza wa rasilimali na mazingira yanayozunguka Ziwa Tanganyika.

MHE. SUSAN L.A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa suala la upungufu wa samaki katika Maziwa na Mito mbalimbali katika nchi yetu sasa ni suala ambalo linaonekana kama ni la mazoea.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilombero, Mto Kilombero kuna samaki maarufu sana wanapatikana tu wakati wa mavuno wanaitwa Njuju, Mlamukaliandili na Ndipi, lakini sasa Serikali bado inakataza wananchi kuvua wale samaki ambao hawapatikani kipindi kingine chochote. Ni nini kauli ya Serikali kuwazuia wananchi wa Kilombero kuvua samaki ambao wanapatikana kipindi cha mavuno tu?

SPIKA: Mkiangalia maswali kama hayo, yanafanana kabisa na swali la mwanzo? Hayafanani kabisa. Kule wanazuia kuvua, wewe unasema kwa nini hawavui.

Mheshimiwa Naibu Waziri, labda unawajua hao samaki. Waheshimiwa Wabunge msiulize maswali ya namna hiyo. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, tunapotazama bio-*diversity* ya samaki, kuna *species* ambazo zinapatikana kwa wingi na kuna nyingine ambazo kwa kweli zipo hatarini kutoweka. Kwa hiyo, sera inaelekeza baadhi ya *species* kutovuliwa, sababu ni hiyo ya *sustainability* kuhakikisha kwamba hawatavuliwa wakaisha kwa sababu na wao wenyewe wana mchango mkubwa sana katika bioanuwai ya maeneo hayo na pia katika rasilimali za samaki. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, kilimo cha samaki duniani ni miongoni mwa kazi ambazo zinaajiri watu wengi duniani. Leo Nigeria wana mpango wa kuzalisha tani milioni tano, mradi ambao utaajiri takribani watu milioni nne. Sisi Tanzania...

SPIKA: Jamani hotuba hapana, maswali ni maswali.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna *potential* kubwa sana za *fishing*. Ukiangalia Tanzania na Namibia kwa mfano, Namibia wana *Coastal Zone* kwenye *Indian Ocean*

takribani kilomita 1,500; Tanzania tuna kilomita 1,424 tunakaribia kulingana, lakini kiasi ambacho tunakipata...

SPIKA: *Please ask a question*, hotuba za kazi gani? Maana hizo ni hadithi, uliza swali, wewe unataka kuuliza nini sasa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, namjengea uwezo ili kusudi ajibu vizuri. (*Kicheko*)

SPIKA: Hapana, kama hutaki naendelea.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, nauliza swali, Tanzania kwa *potentials* kama hizo ambazo tunazo ambazo kimsingi tunalingana na Namibia, ni kwa nini tumeshindwa kuwekeza na kwa nini tumeshindwa kuifanya sekta ya uvuvi kuchangia sehemu kubwa ya pato la Taifa pamoja na ajira kama ambavyo Namibia wamefanya na wakati tunalingana katika *Potentials?* (*Makofi*)

SPIKA: Sawa, hilo ndiyo swali. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Tanzania ina fursa nyingi na tuna rasilimali za uvuvi nyingi. Lakini niseme tu, ni moja kati ya changamoto ya maendeleo, maana unapokuwa nchi changa inayokua, vipaumbele ulivyonavyo vinashindania rasilimali zilizopo. Kama tulivyopitisha bajeti yetu, pesa imekwenda kwenye maeneo ambayo pia ni muhimu katika kuja kuchochea baadaye sekta kama hii ya uvuvi pia kukua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani ni suala la mipango yetu maana kupanga ni kuchagua na kuchagua ni kupanga. Tumeweka maeneo mengine kama ya barabara na miundombinu mingine kama ndiyo kipaumbele, sekta ya uvuvi na yenyewe itakuja. Lakini kwa uhakika muda si mrefu, tumejipanga, kwa hiyo, tutaanza kuingia huko na kuhakikisha kwamba sekta hii itazalisha vizuri zaidi na hata kuzidi nchi hizo anazotoa Mheshimiwa Mbunge kama mfano.

Mheshimiwa Spika, isitoshe, sekta imeendelea kukua kwa kiasi cha watu wanaoajiriwa katika sekta hiyo, kiasi cha pesa zinazoingizwa kwenye *GDP* na katika maisha ya watu, kiasi kinachochangia katika *food security*. Kwa hiyo, ukitazama sekta kwa stahili zake yenyewe, imeendelea kukua japo huenda kukua kwake si kwa kiasi ambacho tungeweza kulinganisha na maeneo mengine ambayo Mbunge ametoa. Lakini huenda na sisi tukiwa *realistic* kama nchi, tumepiga hatua katika maeneo mengine kuzidi nchi hizo unazotoa mifano. (*Makofi*)

SPIKA: Tumepiga hatua, sisi tupo milioni 45, wenyewe wapo milioni moja na laki nane (1,800,000). Mheshimiwa Jenista Mhagama!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa, matatizo haya ya upungufu wa samaki na hasa katika Ziwa Nyasa yanasababishwa na tabia ya viwanda vingi kutengeneza nyavu haramu ambazo wavuvi ndiyo wanazitumia, kitu ambacho Serikali ingeweza tu kupiga marufuku uzalishaji wa nyavu haramu.

Je, ili kuhifadhi hao samaki wanaopotea sana kwenye Maziwa yetu kwa matumizi ya nyavu hizo haramu, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kuchimba mabwawa ya ufugaji wa samaki ili kuhifadhi mbegu nzuri ya samaki katika Maziwa kama vile mipango tuliyonayo kwenye Jimbo la Peramiho?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza Sheria na Kanuni zetu zipo wazi kwamba, nyavu haramu zimepigwa marufuku. Ili kuweka msisitizo kwamba nyavu hizo zinadhibitwa, Waziri Mkuu katika barua yake ya tarehe 18 Januari, 2010 aliandika kwa Wakuu wa Mikoa yote Tanzania, akiwataka wahakikishe kwamba utengenezaji, usafirishaji na matumizi ya nyavu hizi zilizo haramu zinadhibitwa na kuhakikisha kwamba hazitumiki.

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, doria nyingi zimefanyika na hata katika viwanda hivyo kuna watu wanaotengeneza

wameshikwa na wakafunguliwa kesi ambazo zipo Mahakamani. Lakini kama alivyosema Mbunge, katika mkakati wetu wa kuendeleza Sekta ya Uvuvi, *aquaculture* ama ukuzaji wa viumbe ndani ya maji ni kitu tunachoweka mkazo sana.

Mheshimiwa Spika, pia tayari kuna maeneo mengi ambayo mabwawa ya samaki yametengenezwa mazuri na yanachangia sana katika sekta hii ikiwemo mikoa kama Kagera na kule kwa Mbunge anakoongelea pia hiki ni kitu kinachoshika kasi na sisi kama Wizara kwa uhakika tutahakikisha kwamba Maofisa wanapatikana kutoa ushauri na kuhakikisha kwamba *future* ya uvuvi haitategemea maji asili tu bali pia mabwawa na watu wanufaike na mabwawa hayo ya samaki.

SPIKA: Mheshimiwa Hilda Ngoye, swali la mwisho.

MHE. HILDA C. NGOYE: Mheshimiwa Spika ahsante. Naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Katika Maziwa haya yanayotamkwa hapa sasa na hapa nchini, inavyooleweka Maziwa makuu yaliyopo ni Victoria, Tanganyika na...

SPIKA: Yanajulikana, uliza swali.

MHE. HILDA C. NGOYE: Mheshimiwa Spika, kuna samaki ambao walizoeleka kwa majina kama ningu, mbelele, mbasa, wamepotea kabisa katika eneo la Ziwa Nyasa. Tafiti nyingi zimefanyika ili kuonesha ni namna gani watafufuliwa. Je, ni mpango gani ambao Serikali kupitia Wizara hii umewekwa ili kuhakikisha samaki hao ambao walikuwa wenye biashara kubwa na watamu sana katika Afrika Mashariki wanarudi tena katika eneo hilo la Ziwa Nyasa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna aina nyingi za samaki kama nilivyosema ambazo ama zimeanza kutoweka ama wapo hatarini kutoweka. Kwa sababu hii ndiyo maana sera ya uvuvi imeweka mkazo katika kuhakikisha kwamba uvuvi wetu ni uvuvi endelevu. Kwa hiyo tumejipanga vizuri kwa upande wa sera na kwa upande wa sheria na kanuni tulizonazo, mkazo ni uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa tujaribu kuwafahamisha wavuvi popote walipo Tanzania kwamba, Serikali haina maana ya kuwabughudhi na kufanya maisha ya wavuvi kuwa magumu, lakini ni kutaka kuhakikisha kwamba rasilimali za samaki zinatunzwa, zinaendelezwa na zinaongezwa.

Mheshimiwa Spika, mipango tuliyonayo nirudie tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge, moja mara nyingine, uvuvi unafungwa kwa misimu fulani ili kuhakikisha kwamba samaki wanazaliana na hasa mkazo unawekwa katika samaki hawa ambao inaonekana zaidi kwamba, wapo hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa upande wa Ziwa Nyasa kama ilivyo katika maeneo mengine yoyote ya nchi, mpango huu na mkakati huu tutaendelea kuutumia ili kuhakikisha kwamba kuzaliana kwa samaki hao anaowaongelea Mbunge kutaongezeka na kwamba watakuwepo na watu wanaovua nao washiriki katika kuhakikisha kwamba kizazi cha samaki hao kinadumu, kinaendelea na kinaongezeka.

Na. 480

Kuifungua TAFICO

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y MHE. MKIWA A. KIMWANGA) aliuliza:-

Uamuzi wa Serikali wa kuifufua treni ya Dar es Salaam ni jambo zuri na la kufurahisha:

Je, kwa nini sasa isifikie uamuzi wa kuifufua *TAFICO* ili iweze kutoa huduma na kutoa ajira kwa vijana wengi katika sekta ya uvuvi?

SPIKA: Ahsante. Hee! utakoma leo, Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lililokuwa Shirika na Uvuvi la Tanzania (*Tanzania Fisheries Corporation (TAFICO)*) lilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969 na kutolewa katika Gazeti la Serikali Na. 58 la tarehe Mosi Machi, 1974, Toleo la Pili. Lengo kuu la kuanzishwa kwa shirika hili lilikuwa ni kuendesha shughuli za uvuvi kibiashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa tamko la kubinafsisha Mashirika ya Umma ambapo *TAFICO* iliwekwa chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) mwaka 1998 hadi mwezi Oktoba 2005. *PSRC* iliiondoa *TAFICO* katika orodha ya mashirika ambayo yalikuwa yabinafsishwe ikawa *de-specified* na Serikali iliamua kuirejesha *TAFICO* Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitangaza kuuzwa kwa *TAFICO* ndani na nje ya nchi mwaka 2005/2006 ili kupata wanunuzi wenye sifa, lakini hawakupatikana na hivyo Serikali kuamua kazi zilizokuwa zinafanywa na *TAFICO* zifanywe na sekta binafsi na mali za *TAFICO* zihamishiwe Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya Sera ambapo Serikali ilijitoa kufanya shughuli za moja kwa moja za uzalishaji na biashara, Serikali iliiza mali za *TAFICO* zinazohamishika mwaka 2008 na kubakiza mali zisizohamishika ikiwa ni pamoja na majengo ambayo iliyakarabati ili yatumike kama Ofisi na matumizi mengine ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uvuvi kwa sasa zinafanywa na Sekta Binafsi ambapo hadi mwaka 2011/2012 wapo wavuvi waliosajiliwa jumla yao ikiwa 182,816 wakiwemo wavuvi wa kati 75 na wavuvi wadogo 182,741. Serikali inaendelea kuhimiza Sekta Binafsi kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi ili iweze kutoa ajira kwa vijana na wananchi wengi zaidi waweze kunufaika.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali ni kweli ilijitoa katika shughuli hizi, lakini kwa mujibu wa Taarifa za malengo na mipango ya Serikali ni kuinua na kuendeleza Sekta hii ya Uvuvi ili iwe ni moja ya Sekta ambazo zinaweza kusaidia katika pato letu la Taifa. Suala la msingi limeuliza ni kwa nini sasa Serikali isifikirie uamuzi wa kuifufua *TAFICO* wakati ambapo tumeweza kuirejesha *ATC* au Reli bado kuwa...

SPIKA: Swali ni *TAFICO*, *ATC* zinakwenda wapi huko?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Nataka kujua, je, Serikali itakuwa tayari kulirejesha Shirika hili la *TAFICO* ili liendane na azma nzima ya ukuaji wetu wa uchumi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, idadi ya wavuvi waliosajiliwa ambao Mheshimiwa Waziri ameieleza hapa laki moja na themanini na mbili hailingani kabisa na eneo letu la uvuvi katika nchi yetu. Hii ni kusema kwamba, Serikali bado haijawa makini katika kuwatambua wavuvi wetu. Je, Wizara sasa ina mpango gani makini wa kuwatambua wavuvi wetu ili wawe wavuvi endelevu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, moja, Serikali huwa tayari kurejesha *TAFICO*, niseme tu kwamba, kinachogomba hapa kwa kweli ni Sera tuliyojiwekea wenyewe. Kwa sababu tulikuwa na Mashirika ya Umma zaidi ya 340 huko nyuma, lakini yote yali-*operate* kwa hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo Sera ikatungwa kwamba, Serikali ijikite zaidi katika kuandaa mazingira wezeshi, lakini biashara kama biashara, iachwe katika mikono ya Sekta Binafsi na kama kuna haja sasa ya kuanza kufanya mabadiliko katika Sera, niseme Mbunge tu ashauri na sisi tutatazama kama kuna haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme ni Sera ndiyo imetaka hivyo, hasa kwa sababu ya *performance* ya Mashirika ya Umma na hata hayo unayoyatoa kama mfano, kwa kweli yote yameendelea kuwa mzigo, yana-*operate* katika mazingira ya hasara. Lakini pendekezo analolitoa tatalichukua, lakini tuone kwamba tuta-*harmonize* vipi pendekezo hilo pamoja na Sera iliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha wavuvi waliotajwa laki moja themanini na, hawa ni wale waliiosajiliwa. Lakini niseme kuna wengi maana Sekta ya Uvuvi ni Sekta pana na ipo katika maeneo mengi, ina-*operate* katika mazingira mengi. Kuna wengi ambao hawajasiliwa, wana-*operate* katika mfumo wa sekta isiyo rasmi na sisi jitihada zetu ni kuhakikisha kwamba, daftari au *Register* ya Wavuvi itaendelea kujazwa ili tuendelee kuwatambua na kuwarasimishia mazingira yao ya kufanya kazi ili waweze kuwa na tija zaidi katika shughuli hizo wanazozifanya.

SPIKA: Swali la mwisho, Mheshimiwa Shah!

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali, japokuwa kwanza naomba radhi kwa jambo nitakalolisema. Kwa maelezo na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya heshima zote ninazompa, inaelekea kabisa Serikali haijali kabisa Sekta hii ya Uvuvi na wala haioni maana ya kuwa uvuvi unaweza kusaidia kuondoa umaskini na kuliletea tija Taifa letu kwa mapato makubwa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mpango huo, kwa nini msimshauri Mheshimiwa Rais kwa sababu Idara ya Uvuvi kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imekwisha tikitiki. Sasa kwa nini msimshauri Mheshimiwa Rais aiondoe Idara hii na kuirudisha Wizara ya Maliasili ili iweze kupata nguvu kama ilivyokuwa zamani, kwa sababu sasa wale watendaji na Waheshimiwa Mawaziri, viongozi wangu wameshindwa kabisa kutoa ushauri au kuiendeleza Sekta hii ya Uvuvi? (*Makofi*)

SPIKA: Hili swali siyo la Naibu Waziri. Wala hata Waziri mwenyewe sio lako, hata Waziri Mkuu hayupo. Mheshimiwa Arfi. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nina swali dogo. Pamoja na kwamba, Sera tuliyonayo sasa ni ya Serikali kujitoa kwenye biashara na kuiweka katika Sekta ya Binafsi. Je, unafahamu kwamba pamoja na nia njema hiyo ya Serikali, samaki ambao wanapatikana katika masoko yetu hususan Dar es Salaam, wanatoka Yemen na India na siyo samaki ambao tunao nchini? Je, kuna mkakati gani sasa wa kuvuna rasilimali ambayo iko nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane naye kwamba, bado kuna uagizaji wa samaki kutoka nje. Hii inatokana nadhani na vionjo vya soko huria kwamba, kuna mahoteli na watu wanaopendelea zaidi aina ya samaki hasa wanaofungwa katika makopo.

Mheshimiwa Spika, hivyo, uagizaji huu hautokani tu na uhaba wa samaki, bali ni *test* na mapenzi ya walaji na ndio maana kuna uagizaji huo.

Mheshimiwa Spika, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mipango ipo, tumeiwasilisha hapa, fedha inaongezwa na kadiri rasilimali zitakavyowekwa humo, hatuna uhaba wala upungufu wa Sera. Sera yetu imekaa vizuri, mikakati imekaa vizuri na inapokuwa kwamba tutaongezewa fedha na uwezo, miundombinu kwa uhakika itajengwa kama mipango inavyosema. Njia za uvuvi njia zitaboreka na kuongezeka, watakachopata wavuvi watauza huko na viwanda vinakokuwepo.

Mheshimiwa Spika, hicho wanachoagiza kutoka nje hakitaagizwa tena kwa sababu kutoka ndani tutakuwa na kila aina ya samaki na aina ya *test* zote zinazotakiwa, walioongezewa thamani na waliofungashwa na hivyo hawa wanaokimbilia kuagiza nje kwa sababu tu ya kujisikia salama zaidi watapata kile wanachokitaka katika viwanda vyetu vya ndani.

SPIKA: Naambiwa kwamba Waziri wa Maendeleo ya Mifugo anaweza kujibu swali la Mheshimiwa Shah kwamba wafute hiyo Idara kutoka Wizarani kwake. Mheshimiwa Waziri hebu jibu!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUI: Mheshimiwa Spika, Idara ya Uvuvi haitengewi fedha kwa sababu iko Wizara fulani. Inategemea tu Mfuko wa Serikali kuziwezesha Idara ndivyo vitakavyotengewa fedha. Kwa hiyo, kama iko Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ama ipo Wizara ya Maliasili na Utalii haijalishi, kinacho-*matter* ni upatikanaji wa fedha. Lakini suala la kupanga Idara ama kupanga *instrument* ni jukumu la Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

SPIKA: Rais mwenyewe amesikia. Waheshimiwa, huyu jamaa hamwezi kukubali kwamba amejitahidi? Amejibu maswali mpaka unamwonea huruma, kwa hiyo nimesitisha. (*Makofi*)

Ubaya wenyewe maswali mengine yalikuwa hayahusiani na ya msingi, lakini ameyajibu yote. Kwa hiyo, nimeona nitishe, tuendelee na shughuli zingine.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo mchana saa saba watakuwa na Kikao katika Ukumbi Na. 133.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, hapana kikao hakiwezi kuwa asubuhi, kitakuwa saa saba mchana *Basement*. Maana yake anayeomba kikao saa tano, lazima aniombe mimi ruhusa, kwa sababu hamwezi mkaondoka, mkaenda kwenye kikao. Kwa hiyo, ni saa saba. Sijapata mtu ambaye kaomba ruhusa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao leo. Hawa saa hawakutaja, nadhani saa saba katika Ukumbi wa Msekwa.

Halafu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yao kwamba, leo saa saba mchana

watakuwa na Kikao na wao *Basement*, sasa kule *Basement* mtajua wenyewe kwa sababu wengine wako pia *Basement*.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Said Nkumba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa saba watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa (C).

Halafu Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi Bungeni, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa kutakuwa na kikao cha Chama mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba, anasema kikao hicho ni muhimu sana. Kwa hiyo Wajumbe wote wa *Caucus* ya CCM wakutane Msekwa.

Halafu huyu Katibu Msaidizi wa Chama cha Wabunge wanaopambana na UKIMWI, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa *TAPAC* kwamba kutakuweco na Kikao leo mchana saa saba katika Ukumbi wa Msekwa na huko kuna mkutano mwingine. Kwa hiyo, sijui kama ni Wajumbe wote, lakini mtajua wenyewe.

Pia Ofisi inatangaza kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wachukue nyaraka zilizoko kwenye *Pigeon hole* zao ili kutoa nafasi kwa nyaraka nyingine muhimu kuwekwa kwa ajili yao. Maana yake hawa ambao hawajatoa *Pigeon holes* zimejaa, kwa hiyo, hakuna kwa kuweka nyaraka zingine, mkatoe kusudi muwekewe zingine. (*Makofi*)

MISWADA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013 (The Finance Bill, 2013)

(Kusomwa Mara ya Pili)

ISSN 0856-035X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BILL SUPPLEMENT

No. 9

14th June, 2013

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 24 Vol. 24 dated 14th June, 2013

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE FINANCE ACT, 2013

ARRANGEMENT OF PARTS

<i>Part</i>	<i>Title</i>
PART I	PRELIMINARY PROVISIONS
PART II	AMENDMENT OF THE CAPITAL MARKETS AND SECURITIES ACT, (CAP.79)
PART III	AMENDMENT OF THE EXECUTIVE AGENCIES ACT, (CAP.245)
PART IV	AMENDMENT OF THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF) ACT, (CAP.147)
PART V	AMENDMENT OF THE ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY ACT, (CAP.413)
PART VI	AMENDMENT OF THE GAMING ACT, (CAP.41)

- PART VII AMENDMENT OF THE INCOME TAX ACT, (CAP.332)
- PART VIII AMENDMENT OF THE NATIONAL PARKS ACT, (CAP.282)
- PART IX AMENDMENT OF THE NGORONGORO CONSERVATION AREA ACT, (CAP.284)
- PART X AMENDMENT OF THE PORTS ACT, (CAP.166)
- PART XI AMENDMENT OF THE PUBLIC FINANCE ACT, (CAP.348)
- PART XII AMENDMENT OF THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP ACT, (CAP.103)
- PART XIII AMENDMENT OF THE PUBLIC PROCUREMENT ACT, (NO.7 OF 2011)
- PART XIV AMENDMENT OF THE ROAD AND FUEL TOLLS ACT, (CAP.220)
- PART XV AMENDMENT OF THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY ACT, (CAP.413)
- PART XVI AMENDMENT OF THE TANZANIA CIVIL AVIATION AUTHORITY ACT, (CAP.80)
- PART XVII AMENDMENT OF THE TANZANIA COMMUNICATION REGULATORY AUTHORITY ACT, (CAP.172)
- PART XVIII AMENDMENT OF THE TANZANIA FOOD, DRUGS AND COSMETICS ACT, (CAP.219)
- PART XIX AMENDMENT OF THE TANZANIA INVESTMENT ACT, (CAP.38)
- PART XX AMENDMENT OF THE TREASURY REGISTRAR (POWERS AND FUNCTIONS) ACT, (CAP.370)
- PART XXI AMENDMENT OF THE VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING ACT, (CAP.82)

9A.

PART III
AMENDMENT OF THE EXECUTIVE AGENCIES ACT,
(CAP.245)

Construction
Cap. 245

5. This Part shall be read as one with the Executive Agencies Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of
section 12

6. The principal Act is amended in section 12 by deleting subsection (4) and substituting for it the following:

Cap.348 “(4) Pursuant to section 11 of the Public Finance Act, every Agency shall remit ten percent of its annual gross revenue to the Consolidated Fund.”

PART IV
AMENDMENT OF THE EXCISE (MANAGEMENT AND TARIFF) ACT,
(CAP.147)

Construction
Cap 147

7. This Part shall be read as one with the Excise (Management and Tariff) Act hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment
of section 2

8. The principal Act is amended in section 2 by inserting in the appropriate alphabetical order the following new definition:

“telecommunication service” means a service of any description provided by a telecommunication company by means of any transmission, emission or reception of signs, signals, writing, images and sounds or intelligence or information of any nature, by wire, optical, visual or other electromagnetic means or systems, including-

(a) voice mail, data services, audio text services, video text services, radio paging;

(b) fixed telephone services including provision of access to and use of the public switched telephone network for the

- transmission and switching of voice, data and video, inbound and outbound telephone service to and from national and international destinations;
- (c) cellular mobile telephone services including provision of access to and use of switched or non-switched networks for the transmission of voice, data and video, inbound and outbound roaming service to and from national and international destinations;
 - (d) carrier services including provision of wired or wireless facilities to originate, terminate or transit calls, charging for interconnection, settlement or termination of domestic or international calls, charging for jointly used facilities including pole attachments, charging for the exclusive use of circuits, a leased circuit or a dedicated link including a speech circuit, data circuit or a telegraph circuit;
 - (e) provision of call management services for a fee including call waiting, call forwarding, caller identification, three-way calling, call display, call return, call screen, call blocking, automatic call-back, call answer, voice mail, voice menus and video conferencing;
 - (f) private network services including provision of wired or wireless telecommunication link between specified points for the exclusive use of the client;
 - (g) data transmission services including provision of access to wired or wireless facilities and services specifically designed for efficient transmission of data; and
 - (h) communication through facsimile, pager, telegraph and telex."

Amendment of
section 124

- 9.** Section 124 of the principal Act is amended-
- (a) by deleting subsection (3) and substituting for it

the following:

“(3) There shall be charged an excise duty on telecommunication service at the rate of 14.5% of the dutiable value”;

(b) in subsection (4) by-

(i) deleting the word “airtime” appearing in paragraphs (a) and (b) and substituting for it the words “telecommunication service”;

(ii) adding immediately after the words “mobile phone” appearing under paragraph (b) the words “fixed or wireless phone”;

(c) in subsection (5A) by deleting the figure “20” and substituting for it the figure “25”;

(d) by adding immediately after subsection (5B) the following new subsections:

“(5C) There shall be charged in addition to any other rates imposed under the law, an excise duty at the rate of 5 percent in respect of imported utility motor vehicle under HS code 87.01, 87.02 and 87.04 aged ten years or more from the year of its manufacture.

(5D) For the purposes of subsection (5C), the term “utility vehicle” shall not include the types of vehicles referred to under HS Codes 8701.10.00, 8701.90.00, 8702.10.11, 8702.10.21, 8702.10.91, 8702.90.11, 8702.90.21, 8702.90.91, 8704.10.10, 8704.21.10, 8704.22.10, 8704.23.10, 8704.31.10, 8704.32.10, 8704.90.10.”

Amendment
of the Fourth
Schedule

10. The principal Act is amended in the Fourth Schedule by introducing new excisable items and rates as follows:

Heading	Hs Code	Description	Unit	Old Excise Rate	New Excise Rates
20.09		Locally produced Fruit Juices (including grape must) and vegetable juices, unfermented and not containing added spirit, whether or not containing added sugar or other sweetening matter.	/	Tshs. 8 per Litre	Tshs. 9 per Litre
	2009.11.00	Imported Fruit Juices (including grape must) and vegetable juices, unfermented and not containing added spirit, whether or not containing added sugar or other sweetening matter.	/	Tshs.. 100 per Litre	Tshs. 110 per Litre
	2009.12.00				
	2009.19.00				
	2009.21.00				
	2009.29.00				
	2009.31.00				
	2009.39.00				
	2009.41.00				
	2009.50.00				
	2009.61.00				
	2009.69.00				
	2009.71.00				
	2009.79.00				
	2009.80.00				
	2009.90.00				
22.02		Water, including mineral waters and aerated waters, containing added sugar or other sweetening matter or flavoured, and other non-alcoholic beverages, not including fruit or vegetable juices of heading No.20.09.			

	2202.10.00	-Waters, including mineral waters and aerated waters, containing added sugar or other sweetening matter or flavoured.	/	Tshs. 83.00 per Litre	Tshs. 91.00 per Litre
	2202.90.00	---Other	/	Tshs. 83.00 per Litre	Tshs. 91.00 per Litre
22.03		<i>Beer made from malt</i>			
	2203.00.10	---Stout and porter	/	Tshs. 525.00 per Litre	Tshs. 578.00 per Litre
	2203.00.90	---Other	/	Tshs.525.0 0 per Litre	Tshs. 578.00 per Litre
22.04		Wine of fresh grapes, including fortified wines; grape must other than that of heading No.20.09.			
		--Sparkling wine			
	2204.10.10	--- With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 145.00 per Litre	Tshs. 160.00 per Litre
	2204.10.90	--Other	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.0 0 per Litre
		--Other wine; grape must with fermentation prevented or arrested by the addition of alcohol.	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.0 0 per Litre
	2204.21.10	---With the domestic grapes content	/	Tshs. 145 per Litre	Tshs. 160.00

	exceeding 75%			per Litre
2204.21.90	---Other	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.0 0 per Litre
2204.29.90	---Other	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.00 per Litre
2204.30.10	--Other grape must --With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 145 per Litre	Tshs. 160.00 per Litre
2204.30.90	--Other	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.00 per Litre
22.05	Vermouth and other wine of fresh grapes flavoured with plants or aromatic substances. --In containers holding 2/ or less			
2205.10.10	---With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 145 per Litre	Tshs. 160.00 per Litre
2205.10.90	---Other	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.00 per Litre
2205.90.10	--Other ---With the domestic grapes content exceeding 75%	/	Tshs. 145 per Litre	Tshs. 160.00 per Litre
2205.90.90	---Other	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.00 per Litre
22.06	Other fermented beverages (for example, cider, perry, mead) mixtures of fermented beverages			

	and mixtures of fermented beverages and non alcoholic beverages, not elsewhere specified or included.			
2206.00.10	--- Cider	/	Tshs. 1,614.00 per Litre	Tshs. 1,775.00 per Litre
2206.00.30	---Beer made from 100% local unmalted cereals	/	Tshs 310.00per Litre	Tshs 341.00 per Litre
2206.00.90	---others (including energy drinks and non alcoholic beverages) Undenatured ethyl alcohol of an alcoholic strength by volume of less than 80% vol; spirits, liqueurs and other spirituous beverages.	/	Tshs. 420.00per Litre	Tshs. 575.00 per Litre
2208.20.00	-Spirits obtained by distilling grape wine or grape marc	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
2208.30.00	-Whiskies	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
2208.40.00	-Rum and other spirits obtained by distilling fermented sugar-cane products	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
2208.50.00	-Gin and Geneva	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
2208.60.00	-Vodka	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
2208.70.00	-Liqueurs and cordials	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre

		-Other			
	2008.90.10	---Distilled Spirits (e.g. Konyagi, Uganda Waragi)	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
	2208.90.90	---Other	/	Tshs. 2,392.00 per Litre	Tshs. 2,631.00 per Litre
24.02		Cigars, cheroots, cigarillos and cigarettes, of tobacco or of tobacco substitutes.			
	2402.20.10	---Without filter tip and containing domestic tobacco contents exceeding 75%.	mil	Tshs. 8,210.00 per mil	Tshs. 9,031.00 per mil
	2402.20.90	---With filter tip and containing domestic tobacco exceeding 75%	mil	Tshs. 19,410.00 per mil	Tshs. 21,351.0 0 per mil
		---Other	mil	Tshs. 35,117.00 per mil	Tshs. 38,628.0 0 per mil
24.03		Other manufactured tobacco and manufactured tobacco substitutes; "homogenized" or "reconstituted" tobacco: tobacco extracts and essences.			
		--Smoking tobacco, whether or not containing tobacco substitutes in any proportion			
	2403.10.10	---Cut rag/filler	kg	Tshs. 17,736.00 per kg	Tshs. 19,510,0 0 per kg
27.10		Petroleum oils and oils obtained from			

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, yenye vifungu namba moja na mbili inahusu masuala ya utangulizi yaani, jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambapo sheria itaanza kutumika tarehe 1, Julai 2013.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Mamlaka ya Masoko ya Dhamana na Mitaji, Sura 79 kwa kufuta kifungu cha 9A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 vinavyorekebisha kupitia Muswada huu, vinavyoweka sharti kwa Mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka, Wakala na Taasisi za Serikali zitachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, inayojumuishwa kupitia Jedwali la marekebisho, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu, Sura 412 kwa kuongeza aya mpya ya (b) ili kubainisha kwamba mojawapo wa vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Elimu ni ushuru wa bidhaa wa asilimia 2.5 utakaotozwa kwenye huduma za simu kupitia Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Elimu Tanzania, matumizi ya fedha za Mfuko huu ni kwa ajili kuimarisha ubora na usawa katika sekta ya elimu Tanzania bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 12 kifungu kidogo cha (4) cha

Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 vinavyorekebisha kupitia Muswada huu, vinavyoweka sharti kwa Wakala za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka, badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka, Wakala na Taasisi za Serikali zitachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano, kama ilivyorekebisha kupitia Jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 katika vifungu namba mbili (2), 124, 125 na Jedwali la Nne kama ifuatavyo:-

- (a) Kurekebisha kifungu cha 2 ili kuingiza tafsiri ya maneno *electronic communication services* ndani ya Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa huduma za simu zitakazotozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia 14.5 kwa kujumuisha huduma zitakazotolewa kupitia simu za mezani na simu zisizotumia nyaya (*wireless phone*).
- (b) Kurekebisha kifungu cha 124, kifungu kidogo cha (3) ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa katika huduma zote zinazotolewa na simu za aina zote badala ya muda wa maongezi pekee (*airtime*), kutoka asilimia 12 ya sasa hadi kiwango cha asilimia 14.5.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiasi cha asilimia 2.5 cha ushuru huu kitawasilishwa katika Mfuko wa Elimu. Vile vile, wigo wa utozaji wa ushuru huu umeongezwa kwa kujumuisha huduma zote zitakazotolewa kupitia simu za mezani na simu zisizotumia nyaya (*wireless phones*).

- (c) Kufanya marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 124 kifungu kidogo cha 4(a) na (b) ili kubainisha kwamba, ushuru wa bidhaa wa asilimia 14.5 utatozwa katika huduma zote zinazotolewa kupitia simu za mikononi, mezani na simu zisizotumia waya.

- (d) Kurekebisha kifungu cha 124 kifungu kidogo cha (5A) ili kuongeza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji (*Non-Utility Motor Vehicles*) yenye umri wa zaidi ya miaka 10 kutoka asilimia 20 hadi asilimia 25. Hatua hii inalenga katika kupunguza uagizaji wa magari chakavu ambayo ni mojawapo ya chanzo cha ajali nchini na pia kulinda mazingira.
- (e) Kurekebisha kifungu cha 124 kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (5C) na (5D) ili kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia tano kwenye magari ya uzalishaji (*Utility Motor Vehicles*) yenye umri wa zaidi ya miaka 10 yanayotambuliwa katika *HS Code* 87.01, 87.02 na 87.04.

Hatua hii haitahusisha magari chini ya *HS Code* 8701.10.00 na *HS Code* 8701.90.00 ambayo kimsingi ni matrekta yaliyounganishwa; na magari yaliyounganishwa chini ya *HS Code* 8702.10.11; 8702.10.21, 8702.10.91; 8702.90.11, 8702.90.21; 8702.90.91; 8704.10.10; 8704.21.10; 8704.22.10; 8704.23.10; 8704.31.10 na 8704.32.10, 8704.90.10.

Lengo la kuanzisha kiwango hiki kipyua cha ushuru ni kupunguza uagizaji wa magari chakavu, kulinda mazingira na kupunguza ajali. Aidha, matrekta na magari yaliyounganishwa hayatatozwa ushuru huu kwa nia ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uunganishaji wa magari na hivyo kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

- (f) Kurekebisha kifungu cha 125 kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:-
 - (i) kufuta aya namba (d) na kuiandika upya ili kubainisha kwamba kampuni zinazotoa huduma zote zinazotolewa kupitia simu za mikononi, mezani na simu zisizotumia waya zitapaswa kulipa ushuru wa bidhaa wa asilimia 14.5.

- (ii) Kuongeza aya mpya ya (f) ili kubainisha kwamba taasisi za fedha, kampuni za simu na mabanki yatapaswa kulipa ushuru wa bidhaa wa asilimia 0.15 utakaotozwa kwenye huduma za kuhamisha fedha.
 - (iii) Kuongeza aya mpya ya (g) ili kubainisha kwamba kampuni ya simu ndiyo itakayopaswa kulipa ushuru wa bidhaa wa sh. 1,000 utakaotozwa kwenye kadi ya simu kwa mwezi.
- (g) Kurekebisha Jedwali la Nne kwa kurekebisha viwango maalum (specific rates) vya Ushuru wa bidhaa zisizokuwa za mafuta kama vile vinywaji baridi, mvinyo, pombe, vinywaji vikali, sigara na kadhalika kwa asilimia 10. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-
- (i) Vinywaji baridi, kutoka shilingi 83 kwa lita hadi shilingi 91 kwa lita sawa na ongezeko la shilingi nane tu kwa lita;
 - (ii) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (Juisi) yaliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini kutoka shilingi nane kwa lita hadi shilingi tisa kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi moja kwa lita;
 - (iii) Ushuru wa bidhaa kwenye Juisi iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini kutoka shilingi 100 kwa lita hadi shilingi 110 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 10 kwa lita;
 - (iv) Bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 310 kwa lita hadi shilingi 341 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 31 kwa lita;

- (v) Bia nyingine zote, kutoka shilingi 525 kwa lita hadi shilingi 578 kwa lita; yaani ongezeko la shilingi 53 kwa lita;
 - (vi) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango kinachozidi asilimia 75, kutoka shilingi 145 kwa lita hadi shilingi 160 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 15 kwa lita moja;
 - (vii) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,614 kwa lita hadi shilingi 1,775 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 161 kwa lita;
 - (viii) Vinywaji vikali, kutoka shilingi 2,392 kwa lita hadi shilingi 2,631 kwa lita; sawa na ongezeko la shilingi 239 kwa lita moja; na
 - (ix) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya chupa yanayotengenezwa viwandani hautaongezeka.
- (h) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-
- (i) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 8,210 hadi shilingi 9,031 kwa sigara elfu moja; sawa na ongezeko la senti 82 kwa sigara moja;
 - (ii) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 19,410 hadi shilingi 21,351 kwa sigara elfu moja; ikiwa ni ongezeko la shilingi moja na senti 94 kwa sigara moja;

- (iii) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 35,117 hadi shilingi 38,628 kwa sigara elfu moja; ikiwa ni ongezeko la shilingi tatu na senti hamsini kwa sigara moja;
 - (iv) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara (*cut filler*) kutoka shilingi 17,736 hadi shilingi 19,510 kwa kilo; na
 - (v) Ushuru wa Bidhaa kwa *Cigar* unabaki kuwa asilimia 30.
- (i) Kutoza ushuru wa bidhaa kwenye Gesi asilia inayotumika viwandani kwa kiwango cha Shilingi 0.39 kwa kila futi ya ujazo (Shs. 0.39 *per cubic feet*) badala ya shilingi 0.35;
 - (j) Kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 44 kwa bidhaa zinazohifadhi muziki na filamu (mfano *DVD, CD, VCD* na mikanda ya video na muziki iliyorekodiwa), badala ya shilingi 40.
 - (k) Kupitia Jedwali la Marekebisho, napendekeza kurekebisha viwango vya Ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya Petroli kama ifuatavyo: -
 - (i) Kurejesha ushuru wa bidhaa wa shilingi 215 kwa lita kwa mafuta ya Dizeli badala ya kiwango cha shilingi 217 kwa lita nilichopendekeza awali kupitia Hotuba ya Bajeti;
 - (ii) Mafuta ya Petroli kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 339 kwa lita hadi shilingi 400 kwa lita;
 - (iii) Mafuta ya taa kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 400.30 kwa lita hadi shilingi 475 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonyesha kwamba endapo ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya taa utabakia kuwa shilingi 400.30 kwa lita, tofauti ya

viwango vya kodi baina ya mafuta ya taa na dizeli itapanda kutoka shilingi 14.7 kwa lita hadi shilingi 129.7 kwa lita na tofauti baina ya mafuta ya taa na petroli itapanda hadi shilingi 312.7 kwa lita na hivyo kurejesha tatizo la uchakachujaji wa mafuta. Hali hii itaathiri sekta ya usafirishaji ambayo inategemea magari makubwa ya mizigo na sekta ya kilimo ambayo inatumia matrekta.

Aidha, mapato yataathirika kwa kuwa uagizaji wa mafuta ya dizeli na petroli utapungua na biashara ya mafuta na nchi jirani zinazoagiza mafuta kupitia Dar es Salaam itaathirika kama ilivyotokea hapo awali nchini Rwanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali imeibua vyanzo vipya vya mapato kwa kutoza ushuru kwenye bidhaa mpya na kuweka viwango vya ushuru kwa bidhaa hizo kama ifuatavyo:-

Kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia kati ya 10 hadi asilimia 25 kwenye bidhaa mbalimbali zinazozalishwa au kuingizwa nchini kama vile; Mazulia, vipodozi, mafuta ya kujipaka, bidhaa na mifuko ya ngozi, bunduki na risasi, boti za kifahari, ndege na helikopta.

Hata hivyo, kupitia Jedwali la marekebisho, napendekeza kwamba ndege na helikopta zitakazotozwa ushuru huu ni zile zitakazokuwa zikitumika kwa ajili ya starehe au michezo (*for pleasure and sports*). Ndege zinazotumika kwa ajili ya kusafirisha abiria (*commercial airline*) hazitatozwa ushuru huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia hapo, napendekeza kwamba ndege na helikopta zitakazotozwa ushuru huu ni zile zitakazokuwa zikitumika kwa ajili ya starehe na michezo (*for pleasure and sports*). Kwa maana nyingine ndege zinazotumika kwa ajili ya kusafirisha abiria yaani *commercial airlines* hazitatozwa ushuru huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuanzisha kiwango cha ushuru wa bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, zinazotambulika katika *HS Code* 94.03. Hatua hii inalenga katika

kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa samani kwa kutumia mbao zinazozalishwa hapa nchini. Aidha, hatua hii itachochea ukuaji wa ajira na kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti nilipendekeza kufuta ushuru wa bidhaa kwa kadi ya simu wa shilingi 1,450 kwa mwezi kama ulivyokuwa umependekezwa na Kamati ya Bunge. Hata hivyo, baada ya kupokea maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuhusu kurejesha ushuru huu ili kuweza kutumia mapato yake katika kupunguza kiwango cha ongezeko la kodi katika bidhaa za mafuta, kupitia Jedwali la Marekebisho, napendekeza kurekebisha kifungu cha 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 6C ili kuurejesha ushuru wa bidhaa kwa kadi za simu (*sim card*) kwa wamiliki wa simu za kiganjani/mkononi kwa kiwango cha sh. 1000 kwa kadi kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la marekebisho, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura, 147, kwa kuongeza kifungu kidogo cha 6A, ili kuanzisha ada ya uhawilisho wa fedha (*money transfer*) unaofanywa na mabenki, kampuni za simu na Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali. Kiwango cha ada kinachopendekezwa kutozwa ni asilimia 0.15 ya kiasi cha fedha kinachohawilishwa ndani au nje ya nchi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, punguzeni kelele.

Mheshimiwa Spika, aidha, kodi hii itatozwa kwenye uhamisho wa fedha wa kiasi kinachozidi sh. 30,000 na siyo kile kilicho chini ya sh. 30,000. Taasisi husika ni zile zinazohawilisha fedha mfano, Benki na taasisi zote za kifedha. Taasisi hizi zitatakiwa kukusanya kodi hii kwa niaba ya Serikali na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*).

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la marekebisho, napendekeza marekebisho katika kifungu cha 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 6B ili kuweka sharti kwamba, ushuru wa bidhaa utakaotozwa kwenye

uhamisho wa fedha hautatozwa kwenye malipo yanayohusu kodi za Serikali ikiwa ni pamoja na malipo ya mishahara, malipo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Serikali, malipo kati ya benki na benki na malipo yanayohusisha shughuli za kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita, inapendekeza kufuta kifungu cha 49A cha Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Utoaji wa Huduma za Maji, Nishati na Bidhaa za Petroli Sura 414, ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 vinavyorekebisha kupitia Muswada huu, vinavyoweka sharti kwa Mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka hii itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba, kama ilivyorekebisha kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura 41 kwa kurekebisha aya namba (4) ya kifungu cha 31, kifungu kidogo cha pili kwa kufuta neno *monthly* na kuweka neno *weekly* ili kubainisha kwamba ukokotoaji wa kodi ya *casino* utafanyika kwenye mapato ya kila wiki.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuwianisha kifungu hiki na matakwa ya kifungu cha 32(1) cha Sheria hii kilichoweka sharti la kukusanya kodi ya *casino* kwa kila wiki. Hivyo kuzuia *casino* kupunguza mapato yake kwa kuhamisha hasara ya wiki ya kwanza ya mwezi kwenda wiki ya pili au ya tatu ya mwezi husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane, kama ilivyorekebisha kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kurekebisha kifungu cha tatu kwa kuorodhesha ndani ya Sheria tafsiri ya maneno *money transfer commission, money transfer agent, contract area, mining area* na *petroleum agreement* ili kuwezesha utekelezaji wa baadhi ya

vifungu vya sheria hii vinavyohusu utozaji wa kodi kwenye huduma za kutuma fedha kwa njia ya simu, kampuni za madini na kampuni za utafutaji na uchimbaji wa bidhaa za petroli.

Mheshimiwa Spika, pili, kupitia Jedwali la marekebisho, kufuta marekebisho yaliyofanyika katika kifungu cha nne na aya ya tatu ya Jedwali la kwanza kuhusu kuongeza muda wa kutoza kodi ya mapato kwenye makampuni yanayoripoti hasara ya kikodi mfululizo. Kodi hiyo itaendelea kutozwa kwa makampuni yanayoripoti hasara mfululizo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kurekebisha kifungu cha 11 na 19, kifungu kidogo cha nne ili kuzuia kampuni za utafutaji au uchimbaji wa mafuta na madini zenye mgodi au eneo la uchimbaji mafuta zaidi ya moja, kuchanganya gharama au hasara za eneo moja kwenye mapato ya mgodi na eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kupanua wigo wa kodi kwa kupata mapato halisi ya kila eneo la utafutaji au uchimbaji mafuta au madini.

Mheshimiwa Spika, nne, kufuta kifungu cha 98, kifungu kidogo cha (3) na kurekebisha kifungu cha 80A kwa kuweka kifungu kipya kidogo cha (3) ili kuweka adhabu kwa wafanyabiashara na walipa kodi watakaokiuka kifungu cha 80A kilichoweka sharti la kutumia mashine za kielektroniki (*EFD*) katika kutoa stakabadhi na kuhifadhi kumbukumbu za mauzo ya kila siku. Adhabu zinazopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

- (1) Kwanza, faini ya kiasi cha asilimia tano ya thamani ya bidhaa zitakazouzwa pasipo kutolewa kwa stakabadhi ya mashine za *EFD* kwa mkosaji wa mara ya kwanza.
- (2) Pili, faini ya kiasi cha asilimia 10 ya thamani ya bidhaa zitakazouzwa pasipo kutolewa kwa stakabadhi ya mashine za *EFD*, kwa mkosaji wa mara ya pili.
- (3) Tatu, adhabu ya faini ya shilingi milioni tatu au kifungo kisichozidi miaka mitatu, kwa mkosaji wa mara ya tatu atakayekiuka sharti la matumizi ya mashine za kutoa

stakabadhi za kielektroniki au kutotoa stakabadhi ya malipo ya eletroniki.

Mheshimiwa Spika, tano, aidha, marekebisha husika yanapendekeza kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa *TRA*, kupitia kanuni kuweka utaratibu wa ukusanyaji na utozaji wa adhabu husika. Kurekebisha kifungu cha 82 kifungu kidogo kipya cha pili na kufuta aya (namba q) iliyopo katika Jedwali la Pili la Sheria hii kwa kufuta msamaha wa kodi ya zuio kwenye ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakazi (*non-resident*) ambapo huduma hii itaanza kutozwa kodi ya zuio. Hatua hii inalenga katika kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sita, kurekebisha kifungu cha 83 ili kukidhi mambo yafuatayo:-

- (i) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 15 kwenye huduma za ufundi na utawala (*technical and management services*) zinazotolewa na walipa kodi wasio wakazi (*non residents*) kwenye biashara ya madini.
- (ii) Kutoza kodi ya zuio ya asilimia 10 kwenye kamisheni (*commission*) inayolipwa katika kutuma fedha kwa njia ya simu za mkononi. Kodi hiyo itakayokusanywa na kampuni za simu itatozwa kwa wakala wanaotoa huduma za kutuma fedha kupitia simu za mkononi.
- (iii) Kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia tano kwenye malipo yatokanayo na huduma mbalimbali kama vile huduma za ushauri wa kitaalam na nyinginezo (*Consultancy services and other services*) zinazotolewa na wakazi (*residents*) na wasio wakazi. Lengo la hatua hii ni kudhibiti na kulinda mapato ya Serikali kwa kupitia huduma hii.

Mheshimiwa Spika, saba, kurekebisha kifungu cha 96 ili kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa *TRA* kuongeza muda wa kurekebisha (*adjust*) makadirio ya kodi yanayohusiana na *transfer pricing arrangement* kutoka kipindi cha miaka mitatu hadi sita.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kupata mapato endapo itabaini kuwepo kwa ukwepaji kodi kwenye baadhi ya kampuni.

Mheshimiwa Spika, nane, kufuta kifungu cha 83A na kukiandika upya ili kutoza kodi ya zuio kwenye bidhaa zinazonunuliwa na Serikali na Taasisi zake kwa kiwango cha asilimia mbili pasipo kuzingatia endapo muuzaji wa bidhaa ana Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN). Taasisi za Serikali zitakazotozwa kodi hii ni zile zinazotegemea bajeti ya Serikali pekee au kwa kiwango kikubwa katika uendeshaji wa shughuli zake. Lengo la hatua hii ni kudhibiti na kulinda mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tisa, kurekebisha Jedwali la kwanza ili kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 14 hadi asilimia 13 na kurekebisha viwango vya kodi ya mapato ya ajira katika Jedwali la Kwanza. Hatua hii pamoja na kutoa nafuu ya kodi kwa mfanyakazi itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 126.

Mheshimiwa Spika, kumi, ni kurekebisha Jedwali la Tatu ili kuruhusu uchakavu wa asilimia moja kwa vifaa vitakavyotumika katika utafutaji wa madini na mafuta.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa, pamoja na marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 10(7), inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282 kwa kufuta kifungu cha 10A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 vinavyorekebishwa kupitia Muswada huu, vinavyoweka sharti kwa Mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka, badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Hifadhi ya Taifa itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro, Sura 284 kwa kufanya marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 13(7) na

kufuta kifungu cha 13A ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 vinavyorekebisha kupitia Muswada huu, vinavyoweka sharti kwa taasisi za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka, badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho hifadhi ya ngorongoro itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja, inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 74 cha Sheria ya Bandari, Sura 166 kwa kufuta vifungu vidogo vipya vya (4) na (5) ili kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 vinavyorekebisha kupitia Muswada huu, vinavyoweka sharti kwa mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka, badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka ya Bandari itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili, kama ilivyorekebisha kupitia Jedwali la marekebisho, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 11 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kwa kuongeza vifungu vidogo vya (2) na (3) ili kwanza, kuweka sharti kwa Wakala, Mamlaka na Taasisi za Serikali kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, pili, kumpa Mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kutangaza kupitia Tangazo la Serikali, Taasisi, Wakala na Mamlaka zitakazostahili kuchangia mapato yake katika Mfuko Mkuu wa Serikali, taratibu na kipindi cha kuwasilisha mapato husika kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Tatu, kuweka adhabu kwa Taasisi zitakazokiuka masharti ya kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi kwa Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Taasisi itakayoshindwa kuwasilisha mchango wake kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali itatozwa adhabu ya malipo ya asilimia tano ya mapato iliyopaswa kuwasilisha pamoja na kulipa kulipa asilimia 10 ya mchango stahili.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu, kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 15 cha Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi, Sura 103 kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuongeza kifungu kidogo cha tatu ili kuondoa sharti la ushindani...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunaomba umalize kuisoma hiyo hotuba kwa sababu ni muhimu sana kwa wananchi kusikia. Kwa hiyo isome mpaka umalize.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu, kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 15 cha Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi, Sura 103 kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuongeza kifungu kidogo cha tatu ili kuondoa sharti la ushindani kwa zabuni za miradi ya *Public Private Partnership* iliyoibuliwa na wazabuni wenyewe *unsolicited PPP Proposals*.

Pili, kuongeza aya ndogo ya (4) ili kubainisha kwamba taratibu zitakazotumika kuwapata wazabuni wa *unsolicited Public Private Partnership Proposals* zitabainishwa kupitia Kanuni zitakazotayarishwa chini ya Sheria ya Ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza urasimu na kuvutia wawekezaji katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya kuboresha uchumi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne, kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 80 cha Sheria ya Ununuzi

wa Umma ya mwaka 2011, kwa kurekebisha kifungu kidogo cha kwanza na kuongeza kifungu kidogo kipy cha pili ili Kwanza, kuwezesha zabuni za *unsolicited Public Private Partnership Proposals* kutohusika na utaratibu wa ushindani.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano, inapendekeza marekebisho ya Jedwali la Pili la Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220 ili Kuongeza kiwango cha Ushuru wa mafuta (*fuel levy*) kutoka sh. 200 kwa lita hadi sh. 263 kwa lita, sawa na ongezeko la sh. 63 kwa lita. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Mfuko wa Barabara nchini ili kuuwezesha kugharamia ujenzi na matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita, pamoja na marekebisho ya kiujumla na kiuandishi, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 47 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura 413 kwa kufuta vifungu vidogo vya (6) na (7) ili kuwezesha *SUMATRA* kuchangia kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348, badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho mamlaka ya *SUMATRA* itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 47 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga, Sura 80 kwa kufuta vifungu vidogo vya (6) na (7) ili kuwezesha Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga kuchangia kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka hii itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 54 cha Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma ya Mawasiliano, Sura 172, kwa kufuta

vifungu vidogo vya (6) na (7) ili kuwezesha TCRA kuchangia kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348, badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho mamlaka hii itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tisa, pamoja na marekebisho ya kiujumla na kiuandishi, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha saba, Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Ubora wa Chakula, Madawa na Vipodozi, Sura 219 kwa kufuta kifungu cha 4A ili utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11 vifungu vidogo vya (2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348, vinavyoweka sharti kwa mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka hii itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini, inapendekeza marekebisho katika vifungu vya 19 na 20 vya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 ili:-

Kwanza, kuziondoa baadhi ya bidhaa kwenye orodha ya kupata msamaha. Bidhaa hizo ni zile ambazo hazina uasilia wa kuwa bidhaa za mtaji (*capital goods*) kama vile vifaa vya ofisi, samani, sukari, vinywaji (viburudisho), bidhaa za mafuta ya petroli, magari madogo (*Non Utility Motor Vehicles*), viyoyozi, majokofu, na vifaa vya kielektroniki, mashuka, vijiko na vikombe.

Pili, kupunguza msamaha wa kodi uliokuwa unatolewa kwenye bidhaa zinazotambulika kama *deemed capital goods* kutoka asilimia 90 hadi asilimia 75. Mwekezaji sasa atatakiwa kulipa asilimia 25 ya ushuru wa forodha unaopaswa kutozwa kwenye bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Moja, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Msajili wa Hazina kwa kurekebisha

kifungu cha 8(1) kwa kuongeza jukumu kwa Msajili wa Hazina kuhakikisha Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina yanawasilisha kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya mwaka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa utaratibu utakaowekwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha kupitia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82 ili, kwanza, kurekebisha kifungu cha 14(2) ili kupunguza tozo ya kuendeleza mafunzo ya ufundi stadi (*Skills Development Levy "SDL"*) kutoka kiwango cha sasa cha asilimia sita hadi kiwango cha asilimia tano. Hatua hii itasaidia kuongezeka kwa ajira katika sekta binafsi.

Pili, kuweka sharti kwa Taasisi za Serikali zisizotegemea bajeti ya Serikali katika kujiendesha, kulipa tozo hii ili kuongeza wigo na mapato kwa ajili ya kugharamia elimu ya mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tatu, kama ilivyorekebisha kupitia Jedwali la marekebisho, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:-

Kurekebisha Jedwali la Kwanza kwa kufuta aya ya 17 ili kuondoa utozaji Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye nguo zinazozalishwa na Viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, kurejesha aya ya 14 ya Jedwali la Pili, (linalohusu bidhaa na huduma zilizosamehewa kodi (*exempt supplies and imports*) ili kurejesha msamaha wa VAT unaotolewa kwenye huduma za utalii katika huduma zifuatazo: (i) *Tourist Guiding* (ii) *Game driving* (iii) *Water Safaris* (iv) *Animal or bird watching* (v) *Park fees* (vi) *Tourist Charter Services* (vii) *Ground Transport*.

Mheshimiwa Spika, kurekebisha Jedwali la Tatu; (linalotoa nafuu maalum wa kodi, *VAT Special relief* kwa watu na Taasisi mbalimbali) kwa kuongeza aya mpya ya 33 ili kutoa nafuu maalum ya VAT kwa wazalishaji wa nguo nchini zinazozalishwa kwa pamba

ya ndani kwa bidhaa na huduma zitakazotumika kwenye uzalishaji wa nguo hizo.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza VAT kwa kiwango cha asilimia sifuri, chini ya Jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Hivyo basi, mzalishaji wa nguo zinazotumia pamba ya hapa nchini hatalipa VAT kwenye manunuzi ya pamba, umeme na malighafi za uzalishaji wa nguo hizo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika Hotuba ya Bajeti zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Matangazo ya Serikali (*Government Notices*) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika. Hatua hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuongeza viwango vya Ada ya mwaka ya leseni za Magari (*Annual Motor vehicle Licence Fee*) kama ifuatavyo: -

- (i) Gari lenye ujazo wa Injini 501.cc – 1500.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000;
- (ii) Gari lenye ujazo wa Injini 1501.cc – 2500.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 150,000 hadi shilingi 200,000;
- (iii) Gari lenye ujazo wa Injini zaidi ya 2501.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 200,000 hadi shilingi 250,000.
- (iv) Magari yenye ujazo wa Injini chini ya 501cc yataendelea kutozwa Ada ya leseni za magari ya kiasi cha sh. 50,000 kinachotumika hivi sasa. Hata hivyo ada hii haitahusisha pikipiki na bajaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia ada hii haitahusisha pikipiki na bajaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuwawezesha vijana wanaomiliki na wanaotumia vyombo hivyo vya usafiri wapate unafuu wa punguzo hili na hivyo kujiongezea kipato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua hii itatekelezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya mambo ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, kuanzisha Tozo ya mafuta (*petroleum fee*) ya sh. 12 kwa lita kwa mafuta ya dizeli na sh. 50 kwa lita kwa mafuta ya petroli. Tozo hii itakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ambapo Mapato yatakayokusanywa kutoka kwenye tozo hiyo yatatumika kugharamia mahitaji ya Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*) katika kusambaza umeme vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua hii itatekelezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Nishati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, kuanzisha ada ya kutumia mtambo wa kutambua idadi ya miamala ya simu (*traffic monitoring system*) kwa watumiaji wa mitambo hiyo ya *TCRA*.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itatekelezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mawasiliano kupitia Tangazo katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, nne, Kubadili viwango vya ada mbalimbali za mifugo ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mifugo atahusika katika kutoa Matangazo ya Serikali yenye viwango vipya vya ada hizo.

Mheshimiwa Spika, tano, kuanzisha tozo kwenye huduma za usafishaji wa mazingira (*carbon trade*). Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mazingira atahusika katika kutangaza viwango vya tozo husika katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, sita, marekebisho ya ushuru wa forodha kwa bidhaa mbalimbali kama ilivyotangazwa kwenye Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/14, yatatekelezwa kupitia Matangazo kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu Bajeti ya mwaka wa fedha

2013/2014, ambayo tayari yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ambayo Waheshimiwa Wabunge mliipitisha hapa Bungeni tarehe 24 Juni, 2013. Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wote, muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuhalalisha kisheria Bajeti iliyokwishapitishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge hoja hii imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili atoe maoni ya Kamati yake.

MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa mujibu wa Kanuni ya 88 (1) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2013, niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2013 *(The Finance Act, 2013)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa; Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum; pamoja na Kaimu Katibu, Mkuu Dkt. Likwelile; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano mzuri wa kuboresha marekebisho ya Sheria husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda pia kuwapongeza wadau wote waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni na ushauri wao ambao kwa kiasi kikubwa umesaidia katika kuupitia na kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada; itakumbukwa kwamba tarehe 13 Juni, 2013, Waziri wa Fedha aliwasilisha Bungeni

Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kuipa uwezo wa kupata mapato ya kugharamia Bajeti yake kwa Mwaka huu wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2013, pamoja na marekebisho yake kama yalivyobainishwa katika jedwali la marekebisho, lengo lake ni kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Hivyo Bunge lako Tukufu linaombwa kuhalalisha kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali zitakazoanza kukusanywa na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 kwa mujibu wa Sheria ya *The Provisional Collection of Taxes Act*.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa nyakati tofauti imefanya vikao na Wadau mbalimbali wanaoguswa na mapendekezo ya Serikali yaliyomo katika Muswada huu na kujadili maeneo husika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekutana na Wawakilishi wa Sekta Binafsi (*TPSF*), Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Jumuiya ya Watoa Huduma wa Simu za Mkononi (*MOAT*), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) na Wadau wengine mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Watendaji wa Wizara kuhusu marekebisho ya Sheria ishirini na mbili zilizopo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya Kamati ni matokeo ya mashauriano hayo na naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada Wa Sheria Ya Fedha ya mwaka 2013. Marekebisho ya Sheria mbalimbali zilizoanzisha Wakala, Taasisi na Mashirika ya Umma; sehemu ya Pili, Nne, Sita, Saba, Tisa, Kumi, Kumi na Moja, Kumi na Sita, Kumi na Saba, Kumi na Nane na Kumi na Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu kadhaa vya Sheria mbalimbali zilizoanzisha Wakala, Mamlaka za

Umma, kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa matakwa ya kifungu cha 11(2) na (3) vya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348, vinavyoweka sharti kwa mamlaka za Serikali kuwasilisha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha asilimia 10 ya mapato ghafi ya kila mwaka badala ya utaratibu wa sasa ambapo Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha amepewa mamlaka ya kufanya uamuzi kuhusu kiwango cha mchango wa mapato ambacho Mamlaka, Wakala na Taasisi za Serikali zitachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono pendekezo hili kwa kutambua kuwa yapo Mashirika, Taasisi na Mamlaka za Serikali ambazo zimekuwa zikipata faida kubwa bila kuchangia kikamilifu katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kamati inaafiki kuwa mapato ghafi ya Taasisi na Mashirika haya ndiyo yawe msingi wa kukokotoa asilimia kumi itakayopelekwa katika Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inapendekeza kuwa kwa kuwa suala hili sasa limewekwa vizuri kisheria, kuwepo na ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kuwa kila anayehusika na sheria hii anatekeleza wajibu wake na taratibu za kinidhamu zifuatwe kwa Shirika au Taasisi itakayoshindwa kutekeleza agizo hili kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia hairidhishwi na mwenendo wa baadhi ya Wakala, Mashirika na Taasisi za Umma ambazo zimekuwa zikitekeleza shughuli zaidi ya majukumu yake ya msingi *core business* na hivyo kuyafanya yawe na gharama kubwa za kimtaji. Mfano wa shughuli hizi, ni kama vile ujenzi wa majumba ya vitega uchumi na kadhalika, shughuli ambayo ingeweza kuachiwa Shirika la Nyumba pekee. Kamati ina maoni kuwa, Mashirika na Taasisi hizi yatumie fedha za ziada kuboresha huduma zao za msingi na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kadhaa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 katika kifungu namba 124 na Jedwali la Nne kama kwa kubadili tafsiri ya maneno *telecommunication services* ndani ya Sheria hii kwa lengo la kupanua wigo wa huduma za simu zitakazotolewa ushuru wa bidhaa kwa kujumuisha huduma zitakazotolewa kupitia simu za mezani na simu zisizotumia waya.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua nzuri inayopanua wigo wa kodi kutoka katika mitandao ya simu. Hivyo, Kamati imefarikwa kuona Serikali imebadili tafsiri ya maneno hayo na kuweka maneno *electronic communication*. Tafsiri hii iliyopanuliwa itaweza kubeba maana inayokusudiwa ambayo ni mawasiliano yote yanayotumia njia za kielektroniki yakijumuisha mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, pia kifungu kidogo cha tatu, ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa katika huduma zote zinazotolewa na simu za aina zote badala ya muda wa maongezi pekee *airtime*, kutoka asilimia 12 ya sasa hadi kiwango cha asilimia 14.5. Kiasi cha asilimia 2.5 cha ushuru huu ni kwa ajili ya kuchangia katika Mfuko wa Elimu ili kugharamia elimu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali katika hatua hii ni zuri. Hata hivyo, kwa kuwa tayari wigo wa kodi umeongezeka kwa kutoza kodi huduma zote, yaani muda wa maongezi na huduma nyingine za ziada, Kamati ina maoni kwamba kiasi hicho cha asilimia 2.5 kigawanywe katika utaratibu unaoeleweka ili kiweze kutekeleza azma hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, moja ya huduma zinazotolewa na mitandao ya simu ni kutuma na kupokea fedha. Huduma hizi zimekuwa ni msaada sana hasa kwa wananchi wa hali ya chini ambao hawana sifa za kuhudumiwa na benki, lakini pia zimepanua wigo wa huduma za kifedha hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, Kamati inatoa angalizo kwamba, ushuru wa bidhaa usihusishe huduma za kutuma na kupokea fedha, kwani kwa kufanya hivyo kutaongeza sana gharama ya huduma hii na hivyo kumfanya mwananchi wa hali ya chini kuumia zaidi kwa kuwa hana mbadala wa huduma za kifedha kwenye mabanki yetu.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii ya Muswada, Kamati imebaini kuwa kuna uwezekano wa kuwepo kwa utozaji kodi mara mbili (*double taxation*) katika Kifungu 8(d) cha Muswada huo iwapo mtu ataunganishwa simu kutoka kampuni moja kwenda nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati imeshauri kuwa ni vema eneo hili likaangaliwa upya ili kusiwepo na *double taxation* hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania ni *signatory* wa Mkataba wa Kimataifa *Merlbone Treaty*.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Kamati la kurekebisha kifungu kidogo cha 5A, ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji (*Non-Utility Motor Vehicles*) yenye umri wa zaidi ya miaka 10 kutoka asilimia 20 hadi 25 na kuongeza vifungu vidogo vipya vya 5C na 5D ili kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia tano kwenye magari ya uzalishaji (*Utility Motor Vehicles*) yenye umri zaidi ya miaka 10 halikuafikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii lilikuwa ni kupunguza uingizaji wa magari chakavu ambayo ni mojawapo ya chanzo cha ajali nchini, lakini pia kulinda uchafuzi mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua dhamira ya Serikali katika kulinda mazingira na pia kupunguza ajali za barabarani. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba, ili kuwasadia wananchi kuachana na ununuzi wa magari chakavu ya aina zote, ni lazima Serikali iandae mazingira kwa wananchi wake yatakatayowezesha kununua magari mapya.

Mheshimiwa Spika, hali hii inawezekana iwapo Serikali itapunguza kiwango cha kodi ya magari mapya kwa kadiri itakavyowezekana ili kuleta unafuu kwa wanunuzi wa magari hayo. Kwa kuwa Serikali haikuafiki pendekezo hili, Kamati inapendekeza kwamba, kwa sasa Serikali isitishie kuongeza kodi katika magari chakavu na badala yake iandae mazingira ya kupunguza kodi ya magari mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Viwango vya Kodi katika mafuta; kuhusu kodi katika mafuta, Waziri wa Fedha alijulisha Kamati kuwa Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika viwango vya kodi katika mafuta kama ifuatavyo:-

- (i) Mafuta ya taa kutoka sh. 400 kwa lita hadi sh. 475 kwa lita;

(ii) Mafuta ya Dizeli kutoka sh. 530 kwa lita hadi sh. 490 kwa lita; na

(iii) Mafuta ya Petroli hayana ongezeko, hivyo inabakia kiasi cha sh. 713 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kwa viwango hivi vya kodi na kwa mujibu wa takwimu za *EWURA*, Serikali itakusanya kiasi cha sh. 1,285,051,409,150.17. Kiwango hiki ni pungufu kwa takribani sh. 56,714,835,771.36 ikilinganishwa na mapendekezo yaliyotolewa awali na Waziri wa Fedha katika Hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kupunguza mzigo kwa wananchi unaotokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta, Kamati inashauri Wizara ya Fedha kuangalia upya viwango hivi vya ongezeko la kodi. Hivyo, Kamati inapendekeza viwango vya ongezeko kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 1: **Makadirio yanayopendekezwa na Waziri wa Fedha**

PRODUCT	Sold Volume (July 12- May 13)	Expected Sales	Excise Duty	Fuel Levy	Petroleum Levy	Total Taxes	Expected Total
Motor Spirit Premium	623,618,724.00	734,736,242.09	400.00	263.00	50.00	713.00	523,866,940,610.17
Illuminating Kerosene	72,509,483.00	85,429,354.52	475.00	-	-	475.00	40,578,943,397.00
Automotive Gas Oil	1,248,214,408.00	1,470,623,520.70	177.00	263.00	50.00	490.00	720,605,525,143.00
TOTAL	1,944,342,615.00						1,285,051,409,150.17

(i) Mafuta ya taa kutoka shilingi 400.30 kwa lita hadi shilingi 475 kwa lita;

(ii) Mafuta ya Dizeli kutoka shilingi 530 kwa lita hadi shilingi 490 kwa lita; na

(iii) Mafuta ya Petroli kutoka shilingi 713 kwa lita hadi shilingi 652 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inayopendekezwa na Kamati itaiingizia Serikali kiasi cha sh. 1,240,232,498.382.68. Kiasi hiki ni pungufu ikilinganishwa na mapendekezo ya Waziri wa fedha kwa sh. 44,818,910,767.49. Jedwali Na. 2 linaonesha mchanganuo wa viwango hivyo.

Jedwali Na. 2 : Makadirio yanayopendekezwa na Kamati ya Bajeti

PRODUCT	Sold Volume (July 12- May 13)	Expected Sales	Excise Duty	Fuel Levy	Petroleum Levy	Total Taxes	Expected Total
Motor Spirit Premium	623,618,724.00	734,736,242.09	339.00	263.00	50.00	652.00	479,048,029,842.68
Illuminating Kerosene	72,509,483.00	85,429,354.52	475.00	-	-	475.00	40,578,943,397.00
Automotive Gas Oil	1,248,214,408.00	1,470,623,520.70	177.00	263.00	50.00	490.00	720,605,525,143.00
TOTAL	1,944,342,615.00						1,240,232,498,382.68

Mheshimiwa Spika, msingi wa pendekezo la Kamati ni kupunguza ongezeko la kodi ili kutoa nafuu ya gharama ya maisha kwa wananchi na pia kupunguza mfumuko wa bei utokanao na ongezeko la bei kutokana na hatua hiyo pamoja na uchakachujaji.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana katika Jedwali la pili, ushuru wa bidhaa haujaongezeka katika aina zote za mafuta. Aidha, mapendekezo ya marekebisho yaliyofanywa na Kamati hayajagusa viwango vya tozo *Fuel and Petroleum Levy* kutokana na umuhimu wake katika kuchangia kwenye uboreshaji wa huduma za umeme vijijini na ujenzi wa barabara. Kiasi cha fedha kinachopungua kutokana na pendekezo hili kitafidiwa na hatua mbalimbali za Mapato zitakazopendekezwa na Kamati muda mfupi ujao katika taarifa hii na mapendekezo hayo yaliwasilishwa Serikalini kupitia Waziri mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoza ushuru wa bidhaa katika vyombo vya angani mfano, ndege, helikopta na kadhalika, kwa

kiwango cha asilimia 20. Kamati ina maoni kuwa ushuru huu uondolewe kwa kuwa unaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ya usafiri wa anga, utalii na uchumi kwa ujumla pamoja na kuongeza gharama za ufanyaji biashara, *cost of doing business* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga si anasa tena, hivyo Serikali ione umuhimu wa kutotoza ushuru huu katika sekta hii, kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 20 katika vyombo vya usafiri wa anga, ni kinyume na mategemeo ya maono Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 yaani, *Vision 2025* ambayo inalenga kuleta maendeleo katika sekta ya usafiri wa anga hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia pia mapendekezo mengine yote ya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na baada ya mashauriano ya kina na Serikali, Kamati iliyaafiki.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Sehemu hii inapendekeza kufuta kifungu cha 98(3) na kurekebisha kifungu cha 80A kwa kuweka kifungu kipya kidogo cha tatu ili kuweka adhabu kwa wafanyabiashara na walipa kodi watakaokiuka kifungu cha 80A kilichoweka sharti la kutumia mashine za kielekroniki katika kutoa stakabadhi na kuhifadhi kumbukumbu za mauzo ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na utaratibu uliowekwa wa kutoa adhabu kwa wafanyabiashara wanaokiuka utaratibu. Tunaomba wafanyabiashara popote nchini wajaribu kuzingatia sheria hii. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa bado utaratibu wa adhabu haujakaa sawa hasa ikizingatiwa kuwa upo uwezekano kwa mfanyabiashara kurudia kutenda kosa kwa kuwa kiwango cha adhabu kwa kurudia mara tatu kwa kosa hilo hilo kinaweza kuwa kidogo kuliko kiwango cha adhabu ya mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kiwango hiki kiongezwe ili kuleta nidhamu katika matumizi ya mashine hizi. Aidha, Kamati inawasihi wananchi wote kuhakikisha wanadai stakabadhi kila wanaponunua huduma ili kusaidia jitihada za Serikali katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, badiliko katika Jedwali la pili kifungu (q) cha Sheria hiyo kinachopendekezwa kuondolewa ili kufuta msamaha wa kodi ya zuio kwa malipo ya ukodishaji wa ndege yanayolipwa kwa makampuni ya nje kutoka kwa makampuni yanayofanya biashara ya ndege nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hili, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kukusanya kodi katika maeneo mbalimbali. Pamoja na kwamba eneo hili ni mapato kwa mwenye ndege, Kamati ina maoni kwamba, sekta ya usafiri wa anga nchini bado ni changa. Kiasi kinachotegemewa kukusanywa kwa kodi hii ni shilingi bilioni 4.3 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kurejeshwa kwa kodi hii, ipo hatari kubwa ya kudumaza ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga nchini. Gharama itokanayo na urejeshwaji wa kodi hii ni kubwa ikilinganisha na kiasi kinachotegemewa kukusanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali ione umuhimu wa kuahirisha kurejesha kodi hii kwa sasa kuruhusu sekta hii ikue. Kurejeshwa kwa kodi hii kunaweza kufanyika katika miaka mingine ya usoni. Kufanya hivi kutasaidia kukuza sekta hii ambayo kwa sasa ina matatizo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Namba saba (7) ya mwaka 2011; Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu marekebisho katika kifungu cha 15 kwenye Sheria ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi kwa kuongeza kifungu kidogo cha tatu ili kuondoa sharti la ushindani kwa zabuni za miradi yote ya ubia iliyoibuliwa na Wazabuni wenyewe *Unsolicited PPP Proposals*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011, Kamati inakubaliana na Serikali kurekebisha kifungu cha 80 kwa kuongeza kifungu kipya cha pili kuwezesha zabuni za *unsolicited PPP Proposals* kutohusika na utaratibu wa ushindani na hivyo taratibu zote za ushindani zitabainishwa kupitia Kanuni zitakazotayarishwa chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na hotuba ya bajeti ya Serikali kwa kuunganisha vitengo vinavyojihusisha na masuala ya PPP vilivyopo kwenye Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Wizara ya Fedha kuwa kitengo kimoja. Hii itasaidia kukidhi yale malengo ya kupunguza urasimu na kuongeza uharaka wa kutekeleza miradi hii. Hivyo, Kamati inaona kuwa marekebisho ya sheria hizi mbili:-

Moja, yatasaidia kuvutia wawekezaji katika miradi ya maendeleo kwa madhumuni ya kukuza uchumi wa nchi pamoja na kupunguza urasimu wa kupata wawekezaji husika.

Mbili, mapendekezo haya yatafanya wawekezaji makini waliokwihakamilisha michanganuo ya miradi na ambao wapo tayari wana mitaji kujitokeza kwa wingi na kuwasilisha mapendekezo yao Serikalini kwa lengo la kupewa fursa ya kutekeleza miradi hiyo kwa ubia.

Tatu, utaratibu huu utasaidia kuhamasisha uwekezaji wa ubia kwenye miradi ambayo Serikali haijabainisha kwa ajili ya uwekezaji kwa ubia *unidentified investment opportunities*.

Nne, Serikali iweke vigezo muhimu vitakavyofafanua ni miradi ipi itatimiza sifa za kuwa *unsolicited bids* na hivyo kutoingizwa katika utaratibu wa ushindani.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38. Serikali inapendekeza kufanyia marekebisho vifungu vya 19 na 20 vya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 ili:-

Moja, kuziondoa baadhi ya bidhaa kwenye orodha ya kupata misamaha, bidhaa hizo ni zile ambazo hazina uasilia wa kuwa bidhaa za mtaji *Capital goods*; na

Pili, kupunguza msamaha wa kodi uliokuwa unatolewa kwenye bidhaa zinazotambulika kama *deemed capital goods* kutoka asilimia 90 hadi 75 na hivyo sasa mwekezaji atatakiwa kulipa asilimia 25 ya ushuru wa forodha unaopaswa kutozwa kwenye bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata ufafanuzi toka kwa wadau kuwa, kwa mujibu wa orodha ya Kimataifa ya *Capital Goods ya Brussels*, sasa *H.s Code*; vifaa vinavyostahili kuorodheshwa na Serikali kama *Deemed Capital Goods* ni vile vinavyohusisha vifaa vya mitambo na mashine za uzalishaji bidhaa viwandani tu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali iliamua kuvipa hadhi baadhi ya vifaa kuwa *Deemed Capital Goods* kwa kuwa vinatumika kama mtaji katika kujenga miradi ya sekta za kipaumbele kama kilimo, utalii, miundombinu, usafirishaji, elimu na kadhalika zinazosaidia kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, vifaa vinavyopendekezwa kufutwa kwenye orodha kimsingi havipo, wawekezaji hawasamehewi vifaa hivi kupitia *Deemed Capital Goods* kwa kuwa si vifaa vya mtaji. Kamati inashauri kuwa wawekezaji waliosamehewa kodi hizi hapo awali kwa utaratibu wa *Deemed Capital Goods* wabainishwe na kuchunguzwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo Kamati haikubaliani na pendekezo hili kwa kuwa kuna baadhi ya vifaa vinavyohusika kwenye shughuli za utalii na mahoteli vimeshasamehewa kodi kupitia Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki, 2004 *5th Schedule*.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali iwe inajipanga na kufanyia utafiti mapendekezo ya kodi inayowasilisha kwa maana kuwa utafiti huu ujitosheleze kwa kuanisha mapato yaliyopatikana au yatakayopatikana kutokana na mabadiliko ya kodi inayokusudiwa kuongezwa ama kupunguzwa na hivyo kupunguza usumbufu kwa wadau.

Mathalani katika Mwaka huu wa fedha 2012/2013 Serikali ilifanya mabadiliko ya kupunguza unafuu wa kodi kwa vifaa vilivyotambuliwa kuwa mtaji *Deemed Capital Goods* kutoka asilimia 100 hadi asilimia 90, hata hivyo takwimu zinaonesha kuwa kwa uamuzi huu, uwekezaji ulishuka kwa asilimia 15. Wakati wawekezaji wanaendelea kujipanga kwa kutumia kiwango hiki kipa cha asilimia 90; Serikali katika bajeti hii ya mwaka 2013/2014, imekuja na mapendekezo ya kubadili kiwango hicho kwa kupunguza unafuu uliokuwepo wa asilimia 90 hadi asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona hali hii inatengeneza mazingira ya kutotabirika kwa sera za uwekezaji hapa nchini, hivyo kufifisha jitihada za kuvutia mitaji ya uwekezaji ya ndani kinyume na baadhi ya malengo ya Bajeti hii ya 2013/2014 inayokusudia kujenga mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji. Kamati inapendekeza kuwa:-

- (i) Kamati inapendekeza kuwa Serikali, iendelee na utaratibu wa mwaka 2012/2013 kwa kutoza 90% wakati ikiendelea na utafiti wa kina ili kuepuka athari zinazotokea pindi utakapofika uamuzi wa kutoza 75%.
- (ii) Serikali izingatie utaratibu wa kufanya mashauriano ya pamoja, ndani ya Serikali na kwa kushirikisha wadau mbalimbali kabla ya kufanya Mabdaliko katika Sheria mbalimbali za Kodi, ili kubaini ni mapendekezo yepi yana tija na mapendekezo yapi yana athari.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya hatua za mapato; kwa mujibu wa Kanuni ya 109 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Mbunge yeyote atakayetoa mapendekezo ya kupunguza kodi katika eneo lolote, ni sharti aeleze ni kwa jinsi gani pengo la kodi litakalotokana na pendekezo hilo litazimbwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, kwa kuwa Kamati ya Bajeti imetoa mapendekezo kadhaa ya kupunguza kodi, imeandaa pia mapendekezo kadhaa ya mapato ambayo yatafidia maeneo ya kodi yaliyopendekezwa kupunguzwa ama kufutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malipo ya tozo mbalimbali zinazolipwa wakati wa uingizaji wa mafuta hapa nchini; wakati wa uingizaji wa mafuta hapa nchini, zipo tozo na ada mbalimbali zinazolipwa na mwingizaji wa mafuta kwa mamlaka au Taasisi mbalimbali kama vile *EWURA, TBS, TIPPER, TPS* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi hutoza kiasi cha fedha kutoka katika kila lita ya mafuta inayoingizwa kama ada ya huduma wanazotoa. Kamati ina maoni kuwa, baadhi ya vyombo hivi hupata fedha nyingi sana na kwamba Serikali inaweza kuchukua

kiasi cha fedha zinazokusanywa katika maeneo hayo kwa ajili ya kuzipeleka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati inapendekeza sehemu ya fedha zinazokusanywa kutoka tozo ya *Wharfage Weights and Measures Fee, TIPPER* na *Regulatory Levy Fee* zipelekwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kamati inakadiria kiasi cha shilingi bilioni 36 zinaweza kupatikana katika eneo hili kama nusu ya tozo hizi zitapelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kodi ya usafirishaji nje (*Export Levy*) ya mashudu na mbegu za alizeti; Kamati yangu ilibaini kuwa kwa sasa Tanzania inapoteza wastani wa dola za Kimarekani Milioni 8.2 kila mwaka kwa kusafirisha mashudu yenye mafuta kiasi cha asilimia nne au zaidi kwa upande wa mashudu na mbegu za alizeti nje ya nchi bila ushuru wowote.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hizi husafirishwa nje ya nchi na hutengenezwa mafuta ambayo huuzwa tena na kurejeshwa hapa nchini. Ikilinganishwa na fedha inayopatikana kwa kuuza nje na kununua tena, ni kwamba Tanzania imekuwa ikipunjika sana kwa kununua bidhaa itokanayo na bidhaa hizo hizo zinaporejeshwa hapa nchini, kwa maana hiyo tumekuwa tunapoteza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, Kamati inapendekeza kuanzishwa kwa kodi ya usafirishaji wa bidhaa hizo nje yaani (*Export Levy*) kwa dola za Marekani 100 kwa kuzibadilisha katika Shilingi za Tanzania kwa kila tani ya mbegu za alizeti (*sunflower seed*) na zipewe utambulisho tofauti kwa maana ya *HS Code 260630* na pia kwa upande wa mashudu yaani (*Oil Cake Mill*), yenye *HS Code 23063010* ambayo yana kiasi cha mafuta cha zaidi ya asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inakadiriwa kuiingizia Serikali kiasi cha shilingi bilioni 16. Aidha, Kamati pia imependekeza kutenganishwa kwa *HS Code* ya mashudu na mbegu ili kurahisisha udhibiti wa bidhaa hizi kwa kuzuia mashudu (*Cake*) kusafirishwa katika *Code ya Meal* yenye mafuta chini ya asilimia nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kamati inaona hili ni eneo ambalo Serikali inaweza kujipatia mapato kirahisi kabisa, bado Serikali imeonekana kuwa na kigugumizi katika kutumia fursa hii.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika bahari kuu; tumelieleza vizuri katika Ripoti ya Mheshimiwa Spika ya vyanzo vipya vya mapato, ambapo Serikali ya Tanzania inapoteza mapato ya takriban Dola za Marekani milioni 220 sawa na Shilingi za Kitanzania shilingi bilioni 352. Kamati inapendekeza Serikali kuweka mrabaha katika eneo hili kutokana na thamani ya samaki wanaovuliwa kwa asilimia tatu. Serikali itapata shilingi bilioni 35.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushuru kwenye malighafi ya sabuni; Serikali ikiweka ushuru wa forodha wa malighafi ya sabuni kutoka kiwango cha asilimia 0.0 kinachotumika sasa na kukipandishwa kuwa asilimia 10. Serikali itapata kiwango cha Shilingi Bilioni 1.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iwapo mapendekezo haya yatatekelezwa kikamilifu, Serikali itakusanya kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 89. Kiasi hiki kinaweza kutumika kujaza mapengo ya sehemu zote zilizopendekezwa kupunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William M. Mgimwa; Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Saada Mkuya na Mheshimiwa Janeth Mbene, kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi hatua hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja hizo kwa muda mrefu na jana wametoka saa 6.00 za usiku. Poleni sana kwa kuweza kufanya maamuzi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na upya wa Kamati hii, majukumu mazito iliyonayo pamoja na changamoto zilizopo, Wajumbe hawa

wamefanya kazi ngumu, kwa utulivu, umakini kwa kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mwenyekiti; Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mjumbe; Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mjumbe; Mheshimiwa Josephat Kandege, Mjumbe; Mheshimiwa Christina Lissu, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mjumbe na Mheshimiwa James F. Mbatia, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mjumbe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mjumbe; Mheshimiwa Joseph Selasini, Mjumbe; Mheshimiwa Saleh Pamba, Mjumbe; Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Mjumbe; Mheshimiwa Ritha Mlaki, Mjumbe; Mheshimiwa John Cheyo, Mjumbe Mshiriki na Mheshimiwa Peter J. Serukamamba, Mjumbe Mshiriki.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillilah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa Mbise na Makatibu wa Kamati Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto, Michael Kadebe na Elihaika Mtui kwa kuihudumia vyema Kamati hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha taarifa hii na natamka naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

SPIKA: Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai na yeye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kwa

mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013), naomba kuwasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2013 (*The Finance Act, 2013*).

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu Kwa kuniwezesha kusimama leo hapa katika Bunge lako Tukufu ili niweze kuisoma hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na kwa niaba ya Msemaji Mkuu katika Wizara ya Fedha Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, naomba kusoma Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka wa 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) Kanuni za Kudumu za Bunge mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeleta Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2013, kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha mabadiliko katika sheria mbalimbali ili kuiwezesha Serikali kutoza kodi mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza Bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge tarehe 24 Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Masoko ya Hisa na Mitaji (*Capital Markets and Securities Act*), Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Wakala za Kiutendaji (*Executive Agencies Act*), Sura ya 245 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (*Excise (Management and Tariff Act)*), Sura ya 147 ya Sheria za Tanzania; na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*Energy and Water Regulatory Authority Act*), Sura ya 413 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine zinazopendekezwa kurekebishwa ni pamoja na Sheria ya Michezo ya Bahati Nasibu (*The Gaming Act*), Sura ya 41 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Kodi ya Mapato (*Income Tax Act*), Sura ya 332 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Hifadhi za Taifa (*National Parks Act*), Sura ya 282 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, mapendekezo ya marekebisho yanailenga Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (*Ngorongoro Conservation Area Act*), Sura ya 284 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya

Bandari (*Ports Act*), Sura ya 166 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Fedha za Umma (*Public Finance Act*), Sura ya 348 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Ubia wa Umma na Binafsi (*Public Private Partnership Act*), Sura ya 103 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna Sheria ya Manunuzi ya Umma (*Public Procurement Act*), Na. 7 ya 2011; Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta (*Road and Fuel Tolls Act*), Sura ya 220 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Mamlaka ya Udhubiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (*Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act*), Sura ya 413 ya Sheria za Tanzania na Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*Tanzania Civil Aviation Authority Act*), Sura ya 80 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Udhubiti wa Mawasiliano Tanzania (*Tanzania Communication Regulatory Authority Act*), Sura ya 172 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Chakula, Madawa na Vipodozi Tanzania (*Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act*), Sura ya 219 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Uwekezaji Tanzania (*Tanzania Investment Act*), Sura ya 38 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Kazi na Mamlaka ya Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar [Powers and Functions] Act*), Sura ya 370 ya Sheria za Tanzania; Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (*Vocational Education and Training Act*), Sura ya 82 ya Sheria za Tanzania, na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*Value Added Tax Act*), Sura ya 148 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizi yana athari kubwa kwa maslahi ya wananchi wetu na kwa uchumi wetu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba Bunge lako Tukufu kuyachunguza kwa undani na kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kwamba maslahi ya kweli ya wananchi wetu na ya uchumi wetu yanalindwa badala ya kunufaisha watu wachache wenye ushawishi wa kisiasa na kiuchumi ndani ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuanza maoni haya kwa uchambuzi wa

mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha, unapendekeza kurekebisha Jedwali la Pili la Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta kwa kuongeza ushuru wa mafuta ya petroli na dizeli kwa sh. 63 kwa lita, kutoka ushuru wa sh. 200 kwa lita uliopo sasa hadi sh. 263 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba Serikali hii ya CCM inapendekeza kuongeza ushuru wa mafuta hayo kwa asilimia 31.5 na endapo pendekezo hili litakubaliwa Bunge lako Tukufu, bei ya mafuta hayo itaongezeka kwa sh. 63 kwa lita kutoka bei za sasa za bidhaa hizo muhimu.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta sio pendekezo pekee litakaloongeza bei za mafuta kwa Watanzania. Hii ni kwa sababu, Serikali hii ya CCM inapendekeza pia marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambayo endapo yatakubaliwa na Bunge lako Tukufu yatasababisha ongezeko kubwa la bei za mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwa mfano, kwa mujibu wa mapendekezo haya, ushuru wa mafuta ya petroli ya kawaida (*regular*) na petroli ya *premium* utapanda kutoka sh. 339 za sasa hadi sh. 400 kwa lita, ongezeko la sh. 61 kwa lita. Aidha, ushuru wa mafuta mepesi (*gas oil*) kwa ajili ya magari na injini ziendazo kasi utapanda kutoka sh. 215 kwa lita uliopo sasa hadi sh. 217 kwa lita, likiwa ni ongezeko la shilingi mbili. Kwa mapendekezo haya ya Serikali hii ya CCM, ushuru wa mafuta ya petroli utaongezeka kwa sh. 124 kwa lita, wakati ushuru wa dizeli utapanda kwa sh. 65 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa mafuta ukiongezeka kama inavyopendekezwa na Muswada huu, bei za mafuta ya petroli na dizeli zitaongezeka pia. Bei za mafuta zikiongezeka halikadhalika nauli za mabasi, daladala, *taxi*, bodaboda na bajaji nazo zitapanda. Aidha, ongezeko la ushuru litasababisha ongezeko la bei za bidhaa nyingine ambazo zinasafirishwa kwa magari yanayotumia mafuta ya petroli na dizeli.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Watanzania wategemee ongezeko kubwa la bei za vyakula mbalimbali kama vile mchele, unga, maharage na kadhalika, kwa sababu ya ongezeko la gharama za usafirishaji zitakazotokana na kukubaliwa kwa mapendekezo haya. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapinga mapendekezo ya marekebisho ya sheria hizi mbili ambayo, kwa malengo au taathira yake, yatawaumiza wananchi wengi wenye vipato vya chini ambao wanategemea mafuta ya dizeli au petroli kwa ajili ya mahitaji yao muhimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha unapendekeza marekebisho mengine katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ambayo yatakuwa na athari mbaya na kubwa kwa maslahi ya wananchi walio wengi na wenye vipato vya chini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mapendekezo haya, huduma za mawasiliano za aina zote ikiwa ni pamoja na kutuma na kupokea simu au ujumbe wa maneno au sauti au picha sasa zitatozwa ushuru wa asilimia 14.5, juu ya gharama za sasa za huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, nyingi ya huduma za mawasiliano zinazopendekezwa kutozwa ushuru huo wa bidhaa, kama vile *call waiting, call forwarding, caller identification, three way calling, call display, call return, call screen, call blocking, automatic call back, call answer, voice mail, voice menus* na *video conferencing*, ni huduma ambazo zimerahisisha mawasiliano kwa wananchi wengi wenye vipato vya chini na hasa kundi kubwa la vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa mapendekezo haya ya Serikali hii ya CCM, huduma hizi ambazo zinapendwa na watumiaji wengi na hasa vijana kwa sababu ya urahisi wa matumizi yake sasa zitatozwa ushuru wa asilimia 14.5.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua ukweli kwamba, kwa sababu ya upungufu wa kisheria yaliyopo sasa, Makampuni ya Simu yamekuwa yanalipia ushuru wa kupiga na kupokea simu tu, wakati makampuni hayo yakipata

mapato makubwa kutokana na huduma za mawasiliano ambazo hazitozwi kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaelewa haja ya huduma za mawasiliano kuchangia ipasavyo katika mapato ya Serikali, kwa kupanua wigo wa huduma za mawasiliano zinazotozwa kodi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haiko tayari kuunga mkono marekebisho ya sheria ambayo pamoja na kuongeza mapato ya Serikali yataongeza mzigo wa kodi kwa wananchi wa kawaida wa Tanzania ambao tayari wanaelemewa na mzigo mkubwa wa hali ngumu za maisha, vipato vya chini na umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali hii ya CCM ihakikishe kwamba, ushuru wa huduma za mawasiliano unaopendekezwa kwenye Muswada huu, hautaongeza gharama za matumizi ya simu ambazo tayari ni kubwa sana. Hilo linawezekana kwa Muswada huu kuwa na kifungu kitakachokataza Makampuni ya Simu kuhamishia gharama za ushuru wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wa huduma hizo na hivyo kuongeza gharama za matumizi ya simu.

Mheshimiwa Spika, Katika hotuba ya Bajeti ya Serikali, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itatoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano ili kutoa unafuu kwa viwanda na wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itatoza ushuru wa asilimia 25 kwenye bidhaa za mchele na sukari wakati bidhaa hizo zinapoingizwa nchini kwa msamaha maalum wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa, aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kutoa msamaha wa ushuru wa forodha ... kwa malighafi ya kutengeneza sabuni inayojulikana kama *LABSA* kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja ili kuimarisha uzalishaji na kukuza viwanda vidogo na vya kati vya sabuni hapa nchini."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, nafuu hizo za kodi zimetokana na mapendekezo ya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha, yaani *EAC Common External Tariff (CET)*.

Mheshimiwa Spika, suala la ushuru wa forodha kwa ngano lina utata mkubwa. Hii ni kwa sababu, kwa sasa ngano inayoingizwa Tanzania kutoka nchi za nje haitozwi ushuru wowote wa forodha; wakati nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatoza ushuru wa asilimia 10 (Kenya) na asilimia 35 (Rwanda). Kama Tanzania, Uganda nayo haitozi ushuru wowote wa forodha kwa ngano inayoingizwa katika nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii, maana halisi ya kauli ya Dkt. Mgimwa, kuhusu ushuru wa forodha kwa ngano ni kwamba Tanzania na Uganda zinatakiwa ziongeze ushuru huo kutoka asilimia sifuri hadi asilimia 10, wakati Rwanda inatakiwa kupunguza ushuru wake wa forodha kwa ngano hadi kufikia asilimia 10 kutoka asilimia 35 za sasa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatambua kwamba kampuni ya *S.S. Bakhresa Group* ndio mwagizaji mkubwa wa ngano Tanzania na kwamba kampuni hiyo inafanya biashara hiyo katika nchi nyingine za Afrika Mashariki na Kati kama vile Uganda, Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya, ni wazi kwamba *S.S. Bakhresa Group* ni kampuni yenye ushawishi mkubwa wa kiuchumi na kisiasa katika nchi yetu na katika eneo hili la Afrika. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge lako Tukufu kama Serikali hii ya CCM haijaweka ushuru wa forodha kwenye ngano ulioahidiwa na Mheshimiwa Waziri kwa sababu ya shinikizo au ushawishi wa kisiasa wa kampuni ya *S.S. Bakhresa Group*.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha hauna mapendekezo yoyote yanayohusu punguzo la ushuru wa forodha kwa ngano inayoingizwa kutoka nchi za nje kama ilivyoielezwa

katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haijaona mapendekezo yoyote ya punguzo la ushuru wa forodha kwa bidhaa za mchele na sukari. Hili ni jambo la kushangaza sana kwa jinsi ambavyo kumekuwepo mvutano mkubwa katika suala hili ndani ya Kamati ya Bunge ya Bajeti juu ya kuwapo kwa marekebisho hayo au la.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba, kumekuwepo mjadala mkali ndani ya Kamati ya Bunge ya Bajeti juu ya haja ya kuendeleza msamaha wa ushuru kwa LABSA au kuanzisha tozo ya asilimia 10 kwa malighafi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako Tukufu kwa nini haijaleta mapendekezo ya marekebisho ya Sheria husika katika Muswada huu licha ya ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwamba bidhaa za ngano, sukari na mchele zingepunguziwa ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya bajeti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisisitiza mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba maji ya kunywa hayatahusika na ongezeko la ushuru wa bidhaa zisizokuwa za mafuta kama vile vinywaji baridi, ambavyo ushuru wake unapendekezwa kuongezwa kutoka sh. 83 kwa lita hadi sh. 91 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kauli hiyo ya Waziri wa Fedha haikuwa ya kweli kwani Muswada huu unajumuisha maji katika vinywaji baridi ambavyo ushuru wake unapendekezwa kuongezwa tena kutoka sh. 83 hadi sh. 91 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mwaka jana Serikali hii ya CCM iliongeza ushuru kwenye maji ya kunywa kutoka sh. 69 hadi sh. 83 kwa lita. Kwa mapendekezo ya Muswada huu wa Sheria ya Fedha, Serikali hii ya CCM itakuwa imeongeza ushuru wa bidhaa katika maji ya kunywa kwa sh. 22 kwa lita katika kipindi cha miaka miwili au ongezeko la takriban asilimia 32 katika kipindi hicho!

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 26 Juni 2013 Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwagawia wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti Jedwali la Marekebisho linalopendekeza marekebisho katika

maeneo kadhaa ya Muswada huu. Kwa mfano, aya B ya Jedwali hilo inapendekeza kuongeza Sehemu mpya ya III katika Muswada huu inayohusu marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu (*The Education Fund Act*), Sura ya 412 ya Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya mapya yanalenga kuanzisha ushuru mpya wa asilimia 2.5 kwa huduma za mawasiliano ya kielektroniki. Hii ina maana kwamba watumiaji wa huduma mbalimbali za mawasiliano ya kielektroniki kama vile simu za mkononi wataongezewa mzigo mwingine wa kodi ya ushuru na kuwa asilimia 14.5 kutoka asilimia 12 zilizokuwa zimepitishwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, aidha, Jedwali la Marekebisho linapendekeza kuongeza ushuru mpya wa asilimia 0.15 ya kiwango kinachozidi shilingi elfu 30 kitakachohamishwa kwa kupitia mabenki, taasisi za fedha na makampuni ya mawasiliano. Hii ina maana kwamba huduma za fedha zinazotolewa na makampuni ya mawasiliano kama vile *M-Pesa, TigoPesa, Airtel Money, EzzyPesa, Western Union* na kadhalika, sasa zitatozwa ushuru wa ziada juu ya ushuru ambao tayari unatozwa kwa watumiaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haikubaliani na mapendekezo haya mapya ya kuongeza mzigo mwingine wa kodi kwa wananchi. Kwanza, mapendekezo haya mapya yanaingiza mambo mapya ambayo hayakuwepo kabisa kwenye Muswada uliochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 14 Juni, 2013. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kinyume na matakwa ya kikanuni yanayolazimu marekebisho ya Muswada yawe yanahusu uboreshaji wa Muswada na sio kuingiza mambo mapya ambayo hayakuwepo katika Muswada uliochapishwa katika Gazeti la Serikali. (*Makofi*)

Pili, mapendekezo haya mapya yamelenga kuwaumiza zaidi wananchi wa kipato cha chini ambao ndio watumiaji wakubwa wa huduma za fedha zinazotolewa na makampuni ya mawasiliano. Hii ni kwa sababu Serikali hii ya CCM inapendekeza kwamba ushuru huu mpya "... hautahusu uhamishaji wa fedha kati ya mabenki na taasisi za fedha, Serikali, Mabalazi na Ofisi za Kibalozi."

Mheshimiwa Spika, upendeleo huu unashangaza sana kwani kama lengo la kutoza ushuru huu mpya ni kuongeza mapato ya Serikali, basi Serikali itapata mapato makubwa zaidi kwa kutoza ushuru huo kwa mabenki na taasisi nyingine za fedha na za Serikali ambazo huhamisha fedha kwa wingi ikilinganishwa na uhamishaji wa fedha unaofanywa kwa kupitia huduma za fedha za makampuni ya simu ambayo watumiaji wake wengi ni wananchi wenye kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(c) kinachofanyia marekebisho kifungu cha (5A) kwa kufuta tarakimu 20 na kuweka tarakimu 25. Marekebisho hayo ya Serikali inasema yanataka kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji yenye umri wa zaidi ya miaka 10. Vile vile kuweka ushuru mpya wa bidhaa wa asilimia tano kwa aina ya magari ya uzalishaji yenye uchakavu wa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, ongezeko hili la ushuru inalipinga kwani haliwatendei haki wananchi hasa wa kipato cha chini kwani kutokana na viwango vya mishahara na hali halisi ya maisha ya Watanzania, uwezo wa kununua magari mapya bado Watanzania wengi hawajakuwa nao. Hivyo magari mengi yenye uchakavu huo huo yanaingizwa na Watanzania wa kada ya chini, tukumbuke kuwa usafiri kwa sasa si jambo la anasa tena bali ni mojawapo ya hitajio muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la asilimia tano kwenye magari ya uzalishaji yenye uchakavu wa zaidi ya miaka kumi, kama tayari magari hayo yamekwishatambulika kuwa ni ya uzalishaji, kwa nini ushuru usiende kwenye bidhaa inayo au itakayozalishwa na magari hayo? Kama kweli tunataka kusonga mbele ni lazima kuwa na mkakati mahususi wa kutumia rasilimali zetu kuongeza mapato ya nchi badala ya kuvizia vipato vidogo vya walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; sehemu ya VII ya Muswada kifungu cha 27 kifungu cha (a) kinachofanyia marekebisho jedwali la kwanza katika aya ya kwanza kwa kufuta jedwali lililopo kwenye aya ndogo ya (i) na kuweka aya mpya.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya ya Muswada yanafanywa ili kupanua wigo wa kodi na kupunguza kodi kwa mapato ya ajira Serikali kwa kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 14 hadi asilimia 13 ili kutoa unafuu wa kodi kwa mfanyakazi, hili ni punguza la asilimia moja tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haikubaliani na pendekezo hili kwani halina nafuu yoyote ya kodi kwa mfanyakazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusisitiza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kwa mfanyakazi (*Pay as you earn*) kishuke kutoka asilimia 14 hadi asilimia tisa ya mshahara wa mfanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yetu ni dhahiri kuwa kiwango cha mshahara kipandishwe na kima cha chini cha uchangiaji wa kodi hiyo kiwe shilingi 250,000, hivyo basi Serikali haitakuwa imepunguza mapato kama inavyoonekana hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220; Kifungu cha 46 cha Muswada kinachorekebisha jedwali la pili la Sheria Mama, Serikali inapendekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa mafuta (*fuel levy*) kutoka sh. 200 kwa lita hadi sh. 263 kwa lita, sawa na ongezeko la sh. 63 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haikubaliani na pendekezo hili kwani lina madhara makubwa kwa maisha ya wananchi kwa kuwa linaongeza gharama za maisha kama vile kupanda kwa nauli, kupanda kwa bei za vyakula na kadhalika. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kufutwa kabisa kwa ushuru wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Sura ya 82). Sehemu ya 21 ya Muswada kifungu cha 61 kinafanyia marekebisho kifungu cha 14(2) cha Sheria Mama kwa kufuta maneno asilimia sita na kuweka maneno asilimia tano. Kambi Rasmi ya Upinzani ilikwishashauri kuwa kiwango hiki kiwe ni asilimia nne na badala ya wigo kuishia kwenye sekta binafsi, bali

wigo upanuliwe hadi Serikali kuu pamoja na taasisi zake zote sambamba na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 62 kinachofuta na kurudisha kifungu cha 19 cha Sheria kinachosema kuwa *the provisions of section 14 shall not apply to any Government department or public Institution which is wholly financed by the Government*. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kusiwepo na *exemption* hiyo kwani wanufaikaji wa kodi hiyo wakati wa kutafuta kazi wanapata ajira katika Serikali na Idara za zake pia. Hivyo, ni dhahiri wanufaikaji wa kodi hiyo sio sekta binafsi pekee.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mapendekezo mengine ya kikodi kama ifuatavyo:-

- (1) Kupunguza misamaha ya kodi hadi asilimia moja ya pato la Taifa.
- (2) Kupanua wigo wa kodi kwa kuanzisha tozo ya maendeleo ya michezo (*Sports Development Levy*) ili kukuza michezo nchini na kugharimia timu zinazowakilisha Taifa katika michezo ya Kimataifa.
- (3) Kuongeza wigo wa kodi kwa kuanzisha tozo ya asilimia moja (1%) kwa bidhaa zote zinanazolingizwa nchini kutoka nje na tozo ya asilimia sifuri nukta tano (0.5%) kwa bidhaa zote zinazouzwa nje ya nchi kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Kwa muda nilionao naweza kupata wachangiaji saba tu, wengine wataendelea jioni. Kwa hiyo, namwita mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Godfrey Zambi kama muda utapatikana. Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya!

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa hii nafasi adimu. Lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na pia mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani, kwa sababu kila mmoja amejitahidi kuzungumza kwa kadri ambavyo inatupa nafasi nzuri zaidi ya kuuangalia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nafarijika kuona kwamba ile ndoto ambayo ulikuwa unatuelekeza kila wakati kuhusiana na mabadiliko haya mapya, sasa yanajidhihirisha umuhimu wake. Kilichonifurahisha zaidi ni ile kuona kwamba tunaposema hiki kisiongezwe, tunaposema kodi hii iondolewe, tunapata taarifa ya namna gani tuweze kushughulikia ili kufidia lile pengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba leo niweze kuwatia moyo wananchi wa Tanzania, tumedhamiria kuona kwamba, uchumi wetu unapata kasi na kuongezeka na katika hilo ni kwamba, tumekusudia na tukaamua kwa hiari yetu kwamba tuangalie angalau sekta kuu tano za kuanza nazo ili tuweze kupata matokeo ya haraka. Lakini pia bila kuacha maeneo mengine na hayo yote yanahitaji lazima tuwe na fedha.

Mheshimiwa Spika, kama tunahitaji kuwa na fedha ili tuweze kufanikisha, ina maana hatuna mjomba, kila wakati tunazungumza kwamba tunaombaomba misaada, tuna mahitaji ya barabara, tuna mahitaji ya maji, tuna mahitaji ya umeme mpaka vijijini. Sasa kwa hali hiyo ni kwamba lazima tufunge mikanda hatuna mjomba na kwa bajeti hii inatusaidia kwamba wote kutekeleza lile tulilolidhamiria.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na tozo ambazo zinakusudiwa kwa mfano, kwa upande wa simu. Kwanza, nafurahi kwamba Watanzania tumeweza kujifunza kwa haraka namna ya kutumia teknolojia katika maendeleo yetu ya kiuchumi. Sasa hivi hata ukienda kijijini mtu anatumia simu, anatumia fedha na anapokea fedha, hatuna tena malalamiko ya kusema kwamba benki zipo mjini tu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mazingira kama hayo bado mpaka sasa Watanzania hatujaweza kuwafikia wananchi wote. Kuna wananchi kwa mfano, wanaokaa katika maeneo kama Ngumbo kule Wilaya ya Nyasa, kuna wananchi wanaokaa kama kule Kapozwa, kuna wananchi wanaokaa kule Wampembe, wanaokaa Kalambo *Falls*, wote hawa wanahitaji kutumia fursa hizi za mawasiliano. Lakini kwa sasa hivi mawasiliano hayapatikani kwa sababu yapo katika baadhi ya maeneo na maeneo mengine hayapo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hawa wananchi wanatembea umbali mrefu kwenda kufuata mawasiliano. Sasa kwa sababu tumeamua kuona kwamba wananchi wote tunapata mawasiliano, ipo kila haja na kila sababu ya kuona kwamba sisi ambao tayari tuna mawasiliano tunachangia ili kuwezesha na wenzetu waweze kufikia huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hasa katika hizi tozo zilizowekwa, sioni kama ni kubwa sana ni kidogo kidogo tunachangia na si vizuri sana kila tunapofikiria kodi kuangalia tu wale wafanyabiashara wakubwa tukajiacha sisi wengine ambao pia tupo katika uchumi. Kwa kutumia simu tunawashirikisha wananchi wengi zaidi katika kuchangia kodi yetu na kubeba mzigo kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata meseji nyingine ambazo tunatumiana kwa kweli pengine siyo za muhimu sana. Kwa mfano, meseji kama ni ya matusi, halafu mtu atume bure ina faida gani? Ni vyema angalau kila mtu kuchangia na ndiko atakapoweza kuona umuhimu wa kutumia simu yake kwa mambo ya muhimu na siyo yasiyo ya muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine hata unapotaka kupokea simu au unapiga hupati *network* kwa sababu mtandao umejaa, lakini ukifuatilia pengine ni taarifa ambazo si za lazima sana kwa wakati huo. Kwa hiyo, angalau kwa kuweka kodi kidogo kutamfanya mwananchi kujua kwamba, nitumie kwa uangalifu kwa kujua kwamba, simu inahitajika na watu wengi na mawasiliano ni kwa faida ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa kodi ya bodaboda au bajaji. Hawa watu ndiyo wanachukua ajira kubwa sasa hivi katika nchi yaani vijana wengi wamejiajiri katika eneo hilo. Kweli tunasema kwamba, yawezekana hizo bodaboda nyingine siyo zao, hilo ni kweli wapo wale ambao bodaboda zile siyo zao. Lakini kuna ajira ipo pale, huyo anayeshinda na hiyo pikipiki kuna kitu anapata. Kwa hiyo, naona vijana wengi walikuwa wanalalamika sasa, kwa kuondoa hii tozo naona kidogo itasaidia kuwafanya watu wengi wapate ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri sana bora kuchukua tozo katika maeneo mengine, lakini hawa bodaboda waangaliwe kwamba ni vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumze suala la umuhimu wa wananchi na viongozi wa Serikali wote kujipanga katika nidhamu ya maamuzi tuliyoyafanya.

Mheshimiwa Spika, China walikuwa kama sisi na Katiba ya China inasema wazi kwamba, tutajenga uchumi wetu kwa kuangalia tabia na misingi ya nchi yetu kwa faida ya uchumi wa Wachina na katika hilo wanasema kwamba suala la nidhamu ni msingi namba moja, uadilifu msingi namba mbili na mambo mengine. Sasa kama tunapanga, basi tutekeleze hivyo. Wananchi hawataona uchungu sana kuchangia, lakini wanapenda kuona mchango wao umekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, na hilo liende sambamba na kuangalia uwezekano wa kuleta mapema Muswada wa Sheria ya Manunuzi ije tuifanyie marekebisho hapa. Kuna maeneo ambayo yanatoa *loopholes* nyingi sana ya matumizi mabaya sana ya fedha za Serikali. Unakuta kwa sababu Sheria inasema kwamba atakayechukuliwa ni *lowest bidder*, lakini anaweza kuwa *lowest bidder* wakati akichokiweka hapo siyo *lowest*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu imesema kwamba, kuna watu watasema kwamba, lazima tuafuate utaratibu wa namna ya manunuzi, unakuta hata kitu kidogo ambacho pengine Kamati ingekaa, ikafanyia kazi kikashughulikiwa kwa wakati suala la muda linakuwa halipo. Matokeo yake fedha inakuwa ipo, inakaa kwenye

mtandao haijafanya kazi yake na wananchi wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba na nashauri sana Sheria ya Manunuzi iletwe na ifanyiwe mabadiliko katika maeneo yale ambayo yana upungufu.

Mheshimiwa Spika, nimempongeza sana leo Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani sababu ninazo. Taarifa yake imekuwa nzuri imeeleza mipango mizuri na kwa kweli tupo wote pamoja kwa sababu kila mtu anachangia kwa lengo la kufanikisha na ndiyo maana naiunga mkono leo hotuba ya Kambi ya Upinzani siyo kwa yale mapendekezo bali kwa namna ilivyowasilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo niliyozungumza, niseme tu kwamba, wote tunajenga nyumba moja ambayo ni Tanzania, tuwe pamoja na tuhakikishe kwamba michango yetu itakayofanikisha kupitisha Muswada huu ni kwa manufaa yetu na Watanzania hatujachelewa, tunachohitaji ni kusonga mbele na kuona kwamba Tanzania inapaa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Wewe humjui Christina ni *very neat* na *polite*. Kwa hiyo, hata mimi nimefurahi. Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa James Mbatia ajiandae. Naombeni kwanza naona kuna taarifa za Kamati ya Bajeti ndiyo naona zinaanza kusambazwa.

Taarifa ya Kambi ya Upinzani nayo imeanza kusambazwa kwa sababu hawa watu wote pamoja na Waziri mwenyewe wa Fedha wamemaliza kazi saa tisa za usiku. Ninazo kopi moja moja, lakini zitazambazwa. Kwa hiyo, naomba mwelewe tatizo lililotokea.

Waheshimiwa Wabunge, mkiniambia mtachangia saa ngapi, mjadala huu tunamaliza leo. Kwa hiyo, mtu atakayehamisha jina lake, atakuwa hayupo kwenye mjadala, maana yake nitaweka wengine.

Kwa hiyo, niliowaita; Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Luhaga Mpina wajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nianze ingawaje muda hautoshi kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya iliyotukuka Mungu akujalie sana kwa kazi hii unayoifanya ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwa Muswada mzuri na kwa kweli maeneo mengi ambayo hata amepata ushauri kwenye Kamati ya Bajeti ameyafanyia kazi. Nina matatizo katika maeneo mawili. Moja, ningetaka Waziri atakapokuwa anajibu na hapa nitaleta *amendments* ni kwenye ushuru kwa ajili ya *leasing* ya ndege pamoja na hizi helikopita.

Mheshimiwa Spika, mtakubaliana nami kwamba sasa hivi usafiri wa ndege sio anasa tena, umetushauri tuseme kwamba, tunaposema hapa tutoe, tunataka kuongeza wapi, kwa hayo, wanayotaka kufanya sasa wanataka kupata shilingi bilioni 4.3. Tulianzisha hapa miaka minane iliyopita kuondoa kodi kwenye maeneo haya hasa *excise duty* pamoja na *Withholding Tax* ili hii *industry* kwe. Lakini leo tukirudisha, tunakorudi ni kule kule tulipotoka.

Mheshimiwa Spika, nitawaambia historia kidogo, kwenye *chartered flights* tulianzisha kodi ya VAT, *excise duty* na *withholding tax*, matokeo yake hiyo *industry* imekufa, wamebakia wanaokodisha ndege tu ni Serikali peke yake, *individuals* hawawezi. Maana yake kama tuliweka hizo kodi ili tuweze kuzikusanya hatutozikusanya. Lakini tukitaka kuweka kwenye *commercial flights* na kadhalika hilo halitowezekana.

Mheshimiwa Spika, Waziri amesema kwamba, kwenye *commercial flights*, hapana, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri najua tumemaliza kazi jana usiku alete *amendments* kwa sababu hii ni sheria ambayo tunatunga. Kwa hiyo, ni vizuri alete *amendments* iwe *clear*, tunataka tupate *clarity* hapa kwamba, ni ndege gani zinahusika na zipi hazihusiki?

Mheshimiwa Spika, *profits margins* za ndege ni ndogo sana. Leo hii *Fast Jet* wamekuja Tanzania bei zimeshuka sana, lakini tunapoweka kodi, watarudi kulekule. Matokeo yake kile tunachokitafuta hatutokipata na wao wala hawapati faida. Ukienda kwenye hesabu zao wanakaribia hata kufunga kwa sababu hawapati faida kwa sababu biashara hii ni *very complicated*.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunaiongezea kodi, nadhani kama Taifa, hii ni sehemu ambayo ni ya muhimu sana na kwa ajili ya nchi yetu na kwa kweli Serikali leo ina-*invest* inajenga viwanja vingi sana. Sasa huku mnajenga viwanja huku mnaleta kodi ambazo mna hakika watu hawataleta ndege, sasa hivi viwanja tunajenga vya nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningepomba sana, hizi ndege zinazokuja Tanzania ziwe ndege mpya, tukiweka kodi nyingi *excise duty* asilimia 20, *withholding tax* asilimia 15, VAT asilimia 18, watakwenda kutafuta ndege zilizokaribia kuchoka, tutaanza kupata ajali ya ndege kama nchi zingine ambacho kinaendelea Tanzania. Hii ni hatari kwa nchi yetu na ni hatari kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri ame-*clarify* hapa, namwomba aje na *amendment* na baadaye nimeleta jedwali la kutaka *amendment* ili tufute kifungu cha 28, hizi shilingi 4.3 zinatoka wapi. Tumesema hata kwenye Kamati ya Bajeti, kwenye *deep sea* kuna ripoti ya *FAO* Tanzania inapoteza shilingi bilioni 350 kila mwaka. Tumesema tusipate zote tuweke *royalty* ya asilimia tatu tu na unaiwekaje, unabadilisha sheria kila anayekuja kuomba leseni unamwekea alipe asilimia tatu, tutapata shilingi bilioni 35.

Mheshimiwa Spika, hizo shilingi bilioni 35 chukua 4.3, nenda weka pale ili tuweze kuendelea na msamaha, zile zinazobaki kuna fedha ya mashudu, tuanze kutoza kodi tutapata shilingi bilioni 10. Hizi shilingi bilioni 10 tutapata karibu bilioni 44 na hizi shilingi bilioni 44 nataka niombe Serikali tunaiweka wapi kwenye mafuta.

Mheshimiwa Spika, Waziri ameleta *measure* hapa kwenye mafuta, fedha anayotarajia kupata ni trilioni 1.285 kwa maana ya kwenye petroli, dizeli na mafuta ya taa. Sina shida, lakini tunasema

kwa ajili ya wananchi wetu, kwa ajili ya kupunguza *inflation*, tunamwomba Mheshimiwa Waziri tumekubaliana naye kwenye mafuta ya taa ambayo itakuwa 475, tumekubaliana naye kwenye dizeli ambayo itakuwa 490, tunasema kwenye petroli iwe 652 ile tofauti tutaipata wapi, tuweke mrabaha kwenye *deep sea*, tutoze kwenye mashudu, tutoze kwenye *LABSA* ambao wao *LABSA* wanataka waondoe iwe *zero*, pale tutapata karibu bilioni 45, tuzi-*replace* hapa, kwa nini nasema hivi?

Mheshimiwa Spika, mafuta ndio kitu pekee ambacho tukipandisha gharama za maisha zitapanda. Naomba tuangalie kwa makini sana, naomba Serikali hapa iangalie kwa makini sana kwa mara ya kwanza tumeingiza kodi ambazo zilikuwa hazipo, leo kila anayetuma *M-PESA* zaidi ya shilingi 30,000 atalipa 0.1 *percent* ya *transaction cost*, 10 *percent* kwa ajili ya yule *vendor* ambaye itabidi hai-*factor in* kwenye gharama zake, lakini *above all* tumeongeza 14.5 *percent* ya *excise duty*, yote yatakwenda kwa huyo mlaji mmoja na *M-PESA* wanatumia maskini.

Mheshimiwa Spika, sasa maskini hawa ambao tunawaongezea gharama kubwa, basi tuwape nafuu kwenye mafuta na tumesema tunawapa nafuu, tumeweka wapi pa kupata hizo fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajua nia ya Serikali ni kupata fedha na sisi tunakubali, lakini tunasema huku tupate fedha, huku watu walipe, lakini huku tuwape unafuu. Kwa sababu hapa tuna-*manage economy at all* tusiangalie upande mmoja wa shilingi.

Mheshimiwa Spika, tumeweka 0.15, *of course* kwenye simu nimesahau. Kwenye simu kila mtu atalipa 12,000 kwa mwaka kwa kuwa na ile laini moja, ambayo ni sh. 1,000 kwa mwezi. Wako watu vijijini mwezi unapita hata sh. 1,000 kwenye simu hajaweka, ameweka sh. 500 tu ili apigiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubali yote haya kwa sababu nia yetu tunataka tuendeleo, tufanye maendeleo makubwa, sasa yote haya tumeyafanya, basi wananchi hawa tuwape nafuu kwenye mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaombeni sana Serikali, waende wakakae walitafakari hili jambo, hatujapoteza tutabakia *within the framework* ya 18.2 *trillion* sababu nia yetu na sisi tungependa. Naipongeza Serikali, jambo lingine tumefanya kubwa sana, tumeambiwa tutapata bilioni 160, lakini zitakuwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, leo hii kila atakayefanya *transaction* benki, analipa 0.15 maana yake nini? Zamani ulikuwa ukituma shilingi milioni 100 benki, unalipa shilingi 10,000 *transaction cost*, sasa utakuwa unalipa shilingi 150,000. Ni fedha nyingi sana na *transaction* nyingi sana na hizo zitawahusu wananchi wetu wale wale.

Mheshimiwa Spika, huku ukienda kwenye *Pay As You Earn* wanaendelea kulipa kwa kiasi kikubwa, huku nyumba za kupanga ziko bei juu, mabasi yako bei juu, nawaombeni viongozi tufanye maamuzi, tutafute sehemu za kuwapa ahueni wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimependekeza kwanza hapa kwenye *aircraft*, naomba tufute naleta *amendments*, lakini kwenye mafuta naomba tuchukue jedwali la pili la Kamati ya Bajeti, tumefanya hesabu, tofauti ni shilingi bilioni 44 na tumesema zitatoka wapi, zile shilingi bilioni 44 zitakuwa zinawasaidia Watanzania wetu na bei zitaendelea kushuka. Wale watu wa *deep sea* wafanyabiashara wakubwa kwa nini tusiwatoze.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, namshukuru Waziri wa Fedha, kwa kuwa amekuwa msikivu sana. Kwa kazi hiyo aliyoifanya Waziri wa Fedha ya kutusikiliza yeye na watu wake, nawaomba na haya watusikilize ili twende vizuri na tuweze kuwasaidia Watanzania wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii na nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa James Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwanadamu akiweza kutawala muda basi itakuwa naye binafsi anaweza akajitawala na kujipatia maendeleo endelevu. Nimeanza na hili kwa sababu tukiangalia mihimili hii mikuu mitatu ya dola, Bunge, Serikali na Mahakama, kusema kweli mhimili unaouongoza wewe, Bunge ndilo linaloongoza kwa nidhamu ya kutunza muda, hongera sana, mihimili mingine bado iko hoi kidogo, Mahakama ilikuwa inajitahidi, lakini nayo sasa hivi nidhamu imeshuka kidogo.

Mheshimiwa Spika, nidhamu ya ufanisi katika Muswada tulionao hapa mbele yetu ni muhimu sana tukaangalia suala la muda, gharama na ubora. Tukiangalia ufanisi katika kufanya kazi katika Taifa letu, wafanyakazi wetu wamechukua au tumewatengea zaidi ya shilingi trilioni 4.7 ya bajeti yote ambayo ni asilimia 25.8 ya bajeti yote. Tukisoma Katiba yetu, kazi ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa ibara ya 63(2).

Mheshimiwa Spika, nimeanza na kuisimamia na kuishauri Serikali. Nimeanza na hilo kwa sababu niombe Serikali, Kamati ya Bajeti imekaa kwa niaba ya Bunge hili, ikaleta mapendekezo na iko kwenye jedwali la pili la namna bora ya kuondoa unafuu wa maisha kwa Watanzania na hasa mafuta ikiwepo dizeli, petroli na mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili linamgusa kila Mtanzania na kwa kuwa Bunge linaisimamia Serikali na kwa kuwa litapunguza zaidi ya bilioni 44 kuna vyanzo vingine mbadala tulivyovionesha Serikali vya kupata mapato. Vyanzo hivi mbadala sio kwamba Serikali imeambiwa jana usiku la hasha, imeambiwa tangu mwaka jana na mkasema mnasikia. Sasa tunaiomba Serikali hii inayosema ni sikivu isikie vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tozo hizi kwenye mafuta kuna *TIPPER, EWURA, Weight and Measures*, hapa kuna tozo nyingi nyingi, tunamwomba Waziri alete *amendments*, ziko fedha hapa, Kamati ya Bajeti tumependekeza zaidi ya shilingi bilioni 36 ambazo zitafidia kwenye zile shilingi bilioni 44. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, itakuwa bado, kati ya shilingi bilioni 44, ukiondoa shilingi 36 bado shilingi bilioni nane. Kwenye *deep sea*

Mheshimiwa Waziri asiseme wanafanya utafiti, Kamati ya Mheshimiwa Spika iliyoongozwa na Mtemi Andrew Chenge ilishafanya utafiti na tukawapa takwimu tangu mwaka jana. Kwamba kwenye *deep sea*, fedha zipo, tumekwenda kwenye Ofisi ya Mamlaka inayohusika, tumeona kwa mwaka tunazo zaidi ya shilingi bilioni 352, chukua hapo asilimia 10 tu *compliance*, tutapata zaidi ya shilingi bilioni 35.2.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mnasema wapi tunapata, tunaonesha vyanzo vya mapato. Tulikuwa tunaongea Bunge hili matumizi, matumizi, leo tunakuja na mawazo mapana ya kuonesha mapato yatapatikana wapi ili kuweka unafuu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye masuala ya mashudu, mafuta ya alizeti, *semi processed*, nenda kwenye keki ile ambayo inaitwa mashudu, yenyewe ambayo tuna-*export*, tozo ya kuuza tutapata zaidi ya shilingi bilioni 16. Serikali hii sikivu tunawapeni mapato, ushauri wa mapato mbona mnakataa hata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ngozi ghafi, huu ni mwaka wa tatu, Serikali imeshauriwa kwamba, *tusi-export* ngozi ghafi, lakini hatujaona kwenye bajeti hii ngozi ikizungumziwa chochote kwamba namna gani itasaidia uchumi wa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiwekeza vizuri na hapa niingie kwenye sekta ya anga, sekta hii ya *Air Aviation*, angalia wenzetu wanaotuzunguka katika Afrika Mashariki, angalia wenzetu wa Kenya, angalia *Air Rwanda*, angalia Uganda, sisi Watanzania tuna nini. Mashirika tuliyonayo leo hii *Precision* nayo iko katika mgogoro mkubwa, iko hoi. Tukienda kwenye *Fast Jet* iko katika hali ambayo haiaminiki sana.

Mheshimiwa Spika, sasa sekta hii ya anga inasaidiana na sekta ya utalii na Kamati ya Bajeti iliweza ikapambana na Wizara kwenye sekta ya utalii mlikuwa mnataka tozo ya zaidi ya shilingi bilioni 51, tunashukuru mmetusikia na mmeondoa ile shilingi bilioni 51 kwenye sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watalii leo hii wanakuja Tanzania zaidi ya milioni moja na sabini na saba tukiondoa hizi tozo kwenye hizi ndege tukalea vizuri sekta ya anga, watalii watasafirishwa moja kwa moja kutoka Marekani kuja Tanzania kutoka *Spain* kuja Tanzania, mwaka ujao tutapata watalii zaidi ya milioni mbili.

Mheshimiwa Spika, hii *withholding tax* wataanza kuweka spea za ajabu ajabu tutakuwa na ndege kama za *West Africa* huko, ndege wanazotengeneza wanapiga ribiti kwa kupiga shoka na nyundo wenyewe kwa mikono tunakwenda wapi? Wakati Tanzania maisha ya mwanadamu huwezi ukayaweka kwenye gharama ya kitu chochote kile bora, tulete ndege za ajabu ajabu tuanze kuua Watanzania hawa, bajaji zinatimaliza, pikipiki zinatimaliza, magari mabovu yanatumaliza na ndege tena zianze kuua Tanzania, tunasema hapana *with due respect*.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali ikubali kuondoa na kwenye hii sekta ya anga ni shilingi bilioni 4.3 tu. Nimeshakupa vyanzo vya bahari kuu zaidi ya shilingi bilioni 35, tumekupa kwenye haya matozo mbalimbali hapa ambayo kwa mfano, *TIPPER*, haifanyi kazi yoyote, lakini mmeipa mabilioni ya fedha inachukua hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuchukue hizi fedha ili hii sekta tuilee, hatukatai watu walipe, sawa, lakini tuilee ili ikishakua, tuone ndege kwenye viwanja vyetu, kuna Songwe Mbeya, Njombe kuna *Airstrip*, kule Zanzibar kuna uwanja ule, ndege ziko wapi? Sekta hii mbona tunai-*frustrate* jamani na hii sekta inaunganisha na utalii katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Rais anafanya kazi kubwa sana kwenye masuala ya utalii, sekta ya utalii imeanza kukua tunashindana na wenzetu, halafu tena tunataka kuiangamiza sekta hii, hapana sikubali kwa gharama yoyote. Kwa kuwa Kikatiba Bunge linaisimamia Serikali, naomba Waheshimiwa Wabunge chondechonde tusiikubalie Serikali kwenye hili la shilingi bilioni 4.3 ambayo inataka kuiangamiza sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka minane iliyopita tumekubaliana kwamba tuanze kui-*raise* sekta hii, sekta ya anga iweze ikanawiri,

sekta ya anga iwe vizuri, kwa nini tusiangalie Bandari ya Dar es Salaam. Mwaka jana bandari ya Dar es Salaam ilikuwa inapata mapato yake ya shilingi bilioni 24. Lakini tukatoa mawazo tukashirikiana na Serikali, Mheshimiwa Mwakyembe akasimamia vizuri, leo hii kwa mwezi ni shilingi bilioni zaidi ya 40, ongezeko la asilimia 66 na ikilelewa vizuri sekta hii bandari ya Dar es Salaam peke yake miezi mingine ijayo zaidi ya asilimia 66 tutaongeza zaidi ya shilingi bilioni nyingine 16, tutapata mapato, yako waziwazi kwenye sekta kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tusijiingize tu kwenye kuminya hapo hapo, unamlea mtoto huyu unaanza kuona kitu kidogo kimepatikana pale na matatizo makubwa ni kutokufanya maamuzi wakati wa Serikali kwa wakati unaotakiwa. Serikali inakuwa na kigugumizi tunafanya utafiti, tunafanya utafiti, watendaji, watendaji, watendaji wa *Big Result Now*, sawa walifanya kazi nzuri, lakini Wabunge ambao hatukuwa kwenye *Big Result Now*, tumefanya kazi hiyo kubwa na tumeishauri Serikali vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *with due respect*, nahitimisha kwa kukushukuru, kazi iliyofanyika katika mzunguko huu wa bajeti ni kubwa sana na tukijilinda vizuri, tutapiga hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa muda huu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwita Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ingawaje kama tatizo ulilolizungumza wewe mwenyewe kwamba *document* hizi zilizowasilishwa, nyingine zote hatunazo hata ile ya Waziri nayo imekuja kwa kuchelewa. Kwa hiyo, ilikuwa ngumu kidogo kufuatilia jinsi wawasilishaji walivyowasilisha, lakini hata hivyo nitawasilisha kwa kadri ambavyo nimeweza kuchukua.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiomba kwamba, tunapofikia kwenye hatua kama hii na wewe mwenyewe mwaka jana ambavyo uliamua kwa dhati kuunda Kamati ya Kuishauri Serikali

kuhusu Mapato binafsi nilikuwa Mjumbe na nakushukuru kwa kunitiua kuniweka kwenye Kamati ile, lakini nikasema kwamba, Wabunge hawa wote wengine walikuwa na haki ya kusoma kile kitabu na kuelewa tumeishauri nini Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitegemea kabisa kwamba, aidha hii ripoti ingeweza kuwasilishwa hapa Bunge kabla hatujaanza kujadili mapato ya Serikali ili Waheshimiwa Wabunge wakasoma na kujua kwa kina nini tumependekeza mle ndani na wao wakaongezea mawazo pale, maana yake Serikali ingepata ushauri uliokamilika wa kuhusu ni jinsi gani iboreshe mapato yake.

Mheshimiwa Spika, najua hatujachelewa kwa sababu mapambano bado yanaendelea ya kuhakikisha Taifa hili linapata mapato ya kutosha. Hii ripoti kama haiwezi kuwasilishwa ichapwe Wabunge wote wagawiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wawasilishaji wengine wote waliokuwa wanazungumzia juu ya ushuru wa *LABSA* kwamba huu ushuru uwekwe sasa. Mwaka jana tulisamehe, mwaka huu hiyo asilimia 10 ya *LABSA* kwa ajili ya kutoza huu ushuru wa bidhaa wa *LABSA* iwekwe ili kuongezea Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaweka ushuru huu kwa kujua kabisa kwamba tayari tuna viwanda hata kama bado ni vichache, lakini tutaviwezesha kukua, vitaweza kuvutia wengine na mwisho wa siku tutaweza kutengeneza *LABSA* wenyewe hapa nchini na kujitosheleza.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kusema kwamba viwanda hivi havijakuwa, wakati tunavipatia ushindani mkubwa kwa kuingiza *LABSA* iliyosamehewa kodi, maana yake tusitarajie viwanda tunavyotaka kuvikuza hapa nchini vitakuwa na baadaye vitaweza kuwa na uwezo wa kutoa *LABSA* nchini.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha kwa sababu muda wote amesitiza kupata mapato, sioni sababu ya kuyaacha haya mapato ambayo hayana sababu yoyote. Hii kodi iwekwe kama ambavyo Kamati imependekeza na ya Bajeti na kama ilivyo kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hili suala la misamaha ya kodi. Ukisoma kitabu chetu hiki cha taarifa ya Kamati yako uliyoiunda ambayo ina kurasa zaidi ya 150, ukikisoma kitabu hiki na ukaenda kwenye misamaha ya kodi, tumeishauri Serikali kwa dhati kabisa kuhusu kupunguza misamaha yake ya kodi.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri zipo hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuanza kutekeleza hilo ambalo tuliliagiza sisi wenyewe. Ukisoma ukurasa wa 99 mpaka ukurasa wa 107, utaona mapendekezo tuliyoyatoa sisi wenyewe kuhusu Serikali kupunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, ninachoanza kuogopa ni kwamba yale tuliyoyazungumza humu kuhusu Serikali kupunguza misamaha ya kodi, *already* tena sisi wenyewe tumeanza kulalamika Serikali inapoanza kupunguza misamaha hiyo kwamba, inapopunguzwa tunalalamika sisi wenyewe. Kwa hiyo, tunaweza kuleta *contradiction* kubwa sana kwa Serikali kwa sababu wakati huo huo tuliwaambia wapunguze misamaha ya kodi na wakati huo huo tena tukitetea waendeleo kuongeza hiyo misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nam-*support* kabisa kwa asilimia mia moja Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuamua kupunguza misamaha ya kodi kuanzia ile misamaha inayotolewa na kituo chetu cha uwekezaji kutoka asilimia 90 mpaka asilimia 75 ndiyo sisi Wabunge tumetaka hivyo.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi ya nchi hii sasa hivi inatisha. Wenzetu wa Uganda wana misamaha ya kodi ya asilimia 0.4, Kenya wana asilimia moja, sisi tuna asilimia 4.3 na taarifa ya sasa hivi itakapowasilishwa ya *CAG* ya mwaka 2012/2013, misamaha ya kodi itakuwa imefikia zaidi trilioni mbili. Sasa tutaendelea kuendeleza misamaha ya kodi hii mpaka lini wakati Taifa linaangamia kwa kukosa vyanzo vya uhakika vya mapato?

Mheshimiwa Spika, tukasema kwamba ifike mahali hata hii misamaha ambayo Waziri anaibuka *from nowhere* anasema kwamba, nimesamehe kodi katika maeneo fulani. Tumesema

kwenye ripoti yetu kwamba hiyo misamaha sasa iondolewe ibaki tu misamaha iliyoko kwenye Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tena na nisisitize kwamba, Serikali kuchukua hatua ya kufuta baadhi ya misamaha ya kodi hiyo ikiwemo hiyo niliyoitaja pamoja na wenzangu na wengine ambao wamekuwa wakitetea katika maeneo mbalimbali, mimi kama Mpina ni mnufaika wa misamaha hii ya kodi. Ninayo *certificate* ya kusamehewa kodi katika makampuni yangu ambayo nayaongoza, lakini kwa faida ya Taifa, nasema misamaha ya kodi hii ipunguzwe kwa kadri inavyowezekana ili kuliwezesha Taifa kupata mapato ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri tuliutoa kwenye Kamati yako ya Mapato uliyoiunda, lakini bado kuna changamoto kubwa sana na kama ilivyozungumzwa na wenzangu changamoto zipo kubwa sana katika upatikanaji wa mapato ya uhakika wa nchi yetu. Utaona Waziri wa Fedha leo, tunaendelea kuwa na vyanzo vya mapato ambavyo ni vile vile vya siku zote.

Mheshimiwa Spika, wazo langu na nim-*support* Waziri wa Fedha kwa jinsi alivyokuja na hilo ongezeko, kwa mfano, kwenye sigara, vinywaji baridi, vinywaji vikali na mvinyo vimekuwa vikipanda kila mwaka, kwa mwaka jana iliongezeka kutoka asilimia 20 mpaka 25. Mwaka huu imeongezeka tena asilimia 10 katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba kwa mwaka huu tumeongeza hiyo asilimia 10, basi imetosha. Mwaka unaofuata tutafute vyanzo vingine vya uhakika ambavyo vipo kama Kamati ya Bajeti ilivyozungumza. Ukisoma humu utaona.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambieni, leo Bajeti yetu mapato ya ndani tumeongeza trilioni 2.5. Katika ongezeko hilo la trilioni 2.5 kwa mujibu wa Benki Kuu ongezeko lolote la mapato asilimia 56 linatokana na ukuaji wa uchumi. Sasa ukichukua asilimia 56 la ongezeko la trilioni 2.5 ni trilioni 1.4.

Mheshimiwa Spika, maana yake ongezeko lingine linalobaki la trilioni 1.1 litasababishwa na vitu vingine ambavyo; moja, kuanzisha kodi mpya. Pili, kuboresha mfumo wako wa ukusanyaji wa kodi

pamoja na mambo mengine kama kufuta misamaha ya kodi na nini, ndiyo utazipata zile trilion 1.1. Ukiingia kwenye ripoti yetu kwenye kuboresha tu mapato, ukaboresha madini, ukaboresha simu kwa maana sasa hivi jitihada za Serikali ya kuwa na hii *traffic telecommunication monitoring system* utaweza ku-attract mapato mapya zaidi ya bilioni 600, Kamati ilibaini.

Mheshimiwa Spika, kwenye madini ukizingatia ile taarifa ile ya TMAA unaweza kupata mapato ya zaidi ya bilioni 500, tayari zile trilion 1.1 zimepatikana pale. Kabla hujakwenda kuongeza tozo wala kuongeza ushuru wala kuongeza kiwango chochote cha kodi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana muda wote nimekuwa nikisema na huu ni ushahidi tosha kwamba malengo yanayowekwa na TRA siyo sahihi, ingawaje Waziri wa Fedha ameendelea kutetea kwamba, si wao wanaopanga. Sasa mimi nasema wote wanaopanga malengo ya Serikali hayako sahihi.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaona tu, uki-track pale unaweza ukaona. Kwa sababu karibu ile shilingi trilion 1.1 ya ongezeko jipya linatokana na ongezeko la ushuru, tozo na kodi, lakini mfumo wenyewe wa kuboresha makusanyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Bahati mbaya kengele ya pili imeshagonga. Waheshimiwa Wabunge hii ripoti anayosema tutajitahidi sana kuweka nakala za kutosha kule *library*. Kwa sababu tukisema tuchapiche, ni kama alivyoonyesha ile *Bulk report*. Kazi kubwa ilifanyika katika ile taarifa.

Kwa hiyo, tutaweka nakala za kutosha kule *library* na mtu anayetaka kusoma akaazime kule, akasome, lakini tukisema tuchapishe hivi, kwa kweli na sisi tutakuwa na matumizi mabaya kwa sababu kama sasa hivi nawaombeni mkachukue makablasha yenu kwenye *pigeon hall*, yamejaa watu hawachukui.

Sasa tutaweka nakala za kutosha kule na hii haizuii kwa sababu ripoti yao ilikuwa inaonesha mapato ya mara moja ambayo

yangeingia kwenye bajeti hii; kuna mapato ya bajeti ya mwaka kesho na kuna mapato ya bajeti ya mwaka kesho kutwa.

Kwa hiyo, kwa Mbunge mzuri, haya yote ni maandalizi ya kujiweka sawa wakati ukifika anaweza kupata *source* zingine za *revenue*. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwenye jambo hili la mapato na dhamira ya pamoja ya kupanua mapato ya Serikali. Dhamira ya kupanua mapato ya Serikali haitaweza kutekelezwa kwa ufanisi na kwa haraka kama usimamizi wa Kibunge wa kazi mbalimbali za upanuzi wa mapato ya Serikali hautaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63 ndiyo lenye mamlaka ya kuisimamia Serikali. Sasa ni bahati mbaya kwamba, kazi zote nzuri zinazotajwa hapa hazijaletwa Bungeni. Naelewa kwamba uliunda Kamati yako na nashukuru Kamati imefanya kazi yake na natambua maelezo ambayo yameelezwa hapa kwamba, ripoti ya Kamati ile inaweza kupatikana kwenye Maktaba ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, lakini ni ukweli kwamba kuna utofauti kati ya ripoti ambazo ziko pembezoni, iwe ni kwenye maktaba au mahali pengine popote na ripoti ambazo zinawasilishwa na kusomwa na kujadiliwa Bungeni katika usimamizi wa utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningepomba niishauri Serikali na Ofisi ya Bunge, kwa upande wa Serikali tumetumia pesa za wahisani na sehemu kubwa ye pesa zikiwa msaada kutoka Uingereza kwenye mfumo wa matokeo ya haraka kwenye *LABSA* au maabara. Mojawapo ikiwa ni maabara ya mapato ambayo ilichambua vyanzo mbalimbali vya mapato na kupanua wigo wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini ile ripoti imefanywa kuwa ni ripoti ya Serikali peke yake, sio ripoti ya Bunge kwa maana ya kuletwa hapa Bungeni na kupitiwa ili Bunge liisimamie Serikali kuhakikisha kwamba, mapendekezo yaliyoko Ofisi ya Rais yanatekelezwa kwa wakati.

Sasa mwaka huu tumetenga fedha za ndani bilioni 29, kwenye Ofisi ya Rais kwa ajili ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, sasa ili hizi bilioni 29 za ndani zisitumike hivyo hivyo kama ilivyotumika mwaka jana kwa fedha za wahisani. Hii ripoti ya *Lab* isiishie kwenye semina tu, iletwe hapa Bungeni ili Wabunge tuisimamie Serikali kuhakikisha utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ripoti ya Kamati yako uliyoiunda, naelewa kwamba nyaraka inaonekana kubwa sana, lakini tuna makabrasha mengine ya matumizi makubwa sana tunaletewa Bungeni hapa. Sasa kama tunaweza kuletewa makabrasha makubwa ya matumizi, ni kwa nini tunahofia makabrasha makubwa ya mapato ambayo ndiyo muhimu zaidi kwenye kuhakikisha matumizi yanazingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunaona kuleta kama karatasi ni nyingi basi ripoti hii ili hata umma wa Watanzania ili ujue *value for money* kwenye kazi hii iwekwe wazi kwenye tovuti ya Bunge, ripoti hizi ziletwe Bungeni tuweze kuisimamia Serikali ili kuhakikisha utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mchango wangu sitatumia muda mrefu sana kwenye takwimu za mapato kwa sababu toka tumeingia na kuanza Bunge hili ambalo umeanza kuliongoza, tumekwishajadili sana kuhusu mapato.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwenye kila Hotuba ya Bajeti Mbadala iwe ni 2011, 2012 tumekuwa tukianisha vyanzo mbadala ambavyo vingempunguzia ugumu wa maisha mwananchi wa kawaida na wakati huo huo tungeongeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sitatumia muda mrefu sana kwenye kuchambua takwimu za mapato kwa sababu tuna kazi mbele kubwa sana ya kuchambua marekebisho ya Sheria 22 kwa dakika chache tulizonazo. Niseme tu kwamba katika haya marekebisho ya Sheria 22 zilizoko kwenye orodha na maamuzi mengine ya Muswada huu ambayo yatatekelezwa na Mawaziri wa

Kisekta, nitaleta jedwali la marekebisho kwenye vifungu kumi kati ya maeneo haya 22.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa nitazungumza kwa muhtasari tu yale maeneo ambayo naamini kwamba, Serikali inapaswa kuyasikia sio tu kwa maandishi, sio tu kupitia majedwali ya marekebisho, ila itambue moja kwa moja athari zake kwenye maisha ya wananchi na ni mapendekezo ambayo kimsingi hayapaswi kuungwa mkono na kupitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nisikitike kwamba, nitaelekea kwenye vifungu hivi, lakini nikianza na hotuba ya Waziri na nitaanzia mwishoni mwa hotuba. Mheshimiwa Waziri anahitimisha kwa kusema kwamba: "Kama nilivyoeleza hapo awali mengi ya marekebisho yanayopendekezwa ni utekelezaji tu wa kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ambayo yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha hotuba ya Bajeti ya Serikali na Waheshimiwa Wabunge mliipitisha hapa Bungeni tarehe 24 Juni, 2013."

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri wa maneno ya hitimisho ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba, kazi tunayoifanya sasa ni kazi ambayo kimsingi Bunge lilishapitisha. Kwa hiyo, tunaweka tu sura ya utekelezaji wa kisheria, lakini maamuzi yalishafanyika tayari. Maamuzi yalishafanyika tarehe 24 Juni, wakati Wabunge walipoitwa kwa jina mmoja, baada ya mwingine kwa kupiga kura ya ndiyo na hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninachokisema tu ni kwamba, ni jambo la kushangaza kidogo kwa Wabunge walipiga kura ya ndiyo na niseme hivi, Wabunge walipiga kura ya ndiyo kwa sababu waliopiga kura ya hapana na ambao waliamua kususia kwa idadi yao ingetosha idadi ya kikatiba ya kuikataa bajeti ya Serikali, mapendekezo haya yasingepita.

Mheshimiwa Spika, sasa kitendo cha mapendekezo haya kupitia kwa sababu ya uchache ya waliopiga kura ya hapana na uchache ya waliosusua, ni wazi kwamba tunachokifanya sasa hakitakuwa na mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa...

SPIKA: Naomba ukae kidogo na nitoe ufafanuzi maana usi-*mislead* watu.

Anachokisema Waziri ndicho kiko kwenye Kanuni ya 109, kwamba the *bulk figure* tuliyopitisha hapa ile haibadiliki. Lakini kwa Muswada wa Fedha huu ambao mnapitisha na marekebisho ambayo mnayo, kama yatapita kwa maana ya kwamba badala ya kuwa unatoza mafuta, utatoza kitu kingine, lakini idadi yake itabakia ile ile. Naomba hili tusichanganye watu. (*Makofi*)

Mnaweza kuja hata na tozo lingine kwa mujibu wa hii Kanuni ya 109 (2), mnaweza kuleta hata aina nyingine ya kodi hapa ikaingia kwenye Muswada huu. Ndiyo maana unakuwa na *amendments* zako na wengine wanasema wanazo.

Kwa hiyo nakusudia tumalize michango hii ili kesho tuingie kwenye hizo *amendments*. Lakini sio kuchanganya Bajeti tuliyopitisha hapa, ile ni *conclusive* ya ile *figure* ile haibadiliki pamoja na *Appropriation Bill* mliyopitisha jana haibadiliki. Ila hayo maneno mengine ya kubadilisha shilingi ngapi huko mnaweza kubadilisha. Kwa hiyo, naomba msije kuwachanganya wananchi, sio kweli hiyo. (*Makofi*)

Tunaendelea Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naamini umeulinda muda wangu.

SPIKA: Utalindwa tu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nisisitize kunukuu yale ambayo Mheshimiwa Waziri mwenyewe katika hotuba yake ukurasa wa 21 ameyaandika. Ninachoweza kusema kwamba huu ni Muswada wa Sheria ya Fedha, lakini ni Muswada wa Sheria ya Fedha wa majanga na ni majanga ya kuwaongezea ugumu wa maisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize vizuri sana ili kwenye hitimisho la mjadala huu, kabla hata

hatujaenda kwenye kifungu kwa kifungu kwenye marekebisho ambayo tutayaleta, baadhi ya mambo ayarekebishe mapema sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii iliahidi maisha bora kwa kila Mtanzania na iliahidi kuanzia mwaka 2005, lakini toka wakati huo maisha yamekuwa magumu na gharama za maisha zikipanda kwa ari, kasi na nguvu zaidi. Sasa nilitarajia kwamba lengo mojawapo katika Muswada huu kipengele cha madhumuni na sababu, lengo mojawapo kuu lingekuwa ni kupunguza gharama za maisha kwa wananchi. Yaani lingekuwa ni lengo kabisa, kwamba, tunafanya marekebisho ya kikodi kwa lengo la kupunguza gharama za maisha kwa wananchi. Lakini kinyume chake na tutaleta marekebisho ya kukataa mambo haya.

Mheshimiwa Spika, gharama zilizoongezwa kwenye simu kwa sababu ya muda sitarudia kwa sababu zinafahamika. Gharama zilizoongezwa kwenye mafuta, ni gharama ambazo kwa lugha yoyote ile, haziambatani na lengo la Serikali la kupunguza gharama ya maisha kwa wananchi. Hii si sauti ya sisi Wabunge tunaozungumza Bungeni, hii ni sauti ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zinaonesha Watanzania kwa sasa, ukiwaambia tutajie matatizo mawili yanayokukabili, tatizo mojawapo atakalokutajia ni ongezeko la gharama za maisha. Kupungua kwa mfumko wa bei mpaka tarakimu moja, hakujaambatana na kupungua kwa bei, yaani kasi ya mfumuko inashuka, lakini viwango vya bei bado viko juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maamuzi yangefanyika ya kuangalia maeneo ambayo yanakwenda kumpunguzia gharama za maisha mwananchi, huko ndiko ambako tungeepuka kabisa kuongeza kodi kama ambavyo orodha ndefu ilivyo hivi sasa ya kuongeza kodi kwenye maeneo mbalimbali kwenye mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu rahisi sana inayoweza kutolewa na Serikali ni kwamba, ni lazima tujikamue ili tupate maendeleo, inaweza ikatolewa sababu ya namna hiyo, lakini sisi tumeeleza maeneo mengine mbadala ambayo tungeweza kukamua mapato

bila kuongeza mzigo wa gharama za maisha kwa Mtanzania maskini, Serikali hii iliahidi kuwajali wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, mengine tutaonana kwenye vifungu mbalimbali. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Halima Mdee, kwa sababu muda upo, naweza kumpata mchangiaji mwingine. Mheshimiwa Halima Mdee endelea!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza tokea mlipuko wa mabomu Arusha, nachukua nafasi hii kuwapa pole sana Wanaarusha, lakini vilevile nichukue nafasi hii kulaani vikali kauli zenye utata na zenye upotofu mkubwa zilizotolewa na Serikali hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inajua ni nini kilichotokea Arusha, ilitumia kutokuwepo kwetu kupotosha, lakini tunashukuru kwamba, ukweli utadhihiri. Tutakuwa ni wendawazimu kama Chama tukijilipua mabomu wenyewe ili tupate umaarufu wakati hiki Chama mnajua kasi yake na mnajua muziki wake 2015 utakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kwa masikitiko makubwa kwa vyanzo vya mapato vya Serikali, kila mwaka tumekuwa tukitegemea juisi, sigara, pombe kali. Mwaka jana Mheshimiwa Kafulila aliongea, akasema hivi Taifa la Tanzania likiamua kuokoka kumrudia Yesu au kumrudia Mtume na kuacha kunywa pombe nchi itakwenda? Sasa hii inaonesha na inawezekana kabisa Serikali ya CCM iliyotawala nchi hii miaka hamsini uwezo wake wa kufikiri, umefika mwisho na kibaya zaidi mmekuja na tozo zingine zinazomwathiri Mtanzania maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tozo tatu za simu Mheshimiwa Serukamba amezungumza; tozo tatu za simu, kodi ya zuiro 10%, ushuru wa bidhaa 14.5% na ushuru wa bidhaa ya kadi ya simu sh. 1,450/=, zote zinakwenda kwa mlaji Mtanzania maskini. Sasa sidhani kama watu wenye busara ambapo kuna nayaraka hapa za Serikali, tena uzuri nyaraka hii utangulizi wake umeandikwa na Katibu Mkuu wa Wizara

ya Fedha, kitabu chenyewe kinaitwa *transforming the informal sector*.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa pili wa kitabu hiki unasema, kwa makadirio ya makusanyo ya mwaka 2011, kitabu hiki ni cha 2013, kimefanyiwa utafiti, kati ya shilingi trilioni 6.4 ambazo zilitakiwa zikusanywe na *TRA*, imethibitika kuwa ni watu ama makampuni, ama Taasisi mia nne tu zinazolipa *direct tax* Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kinaendelea kueleza hao wana-*contribute 80% tax revenues* za nchi hii na inakwenda mbele inasema inakadiriwa Watanzania milioni 13, hawalipi *direct tax*, kitabu mnacho, tunaambiwa kuna taarifa hapa za vyanzo vipya vya mapato, lakini ni wavivu wa kufikiri, hatuangalii vyanzo vingine tunaangalia kumnyonya Mtanzania kwa kodi nyepesi kwa kuona, lakini nzito na mzigo kwa Watanzania maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niishauri tu Serikali na muwe mnasikiliza na kama hamshauriki basi mtoke! Kwa sababu haiwezekani tunawaahidi Watanzania maisha bora, lakini miaka inavyozidi kwenda, Watanzania wanazidi kupigika, kitabu mnacho aidha, wataalam wamefanya utafiti mzuri, fanyeni kazi tujenge nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa amezungumza kuhusu misamaha ya kodi, nipongeze kidogo kwa hatua ya Serikali ya kusema kuwa itaangalia misamaha ya kodi, nipongeze japo kwa hatua, lakini misamaha ambayo wameonekana kuizungumzia sana ni kituo cha uwekezaji, *TIC* na masuala ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, lakini taarifa ya *CAG* ya mwaka huu inaonesha kuwa, kati ya Trilioni 1.8 ya misamaha ya kodi, ambayo ni sawa na 27% ya mapato ya mwaka ya *TRA* mapato ya kodi, hivi akili inakuambia kwa umaskini walionao wananchi wako *TRA* inakusanya mapato yake kwa mwaka 27% of it ni misamaha, *does it make sense? It doesn't make sense 4.5%* sijui ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nchi maskini, mmechoka, Uganda inakimbia, Kenya inakimbia, Rwanda inakimbia, wao misamaha ya kodi haizidi hata 1% ya *GDP*, sasa tunawaambia hamsikii. Lakini hao *TIC* ambao wanazungumzwa sana, ukiangalia taarifa ya *CAG*, wao

misamaha yao ni bilioni 280 tu kati ya trilioni 1.8. Ukija hapa unakuta kuna makampuni ya watu binafsi kuna bilioni 304 watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuna hisia zilikuwepo kuwa taasisi za dini zinapewa misamaha mikubwa kwa sababu ndiyo zinatoa huduma za mashule na mahospitali, lakini taarifa za CAG zinaonesha kwamba, kumbe taasisi za dini msamaha ni milioni 438 tu, kwenye hizi bilioni 304 ni makampuni yenu ya kimagumashi, mnaunganisha ma- *network*, mnapeana misamaha, matokeo yake ni kwamba, mzunguko wa fedha unabaki kwenu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri wa Fedha pamoja na mambo mengine atuambie mikakati gani ipo ya kuondoa misamaha ya kodi kwa watu binafsi, ni mikakati gani ipo kuondoa misamaha ya kodi kwa miradi ya wafadhili ambayo imeongezeka kutoka bilioni 115 mpaka bilioni 229, mtueleze. Kwa hiyo, niombe Serikali inawezekana Waziri ana nia njema na kwa kweli anaonekana ana nia njema, lakini Mzee wangu sijui kama hayo mazingira yaliyomzunguka ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuzungumza, la mwisho, ni Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na naomba Waziri mwenye dhamana alifanyie kazi. Tumeambiwa mwaka huu wa fedha ilikusanywa 49% tu ya lengo, lakini nyie mnajua kuwa Serikali za Mitaa zina vyanzo vikubwa vya mapato.

Mheshimiwa Spika, makampuni hawalipi *Service Levy*, 0.3% hailipwi na Halmashauri zinalalamika kwamba *TRA* haitoi ushirikiano kwa kuwa ina-*collude* na wenye makampuni, hawatoi taarifa zilizo sahihi. Kinondoni tuna wawekezaji wengi sana, lakini nenda kafanye uchunguzi ni kwa kiwango gani cha *City Service Levy* kinalipwa cha 0.3% kwa yale makampuni makubwa, *you will be surprised*.

Mheshimiwa Spika, kuna *collusion* kubwa kati ya wafanyakazi wa *TRA*, makampuni husika, *annual turnover* hapa inaandikwa ya uwongo, matokeo yake Halmashauri hazipati vyanzo sahihi. Namwomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie, litasaidia kwa kiwango kikubwa sana kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, masuala ya pikipiki, zile tozo inawezekana ikatumika kama siasa, mkifikiria kuwa wale vijana wanaoendesha pikipiki ndiyo wamiliki wa pikipiki, *thus cheap politics*, hizo ni siasa nyepesi, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba, kama kuna wamiliki wa pikipiki, wale vijana hawazidi hata 2%, hii 98% tunamwachia nani? Muache siasa nyepesi, muache kutaka *cheap popularity* angalieni ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu nawafahamu wanamiliki pikipiki na bodaboda zaidi ya hamsini, wengine wana mia. Mngekuwa mna nia ya kuwasaidia vijana mngempunguza mafuta, ukipunguza bei ya mafuta tafsiri yake ni nini? Yeye ule mshiko ambao anatakiwa apeleke kwa tajiri yake kwa wiki moja kwa sababu bei ya mafuta iko chini anaweza akapata salio.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niionbe Serikali...

MBUNGE FULANI: Wataje.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kwa hiyo, niionbe Serikali kama mna nia njema ya kuwasaidia vijana wetu wa bodaboda, punguzeni bei ya mafuta, mkipunguza bei ya mafuta hata mfumuko wa bei ambao unachangiwa 50% na... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zambzi, atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia mambo machache kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha *(The Finance Bill)* ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha na timu yake, lakini pia na Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Ni vizuri tukakiri tu kuwa wamefanya kazi kubwa, ingawa haiwezi kuwa asilimia mia moja, lakini tumepiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Spika, kusema kuwa kuna watu wamepiga kura ya ndiyo kwa bajeti wakati ingeweza kukataliwa, nadhani siyo sahihi kwa sababu wote tuko hapa, tunaomba bajeti hii ili twende kutekeleza miradi ambayo iko kwenye Majimbo yetu na kuwaletea Watanzania huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna watu ambao wamekuwa wanalia hapa kuwa Majimbo yao yanahitaji huduma ya Maji, yanahitaji nini, lakini wakisimama hapa wanakataa bajeti. Sasa tukikataa bajeti ya hizo huduma za maji, za umeme zitatekelezwa kwa fedha kutoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani kama zipo kasoro tuelekeze kukosoa zile kasoro, lakini siyo kwa madhumuni ya kukataa bajeti ya Serikali, naomba nichangie mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nimejaribu kusoma vitabu vyote ambavyo tumepewa kwa ajili ya bajeti hii, lakini najua maeneo ambayo Serikali inapata gawio lake, kwa mfano, najua kuwa Serikali ina *shares* nyingi katika Benki ya *NMB*, Serikali ina *shares* nyingi tu katika *Twiga Bankcorp*, Serikali ina *shares* nyingi *Postal Bank*, lakini kuna Taasisi nyingi ambazo ziko chini ya *Treasurer Registrar*, sijaziona popote zilipo orodheshwa na kwamba zinatakiwa zichangie kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, sasa huku tunazungumza kuwa tuna upungufu wa pesa, lakini Taasisi hizi huwa zinachangia, tumeshafunga bajeti, hizi pesa zitaingia wapi na zitatumika kwa idhini ya chombo gani wakati kimsingi Bunge tumeshapitisha bajeti ya Serikali. Sitaki kuamini, hivi kweli Waziri na timu yake, pamoja na wataalam wote wamelisahau hili au watatueleza kuwa ni *oversight*? Siwezi kuamini kuwa ni *oversight unless* kuna sababu nyingine.

Mheshimiwa Spika, na naomba Waziri atakapokuwa ana *windup* sasa atueleze hizo Taasisi zinatoa gawio gani kwa Serikali maana umehangaika hapa na Wakala wa Serikali kukatwa 10% kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na hizi Taasisi ambazo zinachangia kiasi kikubwa kwa nini mmezisahau wakati kila mwaka zimekuwa zikitupa gawio la Serikali?

Mheshimiwa Spika, nadhani kulihitaji uangalifu mkubwa sana wakati Waziri na timu yake wanashughulikia hili, lakini sitaki pia kuamini kuwa Kamati ya Bajeti haikuliona hili, maana wangeliona wangeweza hata kuandika kwenye taarifa yao kuwa, ni eneo lingine ambalo Serikali sijui kama ni kwa kupitiwa au namna gani waliacha kuweka kabisa Taasisi ambazo zinachangia fedha nyingi tu kwa ajili ya kuingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*windup* hapa atueleze kwa nini iko hivi, lakini pia Taasisi hizo zinachangia shilingi ngapi na zinachangia kiasi gani kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie na limezungumzwa sana na wenzangu wengi na Kanuni zetu zinakataza kurudia, lakini ukiona Wabunge wengi wanazungumzia, maana yake kuwa jambo hili lina umuhimu sana, sikubaliani kabisa na ongezeko lolote kwenye mafuta hasa dizeli na *petrol*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sikubaliani kabisa na hilo tukiongeza bei na tulishachangia huko wakati tunazungumzia bajeti nzima ya Serikali, tulishasema ukiongeza ongezeko lolote kwenye mafuta dizeli na *petrol* maana yake unawagusa Watanzania wote, ni tofauti na ongezeko unaloweza kuchukulia kwenye simu au kwenye nini, lakini kwenye mafuta unagusa maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, sisi tulifikiri kuwa siyo vizuri kugusa mahali ambapo unajua kabisa kuwa athari zake zinakwenda kwa wananchi wa Tanzania, wananchi maskini wa nchi hii, awe amekaa kijijini huko, lakini bidhaa atakayoinunua bado itakuwa imechangiwa bei yake kuwa kubwa kwa sababu ya ongezeko katika bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, hili tulishalizingumza sana na nimekuwa nina-*interact* na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wameishauri sana Serikali, lakini naona Serikali katika hili imeziba masikio, kwa nini tuzibe masikio? Siyo vizuri, nalizungumza hili nikijua kuwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inayoongoza, lakini kama

unaongoza Watanzania hawa waliokuamini, wakakupa kura nyingi, wasikilize basi na timiza matakwa yao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukinyamaza, tusiposema Wabunge wa Chama cha Mapinduzi itaonekana kuwa sisi tunashabikia Serikali kwenda kufanya maisha ya Watanzania yakawa magumu zaidi, jambo ambalo siamini kama Wabunge wa CCM tunashabikia hilo, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali na Waziri wa Fedha na kama nimemsikia vizuri Mheshimiwa Spika kuwa jambo hili litakwenda mpaka kesho, basi mna muda wa kutosha, tuondoeni tozo ambayo mnaipeleka kwenye mafuta, ili angalau Watanzania waone kuwa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi kuwa inawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza, ni suala la msamaha wa kodi. Misamaha ya kodi ni mingi sana, niliwahi kuchangia wakati mmoja hapa kuwa CAG alishawahi kuishauri Serikali tupunguze misamaha ya kodi na kwenye ukaguzi wake wa mwaka 2010/2011 kama sikosei misamaha ya kodi ilikuwa karibu trilioni moja, lakini mwaka uliofuata 2011/2012 misamaha ya kodi imekwenda mpaka trilioni 1.8.

Mheshimiwa Spika, wakati anashauri tupunguze misamaha sisi tunaiongeza, najua azma ya Serikali ni nzuri ya kwamba, tupunguze misamaha ya kodi. Kwa hiyo, tunaomba hili litekelezwe mara moja na tuone kwenye bajeti ya Serikali inayokuja 2014/2015, basi misamaha hii inapungua ili pesa hizo ambazo zinatumiwa ziende kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri alituambia wakati mwingine maeneo mengine Sheria ambazo tumezitunga, ndiyo tatizo. Tulishashauri kama Sheria hizi ndiyo tatizo, zileteni kuna Mkutano wa Nane wa Bunge mngelizeta hizo Sheria na nyie msichukue muda mrefu zaidi, wakati wenyewe mnalalamika kuwa ni tatizo ni Sheria, lakini hamtaki kuzileta hapa Bungeni angalau tuweze kuzirekebisha na muweze kupunguza misamaha ya kodi, tukusanye pesa nyingi zaidi twende kwenye shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuiombe Serikali tunapunguza misamaha ya kodi, Serikalini humo humo mnaanza kuandikiana vi-*memo* huyu mpe msamaha na hili ndilo tatizo, yapo mambo ambayo tunakubaliana ya Kisheria, lakini vi-*memo* vya wakubwa ni vingi kweli, huyu muondoleeni msamaha, muondoleeni msamaha. Naiomba Serikali kama tukishakubaliana kuwa hili tumelifunga, basi tuwe tumelifunga, itakuwa inasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni masuala ya tozo kwa wanyama wetu ambao wanawindwa. Hili eneo limekuwa likilalamikiwa sana kwamba, kodi ambazo zinatozwa au ushuru unaotozwa kwa ajili ya wanyama wetu wanaowindwa ziko chini sana kuliko nyingine ambako wawindaji wanakwenda.

Mheshimiwa Spika, wanakuwa wanakimbilia sana Tanzania kwa sababu wameona kwamba ushuru tunaotoza kwa ajili ya wanyama wanaowindwa ni mdogo sana. Nilitegemea Waziri aje hapa aseme kwa mfano, mtu anayewinda tembo, mtu anayewinda pundamilla, wanatozwa kiasi gani viwango ambavyo vinasemekana ni vidogo sana na pia kulinganisha Botswana wana-*charge* kiasi gani, South Afrika wana-*charge* kiasi gani, mahali pengine wana-*charge* kiasi gani na Tanzania tuna-*charge* kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli upo kwa sababu tumesikia pia Kamati inayohusika imekuwa ikilia sana kuwa viwango viko chini sana. Watanzania wanalalamika wanyama wetu wanakwisha kwa sababu tumeweka tozo kidogo sana na watu wanakuja, wameona hapa ndiyo pa kukimbilia kuja kuchuma pesa kwa ajili ya shughuli za uwindaji. Kwa hiyo, naiomba Serikali ije na viwango ambavyo tunatoza kwa ajili ya wanyama wetu ambao kila siku wanazidi kuuawa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza kidogo ni suala la uingizaji wa magari. Ni kweli magari siyo anasa, kwa hiyo, naomba Serikali ipunguze viwango vyake iviangalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, naona muda umeniishia, nakushukuru sana.
(*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona kuna *vi-note* vinakuja, utaratibu wetu wa kujaza *form* mwanzoni ndiyo unaotumika hapa. Kwa sababu inaelekea kuna *Ammendments* nyingi zinatakiwa kuletwa. Kwa hiyo, ni lazima tufunge mjadala jioni ili kesho tuendelee na maamuzi katika Kamati ya Bunge zima.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, bahati mbaya wakati nasitisha shughuli mchana sikuwataja ni nani wataendelea, lakini namwona Mheshimiwa Christina Mughwai mmojawapo, namwona Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Mussa Zungu na Mheshimiwa Ester Bulaya pia aliomba. Mheshimiwa Christina Mughwai!

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea mambo machache. Jambo la kwanza, ni ongezeko la ushuru wa mafuta linalopendekezwa na Muswada huu. Wasemaji wengi wameongelea suala hili na hii inaonesha umuhimu, unapopandisha bidhaa ya mafuta ya *diesel*, *petrol* na mafuta ya taa ni kwa namna gani unaathiri uchumi na maisha ya wananchi wa Tanzania. Ndiyo maana watu wamepiga kelele, watu wamelisemea kwa nguvu na sitatenda haki kwa wananchi wangu hasa wa Mkoa wa Singida kama sitapinga suala hili la kuongeza ushuru wa mafuta kwa sababu zinazojieleza.

Mheshimiwa Spika, unapoongeza bei za mafuta, unajua kwamba, uta-*affect* sekta mbalimbali za uchumi, nauli kwanza za usafiri kwa abiria zitapanda, nauli za kusafirisha mizigo zitapanda na

bidhaa mbalimbali zitapanda kwa sababu sasa zitasafirishwa kwa bei kubwa kutoka eneo moja hadi lingine. Wananchi watahondwa kumudu gharama hizi, hususani mazao Serikali ya CCM inasema kwamba, Kilimo Kwanza, lakini ukipandisha bei ya mafuta ni wazi kwamba, mazao yatahondwa kuhamishwa kutoka mashambani kwenda sokoni na hivyo wananchi watahondwa kumudu gharama za mazao hayo na hasa chakula.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nizungumzie suala linalopendekezwa la kuongeza ushuru wa aina mbalimbali katika huduma mbalimbali zinazotolewa na makampubi ya simu. Huduma za simu zimerahisisha sana mawasiliano katika nchi hii na hasa kwa wananchi wa vipato vya chini.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wananchi wa kipato wanaweza wakawasiliana mpaka vijijini kwa kutuma ujumbe au kutuma ujumbe unaosema tafadhali nipigie kwa wale ambao hawana hata salio lolote katika simu zao. Sasa tunaambiwa kwamba huduma hizi zote zitatozwa ushuru, ni dhahiri kwamba ushuru wa huduma hizi katika masuala ya mawasiliano ya simu za mkononi, utawafanya wananchi walio wengi hasa wa kipato cha chini washondwe kumudu gharama za simu na watahondwa kumudu mawasiliano na tunajua kwamba mawasiliano ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria kundi la vijana wengi ambao hawana ajira, vijana hawa wamekuwa wakitumia mitandao hii ya simu na *internet* kwa kiasi kikubwa katika kuwasiliana. Vijana hawa ambao Serikali inasema imewapenda sana katika hotuba hii ndiyo wanategemea mitandao hii ya simu ya mawasiliano ili waweze hata kutafuta taarifa mbalimbali, waweze kujitafutia ajira kwa maana kwamba huko majumbani au hawana hata ofisi wanapoweza kusoma magazeti.

Mheshimiwa Spika, lakini taarifa zilizopo katika mitandao ya simu, zinawafanya vijana walio wengi wapate taarifa mbalimbali, waweze kutafuta kazi na kuwasiliana na maeneo mbalimbali. Lakini huduma hizi zikitozwa kodi, zitafanya kundi hili kubwa lishondwe kuwasiliana na watahondwa kutumia hizo huduma na hatimaye Serikali itakosa haya mapato ambayo inayatarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuongeza ushuru wa huduma za kutumia barabara kwa magari yote kwa kiwango cha shilingi elfu hamsini kulingana na aina ya gari. Hili nalo ni tatizo. Japokuwa tumeambiwa kwamba haitawahusu watumiaji wa bajaji na bodaboda, lakini kama wasemaji waliotangulia walivyosema, vijana ambao tunawaona wanaendesha hizo bodaboda na bajaji wao siyo wamiliki, wao ni watumiaji tu.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba hili kusudio la punguzo linaloelezwa na Serikali halitawanufaisha hawa bodaboda wala bajaji, litawanufaisha wamiliki wa bajaji ambao wengi ni miongoni mwetu hapa sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona punguzo la mafuta na *road license*, kwanza katika *road license* pamoja na ongezeko hilo la 50,000, tunajua kwamba, tozo hii inatozwa hata kama gari haifanyi kazi, gari inaweza kuwa imepaki hata mwaka mzima haifanyi kazi yoyote, haizalishi pato lolote lakini siku litakapofufuliwa mwenye gari hilo akienda *TRA* anahesabiwa makato ya *road license*, huu ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali au *TRA* waje na utaratibu ambao utaeleza ni namna gani *road license* haitatozwa pale ambapo gari haikufanya kazi popote na waweke utaratibu wa kujua namna ambavyo ushuru huu utatozwa kwa uhalali bila kutoza wale ambao magari yao yamekuwa hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala limeongelewa pia la malighafi inayotengeneza sabuni ya unga ikijulikana kama *LABSA*. Naunga mkono ongezeko la asilimia kumi kwa maana kwamba, litaongeza pato la Taifa, lakini vilevile italinda viwanda vya ndani. Ni nia nzuri kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, unapoweka ushuru wa sifuri katika malighafi yoyote ile, kama una viwanda vinavyozalisha malighafi hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba, viwanda vyako vya ndani vitashindwa kushindana na bidhaa zitakazoingizwa kutoka nje, kwa sababu kutoka na ughali wa maisha na ughali wa gharama za uzalishaji nchini, viwanda vya ndani vinavyotengeneza *LABSA* vitashindwa kuhimili ushindani wa bidhaa zitakazoingizwa bila ushuru. Kwa hiyo,

napendekeza na naunga mkono ongezeko la asilimia kumi katika malighafi ya LABSA inayotengeneza sabuni za unga.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani mara nyingi tumeshauri juu ya vyanzo vipya vya mapato, lakini Serikali imekuwa haisikii. Serikali wamekuwa kila mwaka wanakileta vyanzo vile vile vya bia, mafuta na hivi moja kwa moja vinakwenda kuwadhuru wananchi, wananchi wanashindwa kuhimili sasa mzigo huu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasikiliza redio, wananchi wanasema kwamba, siku hizi hata mtu akinywa chai asubuhi, wanakatiana andazi moja watu wawili, hivi haya kweli ndiyo maisha bora kweli kwa kila Mtanzania? Katika hali hii utasemaje unaongeza ushuru wa mafuta, unaongeza ushuru wa simu vitu ambavyo vinamgusa mwananchi wa kipato cha chini kwa kila siku, lakini tulipendekeza vyanzo vipya.

Mheshimiwa Spika, Serikali safari hii imekuja na mpya kabisa, moja ya vyanzo vyao vipya wanasema wachaji vipodozi. Hivi kweli Serikali wamekaa wakatafakari kwamba, wakatoze kodi kwenye vipodozi vya akinamama! Ni kiasi gani cha kodi kitapatikana katika vipodozi hivyo?

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe napaka vipodozi, lakini naamini kwamba, Serikali haikufanya *homework* yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna majengo makubwa yanaonekana hata kwa macho tu, kuna watu wanavua *deep sea* hawatozwi ushuru wala hamna mtu anayewafuatilia, hatujaona sekta ya madini na mawasiliano inachangia kiasi gani, leo hii wewe ukasema eti unamtoza mama poda au wanja wake aliopaka. Hii ni nini kama siyo usumbufu, kwanza hatutapata kodi tunayotarajia, hata hela tunayotarajia, lakini ni usumbufu wa kundi kubwa la watu ambao haina sababu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, tumependekeza mara nyingi na Kamati zako ulizounda zimependekeza maeneo ambayo yatalipa ushuru bila kuwasumbua wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, majengo yanaonekana, wamiliki wake wanajulikana lakini Serikali inakuwa na kigugumizi kuwatoza...

SPIKA: Ahsante, muda wako umekwisha ni kengele ya pili. Mheshimiwa Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour pamoja na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed. Mheshimiwa Zungu!

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kwanza nipongeze Mamlaka ya Mapato *TRA*, nimpongeze *Commissioner General*, *Deputy Commissioner General* na Watendaji wote kwa umakini wao wa kufanya kazi na kulipatia Taifa mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia hapa Waziri leo akizungumzia kuhusu bodaboda na bajaji hazitatozwa kodi na baadhi ya Wabunge tumeshangilia sana kisiasa. Unapomfanya mfanyabiashara yeyote wa chini au wa juu kutokotozwa kodi, matokeo yake ni kumfanya huyu kukosa huduma muhimu za kijamii wakati atazihitaji na wakati Serikali sasa hivi uwezo wake ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue mfano mdogo wa Kenya, ambao sasa hivi Serikali ya Kenya inakusanya kwenye sekta ambayo siyo rasmi, trilioni nane na bilioni mia tano ya kodi. Hizi zinatokana na *presumptive tax* kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao ni *Machinga*, *welders*, mamalishe na kadhalika. Watu wanaweza wakalipa laki moja kwa mwaka kuisaidia Serikali kupata siyo chini ya trilioni moja na kuweza kuifanya Serikali iweze kukusanya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoanza kuchekelea watu wasilipe kodi hii tunajiingiza katika matatizo makubwa sana kwa siku zinazokwenda. Mtu ukitaka maendeleo, ukitaka barabara nzuri, huduma za hospitali ni lazima wananchi tuna wajibu wa kuchangia. Tunaacha walipa kodi wakubwa tunaanza kukimbizana na walipa kodi wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ijaribu kutazama mawazo yaliyotoka kwenye Kamati ya Kodi ambayo na mimi nilikuwa Mjumbe, Serikali ipitie isipuuze ripoti kama hizi na Watendaji wa

Serikalini wasione kila kitu wanajua wao tu peke yao, wanapoelezwa kitu wanakuja na majibu mbadala halafu inaishia pale pale. Wasikilize wadau wengine ambao wanaelewa namna gani vitu hivi vinavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, sioni sababu ya kuongeza kodi ya mafuta, sasa hivi hali ilivyo, kodi bado iko juu sana, ziko njia mbadala za kumfanya mtu ambaye hawezi ku-*feel* kwamba analipa kodi ya mafuta. Kwa nini tusianze ku-*introduce road toll*, ni nani atakayeshindwa kulipa *toll* ya barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma shilingi elfu kumi? Kwa hiyo, nafikiri Serikali ingetazama eneo hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwenye *excise duty* kwenye vinywaji baridi kama soda na juisi. Sisemi kusiwe na kodi kwenye *excise duty*, tupunguze *excise duty* ili *compliance* iwe kubwa. Mauzo sasa hivi ya ya makampuni haya yamekuwa chini, unywaji wa vinywaji hivi umekuwa chini kutokana na watu kushindwa kumudu. Leo wananchi wengi Tanzania soda wanaiona kwenye mabango tu, maji safi wanashindwa kunywa.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam watu wanakunywa maji yanaitwa maji ya Kandoro yanayotembezewa mitaani. Gharama za huyu mtu akipata maradhi ya tumbo kwenda hospitali ni kubwa. Kwa hiyo, nafikiri upo umuhimu wa Serikali kupunguza *excise duty* ili *compliance* iwe kubwa, watu wengi waweze kunywa soda hii na mapato ya Serikali yataongezeka zaidi ya haya ambayo sasa hivi wamekusanya.

Mheshimiwa Spika, haya makampuni yana-*create* ajira, kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kutazama makampuni haya ambayo yanazalisha ili wapunguziwe kodi, lakini wengi waweze kunywa soda na maji ili mapato yaongezeke.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Ufaransa imepunguza *capital gain tax*, na nchi nyingi za Ulaya zinapunguza *Capital Gain Tax* ili watu wa-*comply*, leo Tanzania watu wanauza mali zao lakini hawalipi kodi kwa sababu kodi ipo juu sana. *Capital Gain Tax* ikipunguzwa, wananchi wengi watakuwa na uwezo wa kulipa.

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo, hapa karibuni Serikali ilijichanganya humu ndani, hoteli ya *Movenpick* imeuzwa, amenunua *Aghakhan Foundation* na imeuzwa na aliyekuwa anaimiliki hoteli hii na sasa hivi inaitwa Serena, hakuna hata senti tano Serikali imepata, hata senti moja Serikali imepata. Hii inatokana na viwango vilivyowekwa ni vikubwa, vya kutisha ambavyo vinawafanya watu washindwe kuweza ku-*comply*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi za pango; Kariakoo peke yake kuna *potential* ya kukusanya *rent tax* siyo chini ya *fifteen billion shillings* kwa mwaka, lakini hizi nazo hazikusanywi zote sababu hawana *capacity* au nafasi ya kwenda kuwa-*engage* hawa watu, Serikali inakuwa yenyewe inaji-*census*.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijaribu kutazama, wapitie ripoti ya kodi ya Kamati yako uliyoiunda, waipitie kwa uangalifu mkubwa sana waweze ku-*capture* maeneo ambayo ni *potential revenue* ya Serikali kwa sasa na kwa miaka mingine inayokuja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza *Skill Development Levy* ipungue, Serikali imepunguza kutoka sita *to five*, bado hii ni kubwa. *Compliance* yake inakuwa ni ndogo, mashirika mengi hawalipi hii kodi kwa sababu wanaogopa, wanapata hasara kubwa sana. Wakiishusha hii zaidi kutoka sita mpaka nne *compliance* itakuwa ni kubwa na itafanya makampuni mengi yalipe na Serikali itaweza kupata hizi pesa katika Mfuko wa Elimu na Mfuko wowote mwingine watakaoweza kuuweka kwa wafanyabiashara wengi na makampuni mengi kuchangia Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Fedha ajaribu kutazama, inawezekana siyo mwaka huu, lakini watazame sasa ni namna gani ya kupunguza hii *Skill Development Levy* ili makampuni mengi yaweze ku-*comply*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Waziri ameona wazo la Kamati ya Kodi kuhusu makampuni ya simu, kuna mjumbe amezungumza kuhusu vijana wanatumia simu. Ni kweli, lakini vijana hao wanaotumia simu, hawainufaishi Serikali yao, wananufaisha ma-*operator*. Sasa Serikali haimuumizi tena mtumiaji simu bali Serikali inakwenda kudai kile cha kwake ambacho kinastahili kulipwa na

miaka mingi kilikuwa hakilipwi kwa sababu sheria ilikuwa hairuhusu Serikali ikusanye pesa nje ya *voice calls*.

Mheshimiwa Spika, *future development* ya simu ni *value added services, downloading ya data* ambayo sheria zetu zilikuwa haziruhusu ku-*capture* na mapato mengi sana ya makampuni haya, yalikuwa yanapatikana kutokana na hizi *data downloading* na Serikali ilikuwa haipati. Sasa Serikali imeweka kiwango, tumeanza na kiwango kidogo, lakini inategemea siku za mbele tutaweza ku-*capture* mapato mengi sana.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la *levy* kwenye *transaction* za pesa, leo Watanzania wanazungusha 1.7 trillion shillings kwa mwezi kwa kutumia jamaa zao na Serikali hii haipati senti tano kwenye mzunguko huo. Leo Waziri ameweka sheria na nampongeza kwa kukubaliana na Kamati ya Kodi kuwa sasa hivi kuwe na kiwango ambacho Serikali itapata. Nimeambiwa pesa hizi zitakwenda kwenye *REA* hakuna ubaya, lakini isitazamwe *REA* tu.

Mheshimiwa Spika, Kenya wenzetu baada ya maandamano ya Walimu wameweka *transaction* ya *ten percent* kwenye mzunguko wa pesa na wana-*potential* ya kupata dola milioni mia tatu takribani bilioni mia tano. Hizi wao wamezitenga ziende kwa Walimu na sisi ilimradi tumeshaanza mpango kama huu, tutazame Walimu, tutazame Madaktari, tutazame Watumishi wa Umma wote kwa pamoja ili na wao wanufaike na mapato haya yatakayopatikana.

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali ina nia nzuri waiagize *TRA airtime importation* ya makampuni ya simu, value yake haifahamiki bandarini. Wanaagiza *Airtime* ya bilioni 20, watu wa *TRA* wana-*clear* mzigo kama *consignment*. Lakini *value* ya mzigo haifahamiki. Siyo rahisi Serikali kupata kodi yake kama mzigo unaingia nchini hawajui *value* yake. Kwa hiyo, wanavyosubiri kadi hizi ziwe *activated* kwenye simu, iko hatari vile vile makampuni haya ku-*under declare traffic*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sehemu nzuri ya kupata mapato ya Serikali ni kwa *importation* ya vocha hizi pale pale bandarini au *point of entry* Tanzania ili sasa wajue *value* ambayo ilikuwa

imported. Ziko vocha zinatengenezwa Tanzania, ziko *transfer* za *electronic voucher* za Tanzania. Hizi nazo zinafahamika tu wakati wa *activation*. Ukishaingiza kwenye *activation*, haya makampuni yana uwezo mkubwa sana wa ku-*under declare*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali itazame vizuri na TRA wabadilike, uwezo wao bado wa kuelewa masuala ya mitandao bado ni mdogo. Iwe ni changamoto kwao sasa ku-*train watu*, waelewe *industry* hii ili waweze kufanya *forensic auditing* ya makampuni haya na kuweza *capture* pesa ambazo Serikali inataka ipate ili iweze kusaidia watu wake.

Mheshimiwa Spika, kuna kampuni moja tu Kenya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Hiyo ni kengele ya pili.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mohammed Mbarouk. Dakika tano, tano.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa yale maeneo ambayo tumeyapigia makelele na akaweza kuyafanyia ufumbuzi na namwomba kwa yale maeneo yaliyobakia ayafanyie pia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa John Chenge kwa kutuongoza vizuri. Sasa nitaanza kuchangia baadhi ya maeneo. Kwanza nitaanza kuanzishwa kwa ada ya *money transfer* 0.15. Hii ni ada nzuri na itaweza kutupatisha mapato mengi kwenye Sekta hii. Lakini tatizo langu naliona kwa kuwa Sheria hii itafika mpaka kunako *M-Pesa*.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi ukituma pesa kupitia *M-Pesa*, tayari unachajiwa. Halafu inakuja na *zero point one five percent* ati ajue

huyu mtu na watu wanaotumia hii *M-Pesa* ni watu maskini, wasiokuwa na uwezo. Je, hii si itakuwa *double taxation*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba katika Sheria hii Mheshimiwa Waziri aende mbele zaidi aweke kipengele ambacho kitazungumza kwamba, *M-Pesa* zisiweze kuchajiwa. Anao Wanasheria wa kutosha kwa kutumia *excluding M-Pesa* au chochote atakachokiingiza pale, lakini ahakikishe watu wanaotuma *M-Pesa* wasichajiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuja kwenye ushuru wa magari yaliyokaa zaidi ya miaka 10. Haya ni magari ya wanyonge. Tumempigia kelele sana Mheshimiwa Waziri kwamba, watu hawana uwezo wa kununua magari mapya. Magari mapya thamani yake ni mara kumi ya haya magari ya miaka kumi. Kwa nini Mheshimiwa Waziri asiache hii ada ya asilimia 20, akataka lazima twende kwenye asilimia 25? Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hii na aweze kuifanyia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nakuja sas kwenye suala la wafanyabiashara ambao hawatunii zile mashine. Hili ni jambo zuri sana kwa sababu wakwepaji kodi watapatikana na wataweza kushtakiwa na kupata adhabu. Ambapo adhabu hiyo kwa kosa la kwanza utalipa asilimia tano ya mauzo uliyoyauza. Kosa la pili utalipa asilimia 10 ya mauzo uliyoyauza na kosa la tatu utalipa asilimia 20 kwa kosa ulilonalo.

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaliona hapa ni kwamba, wafanyabiashara wengi bado hawajaweza kumudu kununua hizi mashine. La pili, haijatoka elimu ya kutosha kwa umuhimu wa kutumia hizi mashine kwa wafanyabiashara. Ninaloliona hapa ni kuwapa ulaji watu wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, hii sheria itakuwa inawapa ulaji watu wa *TRA*, watabaki kule Kariakoo watavizia maduka, mtu akimkamata hana ile stakabadhi watamwambia mfanya biashara atoe kitu kidogo au watampa adhabu hiyo. Kwa hiyo naona Sheria hii bado wakati wake. Kwanza itolewe elimu ya kutosha kwa wafanyabiashara na mhakikishe angalau *three quarter* ya wafanyabiashara wanazo hizi mashine.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali pamoja na Mheshimiwa Waziri. Nilisema wakati wa kuchangia Bajeti, suala la uchakachujaji, sasa nampongeza sana Waziri suala hili amelipatia ufumbuzi. Pamoja na hayo sijui kama itawezekana, lakini naomba na mafuta ya taa ile bei ni kubwa mno, ipunguzwe. Maana yake Mheshimiwa Waziri anaposema kuhusu suala la uchakachujaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rajab!

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, dakika tano!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nataka nielekeze pongezi zangu kwa Serikali hususan Wizara ya Utumishi kwa kupata tuzo ya utumishi bora katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niende moja kwa moja katika hoja na nataka nianzie na suala zima la LABSA. Kwanza, tutakuwa ni nchi ya ajabu na nafikiri ni nchi ya kwanza hapa duniani kuona mfanyabiashara anakuja anakwambia niongezee kodi asilimia 10. Hili ni jambo la kushangaza, ni jambo ambalo kwa kweli Mheshimiwa Waziri inabidi alifikirie mara kumi kumi. Hivyo kweli leo wafanyabiashara hawa wa sabuni wanamjia wanamwambia hebu tuwekee kodi, amewahi kuona wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ilitokea wa enzi za Mitume, wakati watu ni waadilifu, sio leo. Hao hao ambao leo wanakwenda kumwambia awawekee kodi, ni hao hao ambao wanakwepa kodi nyingine. Namwomba Mheshimiwa Waziri achunge uwezo wake, kwa kuchunga namna anavyowajibika. Mheshimiwa Waziri ahakikishe anakuwa makini sana na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, leo kundi la wafanyabiashara waje kumwambia Mheshimiwa Waziri awawekee kodi kwa asilimia

10. Aah! Hiyo haijawahi kutokea. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hili aliangalie sana na wala si jambo la kulijadili.

Mheshimiwa Spika, anapoweka kodi katika LABSA, tayari ameshaua viwanda vyetu vidogo vidogo, ameshaua viwanda vya kati. Hawa wanaokuja kwa ajili hiyo wana *interest* zao, hawa ni *ma-agent* wa nchi nyingine wa viwanda vya sabuni. Leo tumeweza kudhibiti, wafanyabiashara wadogo wadogo hapa wanauza sabuni nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, leo zianganalie sabuni hapa kutoka nchi nyingine, ziko wapi, hazionekani kwa sababu soko letu linajitosheleza. Wanakuja kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba tuwekee asilimia 10. Lengo lao ni kutaka kuidhibiti hii biashara, ili iwanufaishe wao pamoja na hao ambao wanawafanyia kazi kutoka nchi za nje. Mheshimiwa Waziri nakuomba hili tena nakuomba sana hili halikubaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende katika suala la upandishaji kodi mafuta. Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha bajeti yake hapa alisema kwamba yako makampuni saba makubwa ya uchimbaji madini hapa nchini ambayo kwa mwaka 2013 yameweza kuchangia bilioni 251.8 na akataja zile *tax* ambazo wanalipa. Bodi ya Mfuko wa Barabara imelalamika mara kwa mara na inaendelea kulalamika, Makampuni haya saba Mheshimiwa Waziri hayatozi *road toll*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini hadi leo hawa hawatozwi *road toll*, wakati sisi watu wa kawaida tunatozwa sh. 200 katika kila lita? Kitu gani kinamkwamisha Mheshimiwa Waziri? Haya makampuni ndiyo ambayo yanatuharibia barabara zetu. Wanatupotezea bilioni 26 kwa mwezi. Leo tunakuja kuongeza ushuru katika mafuta ya taa!

Mheshimiwa Spika, yule bibi yetu kule Njombe ambaye ni Mkunga wa kawaida anatumia sijui mnaita kibatari, sijui koroboi ndiyo hilo hilo. Yeye anatumia mafuta ya taa au taa yake ya kandili inayotumia mafuta ya taa, wala hajui habari ya umeme. Mheshimiwa Waziri hapa angalau anatumia umeme na sasa hivi anategemea kuuongeza nguvu kwa kutumia gesi. Bado wako watu ambao wanahitaji mafuta ya taa. Mheshimiwa Waziri ayabane

makampuni haya, yalipe *Road Toll*, atapata pesa bilioni 26 ziko hapa, kila mwaka zinapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya makampuni hayalipi *road toll* na yanatuharibia barabara zetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie viuri na ikiwezekana haya mafuta ya taa basi tuweze kuyateremsha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Ukaona Njombe ndiyo pa kufanyia mfano. Haya! (*Kicheko*)

Nimwite Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Soni.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ingawa siko vizuri kiafya leo, lakini nitajitahidi ili niweze kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa kama vijana wenzangu walikuwa hawajui, kama mnaona kuna maendeleo ya fedha kufika kwa wakati katika Bodi ya Mikopo, basi wajue ni jitihada za Mheshimiwa Mgimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona hili niliseme wazi kwa sababu tuna hulka ya kuongelea mabaya tu anayoyafanya mtu, lakini kuzungumzia kitu ambacho kilikuwa kero kwa muda mrefu, hilo tumekuwa hatusemi. Kwa hiyo, kwa dhamira ya dhati kabisa Mheshimiwa Mgimwa nakupongeza na nimepata taarifa hizo kutoka kwenye Bodi ya Mikopo na baadhi ya vijana ambao wanasoma Elimu ya Juu kwamba sasa hivi wengi wao wanapata fedha kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili limejidhihirisha bila kujali itikadi zetu pande zote mbili humu ndani wameona utendaji wako na sisi tunakuombea kwa Mungu kwa sababu ni mzalendo na una dhamira ya dhati ya kuhakikisha nchi yetu inakwenda. Lakini pia nikupongeze kwa baadhi ya mabadiliko ambayo umesikiliza vilio vya Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia tozo kwenye petroli na mafuta ya taa. Tunapozungumzia mfumuko wa bei kwa asilimia 50 unachangiwa na mafuta, pamoja na chakula. Kwa hiyo, unapoongeza tozo kwenye mafuta ujue kabisa gharama za usafirishaji mali zitapanda na gharama mbalimbali za malighafi kwenye viwanda nazo zitapanda. Hiyo yote inakuja kuonekana moja kwa moja katika suala zima la mfumuko wa bei na watu ambao wanaathirika ni walaji ambao ndiyo Watanzania wa kawaida ambao wanapata madhara ya ongezeko la tozo pamoja na madhara ya mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iangalie ni maeneo gani yanaweza kuongezwa tozo, kuliko kuongeza tozo katika maeneo yanayomgusa Mtanzania wa hali ya chini moja kwa moja. Ukizungumzia kupanda katika masuala ya usafirishaji, pia unakwenda kumwumiza mkulima ambaye atashindwa kusafirisha mazao yake, mwisho wa siku atalazimika kuuza kwa bei ya kutupa kwa sababu ameshindwa kuyasafirisha. Hilo na lenyewe naiomba Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi na nashukuru ina Waziri makini na wala hatujutii hilo, kwamba watalisikia na watalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kidogo ningependa nizungumzie suala zima la msamaha wa kodi. Nilikuwa nimejaribu kupitia ripoti ya *ESAB* ambayo inazungumzia masuala ya *transforming the informal sector* na uzuri hii ripoti imeandaliwa kwa kushirikiana na wataalam wa kiuchumi waliobobea akiwepo Profesa Malya Mkono.

Mheshimiwa Spika, ripoti hii ilikuwa inazungumzia dhana ya Serikali ya kupunguza msamaha wa kodi. Imeonesha kabisa ambavyo Serikali inapunguza misamaha ya kodi katika Makampuni ya Madini, Makampuni ya Utalii na maeneo mengine mbalimbali, ikiwepo na gesi na mafuta.

Mheshimiwa Spika, enzi hizo za miaka 90, lengo la kutoa msamaha wa kodi, bado miundombinu ya nchi yetu ilikuwa mibaya, lakini hata bandari zetu utendaji kazi wake haukuwa mzuri. Lakini hali hii sasa hivi ni tofauti. Leo hii ukizungumzia miundombinu, Serikali imejitahidi kuboresha miundombinu. Ukizungumzia utendaji wa bandari ni tofauti na miaka ya 90.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaona kuna haja ya Serikali kuangalia kwa kina ni maeneo gani ambayo wanapaswa kutoa msamaha wa kodi, maeneo ambayo yataleta matokeo mazuri moja kwa moja. Kwanza, kuisaidia Serikali kuiondolea mzigo na kuiongezea uchumi na kuondolea umaskini kwa wananchi wake, lakini pia hata kutatua tatizo la ajira. Tumeona ni jinsi gani haya makampuni hayajatoa mchango wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri, kuna maeneo ambayo Serikali inaweza ikatoa msamaha wa kodi na matokeo yake yakaonekana moja kwa moja. Kwa mfano, Sekta ya Kilimo, Sekta hii inachangia kwenye pato la Taifa asilimia 30. Pia Sekta ya Kilimo inachangia kwa fedha za kigeni asilimia 40. Vile vile sekta ya kilimo inachangia kutengeneza ajira, kuajiri zaidi ya asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia kitabu cha Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Hakioneshi moja kwa moja ni jinsi gani Serikali imedhamiria kuondoa msamaha wa kodi katika Sekta ya Kilimo. Umuhimu wa kuondoa msamaha wa kodi kwenye sekta ya kilimo tayari umeonesha. Ni sekta ambayo inatoa mchango kwanza kwa pato la Taifa, lakini pia inasaidia kukuza ajira.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia kukuza ajira; kwanza, kumwondolea maskini Mtanzania kwa sababu tayari atakuwa na uwezo wa kupata kipato chake. Pia kusaidia vijana wengi kuajiriwa kwenye sekta ya kilimo, lakini na kutoa fursa kwa wawekezaji wa ndani kuweza ku-*invest* katika Sekta ya Kilimo na kutengeneza ajira nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona ni vema Serikali ikajipanga kwa kina, ikafanya utafiti wa kutosha ni maeneo gani ambayo wanaweza kutoa msamaha wa kodi ambao kwanza utaipunguzia mzigo Serikali, lakini utakuza uchumi na vile vile utasaidia kutengeneza ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la tozo kwenye simu. Kila siku hapa nimekuwa nikisema kwamba, mabenki hayana urafiki na maskini.

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami hata wewe kule kwako Njombe una uwezo leo hii wa kutuma fedha kwa *M-Pesa* kwa ndugu zako walioko vijijini. Lakini leo hii inasaidia watu wa hali ya chini kuwa na mawasiliano, watu wengi vijijini hawawezi kwenda Benki. Kwanza hata hizo benki zenyewe hazina mtandao wa kutosha mpaka vijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa wengi wamekuwa wakizitumia hizi simu kwanza kuwa na urahisi wa kuwasiliana. Lakini kwa namna moja au nyingine ni kama njia moja ambayo wao ni kama benki, wanaweza wakatuma fedha au wakatumia fedha. Kwa hiyo, Serikali iangalie kwa makini ni jinsi gani wanaweza wakafanya marekebisho katika hii tozo ya *sim card*.

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa nasoma kwenye ukurasa wa tano wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema: "Kurekebisha kifungu cha 124(5)(a) ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye magari yasiyo ya uzalishaji yenye umri wa miaka 10 kutoka asilimia 20 hadi 25". Dhamira wanasema ni kutunza mazingira na kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, kiukweli kama ndiyo dhamira hiyo ya Serikali, ingeanza magari ambayo yapo sasa hivi. Tuna magari mengi sana ambayo yapo ya miaka 10 mpaka 20. Naona hapa dhamira ni ukusanyaji wa kodi. Lakini ukusanyaji wa hii kodi unakwenda kuwabana Watanzania ambao wengi wao ni wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, leo hii suala la usafiri siyo *luxury*, ni muhimu, lakini je, ni Watanzania wangapi ambao wanaweza kununua gari jipya. Naungana kabisa na mawazo ya Kamati, Kamati imesema kama tuna dhamira hii tungeweza kwanza kuwatengenezea mazingira Watanzania ya kuwa na uwezo wa kununua magari mapya. Lakini kama kweli tunasema dhamira ni kutunza mazingira na kuondoa ajali, tungeanza ku-*deal* na yaliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tungeanza ku-*deal* na yaliyopo kwa sababu yapo mengi na hata humu ndani tulio wengi hatuwezi kununua magari mapya, tusidanganyane. Hapa dhamira ni kukusanya kodi tu, lakini hii kodi inambana mtu ambaye amejinyima,

mfanyakazi wa kawaida, Mwalimu, Nesi kajikusanya anunue gari, hana uwezo wa kununua gari jipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni vyema Serikali ikaangalia kwa makini suala hili. Inawezekana ikawa na nia njema kabisa, lakini hii nia njema italeti madhara kwa kiasi gani kwa Mtanzania, kwa mfanyakazi ambaye tunajua wote mishahara yao ikoje. Hata sisi tu wenyewe humu ndani, Wabunge hatuna uwezo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Kama wewe mgonjwa umesema hivi, basi ungekuwa mzima tungekoma.

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mmekuja wengi, naomba nieleze yafuatayo:-

Naomba mnisikize kwa sababu ni muhimu kwetu sisi wote. Waheshimiwa Wabunge utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kushughulikia Muswada wa Sheria ya Fedha, *(Finance Bill)*, umewekwa na sehemu ya Tisa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013.

Kanuni mahususi iliyoweka utaratibu wa kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha, *(Finance Bill)* tumeshasema toka asubuhi ni ile ya 109. Halafu Fasili ya kwanza ya Kanuni hiyo inaeleza kwamba: "Muswada wa Sheria ya Fedha utajadiliwa na kupitishwa kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na sehemu ya nane ya Kanuni hii.

Sehemu ya nane ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti ya jumla ya kutunga sheria ambapo kwa mujibu wa Fasili ya tatu na Fasili ya nne ya Kanuni ya 84, inaelekeza kwamba:

"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 99 ya Katiba, Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekabisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri anayehusika na Muswada huo kufanya mabadiliko na kabla ya Muswada wa Sheria uliyofanyiwa mabadiliko, naomba nirudie hapo. Kabla ya Muswada

wa Sheria uliyofanyiwa mabadiliko haujawasilishwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili, utapelekwa kwenye Kamati inayohusika kwa madhumuni ya kuzingatia mabadiliko hayo”.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 109 Kanuni ndogo ya pili, inaelekeza kwamba: “Marekebisho au mabadiliko ya kupunguza kiwango cha kodi katika Ibara yoyote ya Muswada wa Sheria ya Fedha yatakayopendekezwa na Mbunge yoyote hayatakubaliwa iwapo hayatatoa mapendekezo mbadala yanayoziba pengo linalotokana na punguzo lililopendekezwa”. Hivi ndivyo inavyosema Kanuni ya 109.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sharti lililowekwa na Kanuni hiyo ni la lazima, ni *mandatory* na kwa kuwa kuna mapendekezo mengi ya mabadiliko yaliyowasilishwa na Wabunge pamoja na Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1), Spika ana wajibu wa kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni”.

Nimeelekeza kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha upelekwe kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 84(3) na (4) ili ifanyiwe kazi na Kamati ya Bajeti na Waziri wa Fedha kujiridhisha iwapo mapendekezo ya marekebisho yaliyowasilishwa na Wabunge yamekidhi matakwa na masharti ya Kanuni ya 109(2).

Aidha, imeelekeza kwamba, Wabunge wote waliowasilisha majedwali ya mapendekezo ya marekebisho kuhusu Muswada huu, kuhudhuria kikao hicho cha Kamati kwa ajili ya kutoa maelekezo ya ufafanuzi na marekebisho yanayopendekezwa.

Waheshimiwa Wabunge tumesema hivi kwa sababu gani, yapo marekebisho mengi tu yameletwa. Sasa sharti la kwamba, lazima utoe namna mbadala ya kurudishia siyo jambo dogo na siyo jambo rahisi. Kwa hiyo, ndiyo maana wote mliyoleta mapendekezo yenu ambayo yako kwa Katibu wa Bunge, naagiza Kamati ya Bajeti na Wataalam wa Wizara ya Fedha wakakae wjadiliane. Kesho kwa yule ambaye hakushiriki kule tutapata taarifa kutoka Kamati ya Bajeti. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawaombeni wale wote wenye marekebisho yao yaliyopelekwa huko kwa mujibu wa Kanuni, waende wakashirikiane na Kamati ya Bajeti ili waweze kuona ni namna gani inahusika. Kwa sababu hiyo basi, naomba Mheshimiwa John Cheyo azungumze kwa sababu ni Mjumbe wa Bajeti, ili waweze kwenda huko kujaribu kusikiliza tena. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kuungana na Waheshimiwa wote kusema kwamba, mchakato mpya ambao tumeuanza umeleta manufaa makubwa na nakupongeza sana kwa kuthubutu kuleta mchakato huu mpya.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nilipokuwa nagombea urais 1995 na 2000, watu walinicheka nilipokuwa nasema kwamba nia yangu ni kuwajaza Watanzania mapesa kibao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakasahau upande mwingine niliokuwa nazungumzia ili waweze kulipa kodi. Dhana hii ni ya maana sana, kwa sababu ninapoangalia hata Jedwali ambalo tumepewa na Mheshimiwa Waziri, la mapato, ukichukua takwimu kwa mfano za wafanyakazi wote wa nchi hii, ni takribani trilioni 1.3, pesa tunazopata kwa makampuni kama vile kodi ni takribani trilioni moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, trilioni karibu tisa ambao Mheshimiwa Waziri anaziomba, zinatokana na watu wa kawaida, hizo ndiyo *value added tax, excise duty*, vikorokoro mbalimbali na sasa tumefika mahali ambapo tunachaji na simu, tunachaji na mambo ya kupeleka pesa na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa wito kwamba, Serikali kila wakati ifikirie ile dhana yangu ya pili, ni jinsi gani tutawapa watu uwezo wa kuweza kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara nyingine nikiwa hapa Bungeni, watu wananitania, wananiambia huyu ni bwana pamba na nakubali kwa majivuno kwa sababu ukiongeza uwezo wa wakulima wa pamba kuweza kununua bia, kuweza kununua soda, kununua kanga ya wapenzi wao na vitu kama hivyo, ndiyo vinamwezesha Waziri wa Fedha kupata hela nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito mwaka huu tuongeze bei hiyo ifike 850 kwa kilo, badala ya 650 ili hawa watu wapate uwezo wa kununua bidhaa mbalimbali tupate kodi.

Mheshimiwa Spika, watu wananicheka ninapozungumzia juu ya ng'ombe, kwamba ng'ombe wapate masoko, mfugaji aweze apeleke ng'ombe wake na hela nyingi ikaongezeka. Nazungumzia juu ya uwezo wa watu kupata pesa ya kuweza kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, dhana nyingine kila watu hapa wanasimama, wanasema watu walio katika *informal sector*, watu ambao hawako katika mfumo wa kuajiriwa, hawalipi kodi, ni uongo. Ukweli ni kwamba bado watu ambao walio katika *informal sector* ndiyo wanaolipa ma-VAT yote ambayo tumeweka hapa. Hawa ndiyo wanalipa ushuru wa bidhaa ya vitu vyote ambavyo tunaweka hapa.

Mheshimiwa Spika, yale makampuni yenyewe yanakusanya tu, ni *collecting agency* wa Serikali. Kwa hiyo, ni muhimu sana, katika kila bajeti, afikiriwe mkulima na nasema afikiriwe mkulima kwa sababu ndiyo walio wengi. Ndiyo wale ambao wako kwenye *informal sector* zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania tunaozungumza hawa ndiyo walaji na kila mlaji ndiyo anampa Mheshimiwa Waziri pesa za kuweza kuchukua kwa ajili ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kuna nyingine ambayo inatembea hapa mara nyingi kwamba, mtu wa kawaida utampandishia maisha. Hakuna njia, ulimwenguni kote ni wananchi wa nchi hiyo ndiyo wanalipia Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Sweden watu wanachukua zaidi ya 75 ya mapato ya mtu ili waweze kuendesha miradi yao ya maendeleo na ndio maana nchi kama Sweden, nchi kama Finland ziko juu. Kwa hiyo, hiyo propaganda ya kusema, mimi ndiyo namhurumia sana mtu wa chini, tunajidanganya. Sisi tumesema, tumeona manufaa ya kuwa na barabara nzuri na barabara nzuri vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya miaka saba hatujapandisha *fuel levy* ili ikasaidie barabara. Baada ya miaka saba ni vyema ukaweka angalau sh. 63 ili uweze kujenga barabara nyingi zaidi na barabara hizo zielekezwe zaidi vijijini ili huyu mtu wa vijijini afanye biashara. Akifanya biashara ndiyo kusema kuna manunuzi, kuna ulaji, kuna minada mizuri na hivyo ndivyo anakuletea pesa. *(Makofi)*

Tumesema tuweke sh. 50 angalau ili tuweze kupeleka umeme vijijini, ukipeleka umeme vijijini umepeleka maendeleo. Wale vijana ambao wanalima alizeti wataweza kuwa na mashine ndogo ndogo, watakamua mafuta ya alizeti. Wakikamua mafuta ya alizeti hawa watapata pesa na wataongeza uwezo wao wa kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, angalizo hapa, kwa kuwa tumewakamua watu wa kawaida, watu ambao tunawaita ndiyo maskini, basi mtindo wa kupeleka pesa lazima tuugeze. Mambo ya kungojea hela ya maendeleo ya wananchi ipelekwe mwisho, tule kwanza, tupeane mishahara kwanza, halafu zinazobaki ndiyo zipelekwe kwenye maendeleo. Hii hatuwatendei haki watu wa kawaida ambao ndiyo wanatupa fedha ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bilioni 184 za maji ambazo tumetoa, bilioni 156 ambayo tumeongeza kwa *REA*, tunataka wakati wa *quarter* ya kwanza ya mwaka unaoanza tarehe 1 Julai, 2013, pesa hizo tukutane nazo kwenye vijiji vyetu. Hiyo itakuwa heshima ya kumwomba mtu aweke fedha kwenye au tuombe kodi au tozo kwa ajili ya simu na vitu vingine ambavyo tumeongeza hapa. Tusipofanya hivyo haturudishi fadhila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nakubaliana na wewe, kama inabidi tukope Benki Kuu ili *quarter* yetu ya kwanza iwe na pesa ya maendeleo tufanye hivyo, ili huyu tuliyemkamua aone kwamba, kumbe kuna sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi nataka popote walipo, wajivune kwamba wao ndiyo wanaendesha Serikali hii na wawe wakati wowote tayari kudai haki yao ya kupata maendeleo kutoka kwa Serikali yao kwa sababu wao ndiyo ambao wanalipa hizo fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia si sifa kujivuna kila siku kwamba, wewe unategemea nchi nyingine, sifa ni kwamba, mimi naendesha familia yangu kwa juhudi zangu. Sifa ni kwa Serikali, mimi Tanzania kwa fedha za wananchi wangu. Hatuwezi kuendelea milele na milele kutegemea fadhila ya wafadhili. Utaratibu huo kwanza hauwezekani, kwa sababu wafadhili wengi ukitaja nchi, sitaki kuzitaja hapa, wako hoi bin tabani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ukiona mfadhili wako yuko hoi bin taabani, ni vizuri wewe ukajizatiti ndani kuhakikisha unapata fedha ya kutosha kutoka vyanzo vyako vya ndani. Ndiyo maana Kamati ya Bajeti imetusukuma kuelekea huko na ndiyo maana Bunge limemsaidia Mheshimiwa Waziri kupata fedha za hapa.

Mheshimiwa Spika, tusidanganyike, najua baada ya bajeti hii Mheshimiwa Waziri atabanwa na wafadhili kwamba tulikubaliana bajeti yako isivuke kiwango cha trilioni 17.1 na yeye ameongeza ikawa trilioni 17.8 na juzi tumeidhinisha 18.24. Namwomba asikubali kugeuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Jitu V. Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, lakini kanuni inasema msirudie rudie.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Kwanza, nimpongeze Waziri, Manaiibu Mawaziri na timu nzima ambayo imeandaa bajeti hii, lakini zaidi ya yote Kamati ya Bajeti ambayo imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kuwa tunapata bajeti ambayo inaweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo machache ambayo ningependa kuchangia katika Muswada huu wa Fedha, hii *(Finance Bill)*. Kuna maeneo ambapo leo ni mwaka wa tatu, mwaka 2011/2012, tulipitisha sheria ya kufuta baadhi ya kodi kwa ajili ya wakulima hasa katika maeneo ya vipuri vya matrekta, matairi ya matrekta na tela za trekta.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi leo hii, pamoja na kufuta kule kote katika sheria na tumepitisha ndani ya Bunge hili Tukufu, lakini bado Serikali inaendelea kutoza kodi hizo. Ningeomba Mheshimiwa Waziri atuambie hizo fedha ni kiasi gani wamekusanya na zimetumika wapi kwa sababu, zilikuwa zimelenga kumunufaisha mkulima.

Mheshimiwa Spika, lakini hadi leo hii, bado zinaendelea kutozwa. Mzigo wote huu mwingine ambao kodi zinaongezeka iwe ni *petrol, diesel* na hizi nyingine zote, bado huyo huyo mkulima ndiyo anabeba. Mahali ambapo wanakwenda kupata unafuu kidogo, Serikali bado haikubali kumpa ule unafuu kidogo ambao tuliupitisha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambapo safari hii nimeomba iangaliwe, kwenye suala la vipodozi, wameweka *sunscreen*, yaani *lotion* zile ambazo zinatumika na wenzetu hawa wenye matatizo ya ngozi, yaani *albino*.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie madawa yote ambayo yanatengeneza *sunscreen* na *lotion* kwa ajili ya watu wenye matatizo ya ngozi, hiyo kodi ifutwe na wasichajiwe kodi aina yoyote pamoja na vifungashio vyao. Tuangalie kwa sababu, gharama kubwa tunatumia kwenye sherehe zao, lakini idadi ya kodi wanayotakiwa kulipa kwa ajili ya kutengeneza zile dawa ni ndogo. Kwa hiyo, sehemu hiyo Serikali iangalie na kesho wakati anakuja na majibu, aitamke wazi kwamba imefutwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napendekeza, mwaka jana tulipitisha kwenye sheria ya *gas*, kwamba *natural gas*, haihusishi hii *gas* nyingine aina ya *LPG*. Ningeomba katika sehemu hiyo Serikali iangalie vile vifaa ambavyo vinatumia kama *LPG, Gas regulator, cooker* na hivi vyombo ambavyo vinatumia *gas* ya kawaida, pia ipunguzwe ili uharibifu wa mazingira uendelee kupungua na wananchi wa vijijini waweze kununua *gas* za kawaida, ambazo kwa sehemu kubwa mmeshapunguza kwenye ile mitungi; lakini hata vile vyombo ambavyo vinakwenda kutumika basi vipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo Serikali inaweza kupata mapato makubwa sana, ni katika vinywaji kama *juice* na mvinyo. Leo hii Serikali imepandisha shilingi moja kwa mvinyo na *juice* ambazo zinatengenezwa nchini hapa kwa kutumia matunda ya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini asilimia kubwa ya juisi tunazokunywa leo zinatoka nje ya nchi na zinaletwa kwa mfumo wa *concentrate* au *powder*, zinakuja kuwekwa sukari na maji hapa na kuwekwa kwenye vifungashio tunauziwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza badala ya kuongeza shilingi kumi pale kwa kila lita, Serikali ingeongeza shilingi mia ili iweze kukuza soko la juisi ya matunda ya Tanzania. Leo hii hawanunui matunda kutoka kwa Watanzania isipokuwa wanaleta kutoka nje kwa sababu kodi ni ndogo wataendelea kuleta kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kwamba *i-charge* shilingi mia na haitaathiri mtu yoyote kwa sababu wenye kunywa ile juisi ikiongezeka shilingi mia mbili kwa lita ile pakiti moja ni watu wenye uwezo. Kwa hiyo, haitamuathiri mkulima wa kawaida na ile fedha itumike kwenda kufidia maeneo ambapo wanaweza kusaidia sekta ya kilimo au maeneo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia eneo linguine, Serikali ingealia namna ya kuangalia mfumo wa *property tax*, kodi ya majengo, ingepunguza ile kodi ili *compliance* iwe kubwa. Watakapopunguza watu wengi watakuwa wanalipa zaidi na itakuwa siyo mzigo kwa mtu yoyote. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, hiyo waiangalie upya na waweze kupunguza kodi ili watu waweze kulipa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu nyingine ambapo tunapongeza, mtakusanya fedha kwa wingi tusipoangalia Sheria ya Manunuzi. Sheria ya Manunuzi isipofanyiwa kazi, hata fedha yote tunayokusanya na haya matrilioni tunayokusanya, bado yataendelea kutumika vibaya na hiyo Sheria itafanya watu wengine wachache, wanufaike na watajirike kwa migongo ya hawa Watanzania ambao wanakwenda kulipishwa kwenye mafuta, wanakwenda kulipishwa kwenye kadi za simu na nini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Manunuzi iangaliwe upya ili tuweze kubana matumizi ili hizi fedha ziweze kwenda kwenye maendeleo. Watanzania wote naamini leo wamekata tamaa na hawataki kulipa kodi kwa sababu hawaoni manufaa ya ile kodi, kwa sababu inakwenda kunufaisha wachache. Lakini wakiona inakwenda kwenye maendeleo, wakiona barabara zinajengwa, umeme unapelekwa vijijini na huduma zinakwenda vijijini, naamini hata hizo kodi mnazoweka kila mwaka, hata mkipandisha kidogo kidogo wao hawatakuwa na shida, lakini mradi waone ile *trickledown effect*, yaani maendeleo yawe kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu nyingine ambapo naomba Serikali itoe ufafanuzi vizuri, wakati unapopandisha shilingi mbili kwa lita ya dizeli au unapopandisha ile bima hawa ma-*agent* na wale wafanyabiashara wanakwenda kuweka mara mbili au mara tatu, badala ya kupandisha ile asilimia tu iliyopandishwa na Serikali ambayo ni ndogo sana, wao wanakwenda kupandisha mara kumi au mara ishirini na lawama yote inabaki kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingeendelea kutoa ufafanuzi vizuri kwamba, bima imepanda kwenye sekta ipi na imepanda kwa asilimia ngapi, ili wakati wanapopandisha wao ijulikane kwamba haijapanda kwa wingi, imepanda kwa asilimia ndogo tu ili wananchi waweze kuelewa kwamba kodi hizi zote zinazotozwa, hazijapanda sana isipokuwa zimepanda kwa asilimia ndogo tu.

Mheshimiwa Spika, leo hii mzigo ule wa petroli ambapo wakulima wanastahili kulalamika sana, bei ya mafuta kupanda, lakini tunaipongeza Serikali kwa sababu mmetuaminisha kuwa hayo mafuta shilingi hamsini kwa kila lita itakwenda kwenye umeme vijijini ambayo itakwenda kusaidia wakulima vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunawapongeza kwa hilo, lakini mtuhakikishie kwamba hizo fedha zikipatikana hazitakwenda kwingine, zitakwenda huko ambapo zimelengwa, kama ni umeme vijijini, kama ni barabara vijijini au kwenye maji, yaani mtaendelea kupongezwa na wananchi wataendelea kuwachangia kwa sehemu kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niwapongeze pia kwa hili suala la hizi mashine za *electronic fiscal devices* kwamba, zitaendelea kuongeza wigo wa kodi, mtaendelea kukusanya kodi kwa wingi zaidi bila watu kukwepa.

Mheshimiwa Spika, lakini nina pendekezo, Serikali ingeangalia namna, badala ya kumpa mtu mmoja tenda ya kuleta hivyo vifaa, ingeruhusiwa mtu yoyote alete hivyo vifaa ili pawe na ushindani katika vifaa, ili gharama zile za *electronic fiscal devices* zipungue, mradi hivyo vifaa viwe na vigezo ambavyo vinahitajika na *TRA* yaani zile *specification*, kwa sababu sasa hivi ni karibu shilingi laki nane mpaka milioni moja na laki mbili. Lakini ukiruhusu soko huria, naamini vifaa hivyo vitakuwa vinaweza kufika hata kwa shilingi laki tatu au laki nne nah ii itapunguza mzigo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napendekeza Serikali iangalie, ni suala la dawa za mifugo. Leo hii dawa za mifugo zinazotolewa nje ya nchi hazina kodi yoyote lakini malighafi inayoletwa kwa ajili ya kutengeneza hizo hizo dawa ndani ya nchi inatozwa 10% *import duty* na 18% *VAT*. Kwa hiyo ina maana Serikali inataka watu watengeneze madawa nje ya nchi walete bila kodi na kuhakikisha viwanda vya nje vinakua, lakini humu ndani ya nchi viwanda visiendeleo kukua.

Mheshimiwa Spika, tunashauri kwamba, watu ambao wanaleta malighafi ya kutengeneza madawa ya mifugo wasitozwe kodi ili viwanda vya ndani ambavyo vipo waweze kushindana kibiashara na vile vya nje na madawa yatengenezwe hapa nchini. Hii itakuza ajira, lakini pia mtakuja kupata kodi kwa kupitia sehemu nyingine kutokana na biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napenda kuchangia ni kwenye masuala ya magari. Haya ambayo mnataka ku-charge 5% kwa magari ambayo ni ya zaidi ya miaka kumi. Ningeomba Serikali iangalie upya kwa sababu uwezo wa Watanzania kununua magari mapya bado ni mdogo hata taasisi zetu za fedha hazikopeshi kama nchi nyingine. Ukiangalia leo tuna magari ambayo yana miaka 20 mpaka 30 hasa ukiangalia katika sekta ya kilimo, vifaa vinavyotumika kule na magari yana miaka zaidi ya mimi nilipozaliwa na bado yapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwamba, kama ni masuala ya mazingira na nini tungeendelea kuboresha kwanza huku mahali ambapo mazingira yanaharibiwa, ukataji wa miti na nini na kutumia vifaa vingine ambavyo tutaboresha mazingira kuliko kufikiria kodi hiyo ya ushuru.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa wale Wajumbe ya Kamati ya Bajeti, naomba wote mwende huko na wale wenye hoja zao waende huko. Kwa hiyo namwita Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

MHE. CHRISTOPHER OLE SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa fedha wa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mgimwa kwa usikivu wake kwa niaba ya Serikali aliouonesha katika hoja zilizokuwa zimetolewa na Wabunge wakati tulipokuwa tukichangia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu zilikuwepo hoja zilizokuwa zinahusu tasnia ya utalii ambayo kwa kiasi kikubwa ameweza kuzingatia na kuondoa ushuru ule uliokuwa umeelekezwa katika baadhi ya maeneo, japokuwa amebakiza tu sehemu ndogo ile ya kodi ya zuio kwa upande wa ukodishaji wa ndege.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nitakuwa nilimsikia vizuri, nilisikia kwamba, kwa ndege zile za kibiashara zinazobeba abiria, zinazofanya biashara, hiyo kodi ya zuio imeondolewa. Kama nitakuwa nimempata vizuri, nina kila sababu tena ya kumshukuru, lakini kama siyo hivyo namwomba sana ajaribu kutupia jicho suala hili ili nalo liweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu Shirika letu la Ndege mnajua hali yake ilivyo, lakini hata lile la Watanzania wenzetu la *Precision Air* hali yake si shwari sana. Kwa hiyo, tukiendelea

kuwawekea tena kodi ya zuiro maana yake ina athari kubwa sana katika masuala haya ya sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kueleza bayana suala hili la *LABSA*, mmoja wa Wabunge wenzetu kutoka Chama cha Wananchi (*CUF*) amelielezea vizuri jambo hili na nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakuna duniani mtu anayeweza kuamka tu na hasa kwa nchi zetu hizi maskini, ukiona mfanyabiashara anaamka anafanya *lobbying* anasema tutozeni kodi na kodi yenyewe anayoiomba atozwe ni ya bidhaa ambayo yeye mwenyewe ana kiwanda cha kuzalisha na anatakiwa awauzie wafanyabiashara wengine wanaotengeneza sabuni kama yeye mwenyewe, lazima ujiulize maswali, kuna nini hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanaozalisha *LABSA* hapa nchini ni viwanda viwili. Kiwanda kimoja tulipokuwa tunamuuliza Waziri mwenye dhamana alisema hana takwimu zake sahihi, lakini kiwanda cha pili alieleza takwimu zake na akaeleza kwamba miongoni mwa wamiliki au wamiliki wa kampuni hiyo inayozalisha *LABSA* hapa nchini, ndiyo waagizaji wakubwa tena wa *LABSA* katika mwaka uliopita wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ukiwauliza wao wenyewe wengine wanasema walikuwa na ziada. Sasa unajiuliza kama mlikuwa na ziada ambayo nyinyi wenyewe mnaitumia kwenye viwanda vyenu vya sabuni, mnaagizaje tena nyingine na hiyo mnapeleka kwa nani.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo ambalo ni vizuri mlijue ni kwamba *LABSA* hii inatumika kuzalisha sabuni na viko viwanda vingine vya sabuni vya Watanzania wazalendo maskini na wadogo na viwanda vingine vya *SIDO* ambavyo vinatumia *LABSA* hiyo hiyo na wengine wakubwa wanasema wekeni kodi, lakini naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kusema hapana iendelee kubaki *zero* ili kuwasaidia Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, katika hili naungana mkono na yeyote ambaye ameleta hoja ya kuleta mabadiliko ya kuunga mkono Serikali kwenye jambo hili, lakini nitampinga yoyote kwa gharama

yoyote atakayetaka kumlinda mkubwa huyo kwa gharama ya kutelekeza maslahi ya wanyonge walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kuna mahali tumeua viwanda vya hapa nchini, dhambi kubwa tuliyoifanya katika mikataba ya ubinafsishaji wa viwanda vilivyoanzishwa na Mwalimu, masharti yale ambayo tulitiliana na wale, ambayo viwanda vile leo vimegeuka kuwa godauni badala ya kuwa viwanda vya kuzalisha vile ambavyo vilikusudiwa, kwanza ni mikataba ni mibovu tuliyoingia nayo au pengine hofu ya Serikali kuwachukulia wakubwa hao hatua kwa sababu baadhi yao ni wakubwa pia na wana nafasi katika ushawishi mkubwa wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu alisema Serikali *corrupt* haiwezi kukusanya kodi, lakini Serikali pia ambayo ina ubia na wafanyabiashara wakubwa na hasa wale wenye dhamana haiwezi kuwabana kwa sababu na wenyewe wanafika huko saa za jioni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, baadhi ya viwanda vyetu leo vimegeuzwa kuwa magodauni, lakini tunashuhudia na hatuchukui hatua wala hatuvunji mikataba nao. Naomba sana tuangalie viwanda vyetu vimefikia wapi pamoja na mikataba mibovu, lakini wachache walionunua viwanda hivi wamewamaliza wale wengine wadogo na hawawezi kuamka. Mkakati mwingine ambao upo ni huu wa *LABSA* na mtakakapokuja kuchunguza na kujua siri yake, hakika mtaunga mkono Serikali katika kuhakikisha kwamba *LABSA* inakuwa ni *zero*.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Kigoda kwenye Kamati moja alitolea maelezo vizuri na nampongeza sana Waziri Mgimwa kwenye hili. Naliomba Bunge lielewe maana ya hoja hii na tusiende tukafikiri kwamba kwa kuondoa kodi ile kwamba mnawasaidia wadogo, hapana. Mnawasaidia wakubwa waliokwishajijenga ambao wao wenyewe wanazalisha *LABSA*, lakini hawataki kuwauzia wale wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine ambalo ni muhimu sana tuliangalie, Serikali yetu ina mapenzi makubwa sana na Watanzania na mara nyingi tumekuwa tukitoa misamaha ya kodi katika uingizaji

wa mchele na sukari. Nataka niwaambie kama kuna kichaka kinachotumika leo katika kuiibia Serikali hii ni uingizaji wa sukari na mchele nchini kwa kivuli cha kumsaidia mnyonge, ndiyo maana leo sukari inayoingizwa nchini ambayo haijalipiwa kodi, inauzwa kwa bei ile ile ya soko wala hakuna auheni unayoiona tofauti na sukari inayolipiwa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, hili linahitaji kuchunguzwa kwa kiwango kikubwa na wote tuungane bila kujali itikadi za vyama vyetu, kichaka hiki tukivumbue zaidi. Lakini dhambi nyingine kubwa ambayo ipo kwenye sekta ya viwanda nchini, ni pale ambapo tunatoa msamaha na ahueni ya kodi kwenye uingizaji wa mafuta ghafi na *material* nyingine ghafi ambazo hazijakamilika, lakini badala yake watu wanaingiza mali ambayo imekwishakamilika na kazi yao ni kuja ku-*pack* tu hapa nchini na kuuza na kutengeneza faida kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu sana, kama tutaendelea kutokuwa makini sana kwenye mambo haya, inahitaji umadhubuti wa Serikali katika kuhakikisha kwamba watu wanaokwepa kodi wanashughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ni vizuri tukaangalia na vibali hivi tunavyovitoa. Sasa hivi kuna mkakati wa kuwapa wakubwa wachache. Ukienda kwenye sukari, baadhi ya watu wanaopewa vibali hivi vya sukari ndiyo hao hao ambao ni wabia katika viwanda vya sukari.

Mheshimiwa Spika, sasa hebu angalia, wewe ndiyo una Kiwanda cha Sukari, wewe unapewa kibali cha kuingiza sukari bila kulipa kodi na wewe ni mfanyabiashara unayetaka faida kubwa. Utakachofanya ni kuhakikisha kwamba kama uingizaji wa sukari bila kulipa kodi au kodi ya auheni ndiyo inayokuingizia faida huko ndiko utakakoweka nguvu zaidi na kwa maana hiyo unakuta viwanda vingine vya ndani vitadorora na unaweza kukuta miwa ya Watanzania isinunuliwe kwa sababu hao hao wanaohusika ndiyo wanaoweza kudhibiti soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukikubali *monopoly* ya aina hii ni mbaya na hii haijalishi kama inafanywa na Wabunge, haijalishi kama

inafanywa Mawaziri wa Serikali hii kama wana hisa, haijalishi kama inafanywa na wanachama wa Chama cha Mapinduzi au wanachama wa chama chochote cha siasa, naomba wote tuungane kwenye hili na ikibidi Waheshimiwa Wabunge tujenge hoja ya kuunda Kamati Teule ya kuchunguza ufiadini uliopo katika uingizaji wa rasilimali hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakapochunguza, nawahakikishieni wengine humu watakosa mahali pa kuficha nyuso zao, maana ni wabia katika utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hili kwa sababu kuna suala lingine ambalo ningependa sana kulizungumzia nalo ni hili la 10% ambalo ilikuwa pia inahusisha baadhi ya taasisi za umma ikiwemo *TANAPA*. Tena niwaambieni kwa upande wa *TANAPA*, Hifadhi za Taifa ambazo zina faida na ambazo zinafanya *TANAPA* iweze kufanya kazi ni chache sana Kilimanjaro *National Park*, Serengeti *National Park*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla na Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Magdalena Sakaya!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nitachangia vipengele vichache sana. Nitachangia kipengele cha tatu cha Muswada ambacho kinataka mamlaka zote za Serikali kuweza kulipa 10% ya pato ghafi kwenda kwenye Mfuko wa Taifa na moja kwa moja nitakwenda kwenye kipengele cha nane na cha tisa, ambapo kipengele cha nane kinaitaka Mamlaka ya *National Park* kuweza kulipa 10% kwenye pato la Taifa na pia kipengele cha tisa cha Mamlaka ya Ngorongoro ambayo inatakiwa pia na yenyewe iweze kulipa 10% kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwenye mashirika haya mawili, Mamlaka ya Ngorongoro na Mamlaka ya *TANAPA* kwa maana ya Tanzania *National Park*, lengo lake la kwanza ni mashirika ya uhifadhi. Kwa hiyo, tunapoweka pato lolote au tunapoweka kodi yoyote tuhakikishe kwamba, yasitoke kwenye lengo mahususi ambalo ni la uhifadhi kwa sababu faida ni baadaye lakini lengo la kwanza ni uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye Shirika la *TANAPA* lenyewe. *TANAPA* kama alivyosema Mheshimiwa Sendeka ni Shirika ambalo linahudumia *National Park* 16 hapa nchini na kati ya hizo 16 ni mbili tu Serengeti *National Park* na Kilimanjaro *National Park* ndiyo zinaweza kujizalisha na kuweza kujihudumia na *excess* ambazo zinazalisha kwa 76%, zilizobaki ambazo ni Manyara *National Park* na nyingine tatu zinazalisha kwa kuweza kujiendesha zenyewe, lakini hazina *excess*. Zilizobaki zote ambazo ni za Kusini na Magharibi zinategemea kule Kaskazini kwa ajili ya kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunasema miaka yote kwamba, utalii Tanzania ume-*base* Kaskazini, tukaiomba Serikali kwa kupitia haya Mashirika ya Uhifadhi ihakikishe kwamba inaboresha Hifadhi za Kusini na Magharibi ili utalii uwe ni wa nchi nzima na *usi-base* Kaskazini tu. Tumekuwa tunaishauri sana Serikali kwamba, tunazo *National Park* nzuri kama Ruaha *National Park*, Kitulo na nyingine nyingi tu kama Udzungwa zinashindwa kuzalisha kwa sababu miundombinu siyo mizuri, hakuna *accommodation* ya kutosha na mambo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vivutio viko pale, lakini watalii wanashindwa kwenda kwa sababu hawajaboresha zile *National Park* za Kusini. Kwa hiyo, matokeo yake zipo pale, lakini zinategemea zilishwe na *National Park* za Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, *TANAPA* mpaka sasa hivi wanalipa bilioni 4.2 kwa taasisi mbalimbali za Serikali kuendesha kama Chuo cha Wanyamapori cha Mweka, Chuo cha Pasiansi wanalipa na chenyewe kwa ajili ya uendeshaji, wanatoa pia 3% kwenda kwenye *Tourism Development Levy*, wanalipa pia kodi stahiki kwa Serikali shilingi bilioni nne mpaka bilioni tatu kwa mwaka kwa ajili ya pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yote haya *TANAPA* inalipa bila matatizo. Kitendo cha kuweka tena 10% kwenye pato ghafi, ukweli *TANAPA* haitaweza kuendeleza *Park* zao nyingine. Yale tunayojadili siku zote hapa Bungeni kwamba, *park* za Kusini ziendelezwe hawataweza na hapa hapa tujue kwamba, *TANAPA* tumeipa jukumu, kila ambapo Serikali inashindwa kuendesha Hifadhi yoyote, kimbilio ni kwa *TANAPA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuchukue mfano lhefu, wakati mifugo imeondolewa lhefu, kuweza kurudisha ile hali katika hali ya kawaida, kuweza kuhamisha watu, kulipa mpaka watu waliohamishwa, *TANAPA* ilipewa jukumu lile na maeneo mengine ambayo *TANAPA* ilikuwa inafanya kazi hiyo. Tunatambua kazi nzuri ambayo inafanywa na *TANAPA*, lakini tusiipe mzigo mkubwa kiasi kwamba, ikatoka kwenye lengo la uhifadhi, ikabaki ni kuichangia Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, *TANAPA* tumeipa jukumu la kuhakikisha kwamba, ujangili unapungua. Sasa hivi tunaona Waheshimiwa Wabunge kwamba, ujangili umezidi Tanzania kwa sababu, majangili wamekuja na mbinu mpya za kisasa. Leo tembo wanauawa kama kazi, kila siku, inabidi *TANAPA* wabuni mbinu mpya. Tumeingiza vifaru kutoka nje, *TANAPA* ndiyo tumewapa majukumu ya kuweza kuhifadhi na kuhakikisha katika hifadhi zetu kunakaa salama.

Mheshimiwa Spika, jukumu la *TANAPA* ni kubwa. Ningeiomba Serikali, kwa kuwa inaipa stahiki zote kama nilivyotangulia kusema mwanzo, isingize tena tozo nyingine ya asilimia kumi ya pato ghafi. *TANAPA* inategemea Utalii, asilimia kumi ya pato lake ghafi wanaweka kwa ajili ya akiba.

Mheshimiwa Spika, leo ikitokea *crisis* yoyote nje ya nchi na tunajua Tanzania tunategemea sana utalii wa nje. Bado hatujaweza kuimarisha *local tourism*, kwani bado iko chini sana. Tunategemea sana wageni watoke nje, waje kwa ajili ya kutembelea hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, leo tuchukue mfano, ikitokea *crisis* nje ya nchi kama ilivyotokea kushuka kwa uchumi wa nchi za nje, watalii wakapungua. Fikiria sasa *TANAPA* hakuna akiba hata shilingi moja.

TANAPA ita-collapse, kutakuwa hakuna uhifadhi, kwa sababu watakuwa wanakusanya, wanatumia, hakuna akiba hata kidogo, ni hatari sana kwa lengo zima la uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, tunataka Hifadhi zetu ziendeleo kuwepo, vivutio vyetu viendeleo kuwepo, tunataka watalii waendeleo kuja na Taifa letu liendeleo kusifika, kwa ajili ya kazi nzuri tunayoifanya ya Utalii. Kwa hili ambalo limewekwa sasa, kwenye kurekebisha Sheria ya *TANAPA*, tutauwa Shirika la *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, nikiwa hapo hapo, miaka mingi tumekuwa tunapiga kelele ndani ya Bunge hili, ndani ya *TANAPA* kuna hoteli za kitalii, zimejengwa kule na zinapata fedha nyingi sana kutoka kwa wageni wanaokuja kule. Tumekuwa tunaiomba Serikali, ipandishe angalau *concession fees* ili *TANAPA* ipate fedha za kujenga miundombinu. Ni jambo la ajabu mpaka leo ninavyoongea katika hoteli, wamiliki bado wanalipa fedha ya miaka kumi iliyopita huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, miaka kumi iliyopita, walikuwa wanalipa *concession fee* asilimia tatu mpaka tano. Wakati huo walikuwa wanalipa kitanda dola 50 mpaka dola 100. Leo hii wanalipa kitanda dola 500 mpaka dola 1000, bado wanalipa *concession fee* dola tano mpaka dola 10, haiwezekani! Sisi tunashindwa kuelewa, hawa wamiliki wa Hoteli zilizo ndani ya *National Park*, wanapata mgongo wa nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mtu apate dola 500 atoe *concession fee* ya dola tano, hii ni kuinyonya Serikali. Hapo hapo *TANAPA* ndiyo inahusika kuhakikisha kwamba, miundombinu ni mizuri na mandhari ya hifadhi ni nzuri ili watalii waweze kuja kulala kwenye hoteli zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Serikali, kwanza Mheshimiwa Waziri aanze leo, kuhakikisha anaongeza *concession fees* kwenye hoteli za Kitalii zilizoko ndani ya *National Park*. Serikali ipate hela za kutosha, *TANAPA* ipate hela za kutosha ili kuboresha miundombinu na hapo hapo *TANAPA* iweze kuendelea kufanya kazi zake vizuri kwa ajili ya kuhifadhi rasilimali za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa nguvu zote, kutukuongeza kodi ya *petroli*. Wakati wa kujadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri, hakuna Mbunge ambaye alisimama hapa akaacha kuzungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, nategemea kabisa Mheshimiwa Waziri amesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge, ambacho ni kilio cha Watanzania wote kwa ujumla. Naomba Mheshimiwa Waziri tena aliangalie hili, Kamati ya Bajeti imezungumza vizuri na kwa upana na *alternative income* zimetajwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aangilie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niungane na Waheshimiwa Wabunge waliochangia suala la kuongeza kodi kwenye magari ambayo yanatoka nje yakiwa na umri zaidi ya miaka kumi. Tunafahamu hali ya Watanzania, tunafahamu kwa Watanzania kwa sasa hivi, gari siyo anasa, gari ni kitendea kazi, kama vitendea kazi vingine. Leo tunataka, mtu akijikusanya akichukua mkopo, asiweze kuagiza gari.

Mheshimiwa Spika, turudi ndani ya nchi. kama suala ni ajali, mbona kuna magari yanayotoa moshi barabara nzima, yanatembea barabarani. Mengine yana kutu, ukiingia mpaka unaogopa lakini bado yanatembea barabarani. Mengine yanatumia *engine* za malori na yapo barabarani. Kwanza tuanze na ndani, magari yote ambayo yamechakaa, yasiyoweza kubeba abiria, yanayohatarisha maisha ya abiria, kwanza yaondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiamua kwenda nje kuzuia magari kuingia, hatujatoa tatizo la kupunguza ajali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kama Kamati ilivyoshauri kwamba, kwanza wapunguze kodi kuingiza magari mapya, ili Mtanzania anayetaka kununua gari, aweze kumudu kununua gari na tusije tukafanya kwamba, kila kitu kikawa ni anasa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimalizie kuendelea kuungana na Wabunge kwenye suala la kutoweka kodi kwenye malighafi ya sabuni. Tulinde viwanda vyetu vya ndani. Nchi zote zina mikakati madhubuti ya kulinda viwanda vyao. Nchi yetu wafanyabiashara wanaitumia kujinufaisha. Wakishaona kuna mwanya tu, wanaingilia

pale pale, watafanya *lobbying* kwa Wabunge na Mawaziri ili kwamba waendeleo kuwa pale. Tunaomba viwanda vyetu vilindwe. Kodi kama Mheshimiwa Waziri ameacha ibaki hivyo hivyo, Watanzania tunufaike na nchi hii iendeleo kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, *alternative* kwa mapato, kwenye masuala ambayo tumeyazungumza, tumeshasema kwenye *deep sea*, samaki wako pale wa kumwaga, wanavuliwa kama shamba la bibi. Serikali imetoa shilingi bilioni 20 kwenye Sekta ya Mifugo na Uvuvi, tunaiomba ile pesa iliyotolewa kule, ikaboreshe ulinzi wa samaki na kuwepo kitengo maalum kuanzia tarehe moja mwezi wa saba, kila samaki anayevuliwa, wahakikishe wanajua thamani yake, pesa ilipwe, pato liingie kwenye Serikali na maeneo mengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Dkt. Hamis Kigwangalla, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze tu kwa kusema kwamba, asiyeshukuru kafiri. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri waliyofanya ya *consultation* ili kufikia mapendekezo haya ya bajeti mpaka hapa tulipofika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nimpongeze zaidi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kusikia kilio cha Wabunge waliochangia kwenye hotuba yake ya bajeti, kwamba, tusipandishe bei za *fuel* na mimi ni mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, ninavyoona leo hii ameweza kushusha bei ya *diesel actually*, kodi ya bei ya *diesel* kutoka sh. 530 mpaka sh. 490, hili ni punguzo la karibu sh. 40. Vile vile niwapongeze kwa kuamua kuacha kodi ya *petrol*, pale pale kwenye kiwango cha sh. 713; ila bado kilio chetu kitabaki kuwepo kwenye ongezeko la kodi ambayo inatozwa kwenye mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wataendelea kulalamikia hili kwa sababu mafuta ya taa yanatengeneza nishati, ambayo inatumiwa na watu wengi wenye kipato cha chini huko vijijini na kwenye miji yetu. Sasa kuongeza kodi ya mafuta ya taa kutoka 400 mpaka 475, ni ongezeko kubwa na naamini litaleta ugumu katika maisha ya kila siku ya Watanzania walio na kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, naomba, kuliko kushusha sana kiwango cha *diesel*, kwa hii 530 kwenda mpaka 490, pengine badala ya kushusha kwa sh. 40, tushushe kwa kiwango cha sh. 20 tu. Ili tuweze ku-*retain* ile kodi ya zamani ya mafuta ya taa, kwa kuwa *diesel* inanunuliwa zaidi kuliko mafuta ya taa. Tukifanya hivyo, tutaweza kukaba lile shimo ambalo linaweza likaaachwa kwa kuamua kulinda bei ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, nafahamu nia inaweza ikawa nzuri, kwamba tunataka kuzuia uchakachujaji, lakini hatuwezi kuzuia uchakachujaji kwa kupandisha gharama ya maisha ya watu wa chini, hatuwezi kufanya hivyo. Hii ni Serikali na inaweza ikawa na mbinu nyingi za kudhibiti watu wanaofanya uharamia wa uchakachujaji kwenye vituo vyao vya mafuta, ili waweze kupata *profit* kubwa zaidi, lakini hatuwezi kusababisha ugumu wa maisha kwa watu wa chini ili kuzuia uchakachujaji. Hii ni Serikali na kuna mbinu nyingi za kuweza kufanya udhibiti wa wahuni wa aina hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, naomba sasa niungane na mchangiaji aliyenitangulia, kwa kuchangia kwenye Muswada kwamba, ile sehemu ya nane, tisa, kumi na kumi na moja, ambayo inalenga kufanya mabadiliko, kwenye sheria ya *National Parks*, Sheria ya Ngorongoro *Conservation area*, Sheria ya Bandari na Sheria ya *Public Finance*.

Mheshimiwa Spika, naomba ile 10% ambayo inalenga kwenda kupunguza kuongeza kodi kwenye mashirika haya, basi isifanyike, kwa sababu kwa kufanya hivyo, tutapandisha hususan lile eneo la *National Parks* kule TANAPA pamoja na Ngorongoro, kwa sababu tutakapoongeza tu, maana yake bei za utalii zita-*shoot*.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunapozungumza hapa, watu wa Kenya wana-*take advantage* ya soko la utalii. Kwa kuwa wao bei zao za Utalii, kwa mfano, kwa Mtalii ambaye atafanya utalii kwa siku saba, *rate* zao kwa Kenya zitakuwa ni dola za Marekani kati ya 4,000 na 5,000, lakini kwa Tanzania, siku saba hizo hizo akija Tanzania mtalii huyo, atatakiwa kulipa kiwango cha kati ya Dola 7,000 mpaka dola 8,000, jambo ambalo linasababisha Watalii wengi zaidi wafanye Kenya kuwa ndiyo *destination* yao kuliko Tanzania. Hali ya kuwa vivutio vingi zaidi vya Utalii viko Tanzania na haviko Kenya.

Mheshimiwa Spika, naomba tuzuie ongezeko hili la asilimia kumi, kwa kufanya mabadiliko kwenye *section* ambazo nimezisema za sheria hizi angalau, haya mashirika mengine, wakala na taasisi nyingine za Serikali zichajiwe asilimia kumi. Kwa sababu, mengi katika hayo mashirika hayafanyi biashara, *they are not trading organizations*, ni mashirika yanayotoa huduma, lakini yanapata kipato na kwa maana hiyo, hayo hayawezi yakachajiwa.

Mheshimiwa Spika, tayari *TANAPA* na *Ngorongoro Conservation Authority* wao wanafanya biashara, lakini pia wanalipa kodi, na wakati mwingine ni kwamba, wanaleta kipato Serikalini kwa njia ya kodi. Mbali ya kazi hiyo tu ya kuleta kipato, pia hawa *TANAPA* pamoja na Ngorongoro wao wanakuza Utalii, ambapo ukiangalia zile *industries* tano ambazo zimeshikilia uchumi wetu, utalii ni mojawapo.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tutaongeza hii asilimia kumi kwenye *gross revenue* ya *TANAPA* na ya Ngorongoro, tafsiri yake ni kwamba, tutakuza gharama kwenye bei za Utalii. Kutoka hii 7,000 hadi 8,000 ya sasa kwenda mpaka 10,000 hadi 12,000. Kwa sababu ukiangalia mabadiliko ambayo yanapendekezwa na Serikali, yanaongelea kuondoa *VAT exemption*, kuondoa msamaha wa *VAT*, kwenye mashirika, kwa mfano *TANAPA* na Ngorongoro, maana yake ni kwamba, watatakiwa waanze kulipa sasa, *VAT* ambayo ni 18%.

Mheshimiwa Spika, sasa 18% ya *rate* wanayo-charge leo hii, itaongeza zaidi dola nyingine 2,000 tukichukulia ile kesi niliyosema ya Mtalii ambaye atakuja Tanzania na kukaa kwa siku saba. Sasa tafsiri yake ni nini? Bei ya utalii Tanzania zitapanda mpaka kufikia, hiyo

niliyoisema ya dola 10,000 mpaka dola 11,000. Itakuwa mara mbili zaidi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, tafsi yake ni kwamba, wale maarifu wote wa Arusha pale wanaobeba mizigo, wanaoshughulika na utalii, wanaotembeza Watalii, wanaowafundisha lugha watalii, walio na hoteli za Utalii kule Arusha, Mwanza pamoja na Mara maana yake ni kwamba, watapata wateja wachache sana, lakini pia ajira zao zitakuwa matatani.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama hii ni sahihi sana, tayari kule Arusha kuna matatizo ya usalama ambayo yanatishia kuuu biashara ya utalii. Naomba tusifanye mabadiliko haya makubwa ili tuweze kuokoa sekta hii nyeti katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika hili nina mapendekezo kwenye jedwali la mabadiliko ambayo nitayafanya ili kuongeza kodi.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze sasa hivi katika kuchangia jambo moja, kwamba, kuna mapato ambayo tunawadai mashirika makubwa, kwa mfano *Pan African Energy*. Tunawadai hawa zaidi ya shilingi bilioni 100 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *Pan African Energy* nililileta mimi wenyewe, kufuatia *e-mail* niliyoipokea kutoka kwa rafiki yangu anayefanya kazi *action aid* kule Sweden mwaka 2011. Ilipelekea wewe mwenyewe kuunda Kamati Teule ya Bunge ambayo ilichunguza suala hili na kubaini kwamba, zaidi ya dola 30 milioni, hawa mabwana wamekiri kwamba walizikopesha kwa aidha, kuleta mzigo mkubwa wa gharama za uzalishaji ambazo walizifanya kule Ghana na sehemu nyingine hapa Afrika, kuziingiza Tanzania kama ni gharama ambazo wamezitumia kuwekeza hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kwamba, walipohojiwa na Kamati, walikiri na wakasema kwamba, pesa ile watailipa lakini watailipa *at their own comfort*. Nchi hii sasa tuache ku-*negotiate* na wezi. Hatuwezi kupatana na wezi, kwamba watatulipa vile wanavyotaka wakati wameshatuibia na waliiba wakiwa na akili timamu, wakielewa walichokuwa wanakifanya ni wizi. Mbali na kwamba tungetakiwa kuwapeleke Mahakamani watu

hawa kwa kosa hili kubwa la wizi, pia, tungeweza hata kuwanyang'anya mikataba yote ambayo tunayo kwa kosa ambalo walilifanya la kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, pia, Kampuni hii ya *Pan African Energy*, inafanya biashara ambayo ni rahisi mno na inafaidika sana mpaka mtu unajiuliza ni kwa nini watu kama hawa wanaweza wakathubutu angalau kukwepa kodi au kukwepesha mapato ambayo wanayapata kihalali na kwa njia rahisi mno katika nchi yetu. Ni watu wasio na huruma na hawapaswi kwa namna yoyote ile kuhurumiwa.

Mheshimiwa Spika, mara nyingine huwa nataka kujjuliza, hivi ni kwa nini watu hawa mpaka leo hii, hawajalipa dola milioni 30 ambazo ziliripotwa hapa Bungeni na ripoti ya Kamati yako mwenyewe. Huu ni Mhimili wa Bunge, ni mhimili mzito katika dola, lakini leo hii maazimio yalipita hapa na watu wale mpaka leo hii hawajawahi kulipa hizo pesa, tunahangaika kutafuta vikodi huku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Naomba nimwite Mheshimiwa Tundu A. Lissu na Mheshimwia Dkt. Kafumu, Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Jafo pia wajiandae.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika. Siku kama ya leo, naomba ninukuu kauli moja ilizungumzwa na mmoja wa watoto maarufu sana wa bara letu la Afrika miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, baadaye nitanukuu maneno ya mtoto mwingine wa bara hili aliyoyazungumza miaka 60 iliyopita, tarehe 21 Septemba, 1953. Maneno ya watoto hawa wawili wa Bara la Afrika ni muhimu sana katika mazingira tuliyonayo leo na katika mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1993, Mwalimu Nyerere katika moja ya mikutano yake na waandishi wa habari, alizungumzia matatizo makubwa ya kiutawala, yaliyokuwa yanaikabili nchi yetu wakati

anazungumza. Katika mazungumzo yake Mwalimu Nyerere alisema, Serikali ya wala rushwa haiwezi ikakusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha ulioko mbele yetu leo na mapendekezo ya kutoza kodi mbalimbali ambayo yapo katika Muswada huo ni ushahidi wa maneno ya Mwalimu Nyerere kwamba, Serikali ya wala rushwa haiwezi ikakusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina kitabu hapa, hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini mbele ya Bunge lako Tukufu, wiki chache zilizopita na naomba niseme na nioneshe takwimu za jinsi gani Serikali haikusanyi kodi.

Mheshimiwa Spika, katika hiki kitabu, ukiangalia nyuma kwenye takwimu za Wizara ya Madini na Nishati zinaonesha yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kati ya mwaka 1999 hadi 2004, Makampuni yanayochimba Madini Tanzania, yalilipa shilingi sifuri kama kodi ya mapato. Katika kipindi hicho hicho, kodi za wafanyakazi, *Pay As You Earn* na *Skills Development Levy (SDL)* za wafanyakazi walioajiriwa kwenye Makampuni hayo, zilikuwa shilingi bilioni 51.82.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho hicho (1999 - 2012) Makampuni yanayochimba madini nchi hii, yalilipa kodi ya mapato ya shilingi bilioni 467.98, katika kipindi hicho hicho, kodi za wafanyakazi wa makampuni hayo, zilikuwa shilingi bilioni 505.84, Makampuni yalilipa kodi pungufu kuliko kodi za wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2001 - 2012, makampuni yanayochimba dhahabu katika nchi yetu, yalipata mapato ya dola za marekani bilioni 11.9 au kwa fedha za kitanzania shilingi trilioni 19.635, katika kipindi hicho hicho (1999 - 2012), Makampuni hayo ya Madini yalilipa kodi ya shilingi trilioni 1.216 au asilimia 6.2 ya mapato. Serikali ya wala rushwa haiwezi ikakusanya kodi (Mwalimu Nyerere). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki tunachokipigia kelele hapa, tunapoteza muda wa Watanzania na muda wetu. Kama tunataka kukusanya

kodi, tukusanye kodi za Makampuni ya Madini, za makampuni yanayochimba gesi, tuache kufukuzana na wapaka wanja. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mtoto wa Afrika wa pili ninayemzungumzia, yuko kitandani anaweza akafa wakati wowote na tarehe 21 Septemba, 1953...

SPIKA: Sema Mungu ampe afya njema, siyo kumalizia hivyo tu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, umesema mwenyewe nashukuru sana. Tarehe 21 Septemba, 1953, mtoto huyo wa Afrika alisema, alikuwa amepigwa marufuku kukutana na watu zaidi ya watano, yeye na viongozi wote wa *ANC* na *South Africa Indian Congress*. Kwa hiyo, alisema kwa kuandika, hakuweza kwenda kwenye mkutano, alisema hivi:

"And therefore, the road to freedom is not easy, there is no road to freedom anywhere, and many of us, will have to pass again and again, through the valley of the shadow of death, before we can reach the mountain tops of our desires". (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya kwenda kwenye uhuru si rahisi mahali popote na wengi wetu tutapita mara kwa mara katika bonde la mauti ya kifo, kabla ya kufika kwenye kilele cha matazamio yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii nchi yetu inapiga watu mabomu kwenye mikutano ya hadhara, nchi yetu inapiga Wabunge, watu wanateswa Mtwara, wanakamatwa usiku, wanapigwa viboko, wanamwagiwa maji ya chumvi, Watanzania wanateswa, *we are going through*, tunapita katika bonde la mauti ya kifo. Mtasema sana, watu wamekufa, wameuawa! Bunge linaendelea na kikao kama kawaida! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maneno ya Mzee Mandela; hakuna njia rahisi kuelekea kwenye uhuru, mahali popote na wengi wetu tutapita mara nyingi katika bonde la mauti kabla ya kufika kwenye uhuru, ni maneno muhimu kuyakumbuka kwa siku kama ya leo ambayo mzee Mandela yuko kitandani.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu yote uliyosema sawa, lakini kwamba Bunge hatukuacha kwa sababu uliyoisema siyo sahihi!

Kwa hiyo, naomba niendelee na Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu, Mheshimiwa Murtaza Mangungu na Mheshimiwa Selemani Jafo!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Dkt. Kafumu hayupo.

SPIKA: Aaa, hayupo, basi Mheshimiwa Murtaza Mangungu tafadhali!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kwa kipindi hiki cha Bunge, naamini inaweza ikawa leo ndiyo mchango wangu wa mwisho katika Wizara hii mpaka pale Bunge lijalo ambalo litakuwa limepangwa hapo baadaye. Kwa hiyo, nikupongeze sana na kukuombea Mungu akulinde na Baraka zote ziwe kwako na Wabunge wote katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia tu, nimesikiliza mchango wa Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini nataka nimkumbushe mambo mawili. La kwanza, nataka nimkumbushe kwamba Tanzania ilipata Uhuru tarehe 9 Desemba, 1961. (*Makofi*)

Kwa hiyo, harakati za ukombozi wa nchi yetu zilishafanyika na tumeweza kuzisaidia nchi zote za Kusini mwa Afrika na tumepata uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ningepomba nimkumbushe, mazingira mazuri ambayo mpaka leo hii tunachangia kwenye Muswada wa ukusanyaji kodi wa nchi yetu, hayawezi kujengwa kama kutakuwa na vurugu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii nchi ilidai uhuru, lakini hatukumwaga damu na wala hatukupoteza roho za watu katika kudai uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wasomi ambao wanaaminika kwamba, wamesoma sana, tungeomba pia wazingatie kwenye Kanuni za Bunge ambazo zinatulazimisha tuchangie mada zilizowasilishwa ndani ya Bunge na siyo kuhusianisha mambo ambayo hayapo na tunawapotosha wananchi wanashindwa kuelewa yapi ambayo tunayafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa Sheria ya Fedha mwaka 2013, nimeleta *schedule* kwa *amendments*, nataka nizungumzie kwenye suala la *Incentives* ambazo zinatolewa kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya uwekezaji, pamoja na maneno mazuri ambayo yametamkwa na Kamati ya Bajeti ambayo ilipewa jukumu la kuchambua bajeti na Miswada hii, tumekuwa tukitoa *incentives* nyingi hata katika maeneo ambayo hayasitahili kupewa *incentives*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi utakuta kwamba ukienda Kariakoo au maeneo mengine ya Mji wa Dar es Salaam na kwingineko Tanzania, kuna wafanyabiashara ambao wanafanya biashara ya uchuuzi. Mathalani wale ambao wanaweka maduka ya kuuza bidhaa.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajitahidi na naamini kabisa Serikali imefanya jitihada kubwa sana ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, lakini ni lazima tuangalie maeneo yale ambayo tunatoa fursa za uwekezaji yanasaidia kiasi gani kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa mazingira haya ambayo tumeyaweka hivi sasa, wafanyabishara kutoka katika nchi ambazo tunaagiza bidhaa kwa wingi, nchi za *Far East*, kama Uchina, India, Malaysia, Indonesia, Singapore. Wanakuja kufungua wenyewe maduka na wanaendesha hizi biashara, kwa hiyo, wananyang'anyana ushindani wa biashara na wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanaweza wakawekeza mitaji ya biashara za aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, hili liangaliwe vizuri, tuweze kujenga mazingira mazuri ya Watanzania ili waweze

kushiriki katika uchumi wa nchi yao ambao unakua kwa kasi ambayo imetamkwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka niangalie kwenye hizi *HS codes* ambazo tunazitumia, hizi *HS codes* ambazo tunazipanga kama ndiyo viwango vya kodi vya ulipaji wa bidhaa ambazo tunaziagiza kutoka nje, tunaangalia zaidi kwenye *World Market*, lakini hizi bidhaa nyingi, au tunaweza tukasema asilimia karibu 90 ya bidhaa ambazo zinaingizwa Tanzania ni zile *limitation*. Sasa naishauri Serikali iweke kodi ambayo iko *reasonable*, wafanyabiashara wawe tayari kushiriki na kulipa hizi kodi na wasiwe wanatafuta mianya ya kukwepa ili kuweza kuokoa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi tutasaidia kwa sababu, kuingiza bidhaa Tanzania kuna *multiplied factors* ambazo wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali ambazo zinatuzunguka hapa wanaingia Tanzania kuja kununua bidhaa na leo hii kutokana na kodi kubwa ambayo tunaweka katika bidhaa hizi, wanakimbilia katika maeneo mengine, kama vile Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri Serikali, kwa kipindi hiki cha mpito, lazima tuangalie, tuweke kodi *reasonable* na tutanue wigo wa kodi ili Watanzania wengi zaidi waweze kulipa kodi, lakini walipe kodi kwa hiari, na vile vile tuzibe mianya ya upotevu wa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie, ni hizi *incentives* katika ku-*attract* watu kuja kuwekeza kwenye viwanda vya mkakati. Sijaona mkakati ambao Serikali imeweka na kwenye *schedule* ambayo nimeiwasilisha, nimeishauri Serikali kwamba iondoe kabisa kodi na vikwazo vyote katika viwanda vya mkakati, kama Viwanda vya Nyama, vya Ngozi, vya Kusokota Kamba, vya Katani, vya Kukamua Mafuta ya Kula, vya Matunda, vya Kuchakata Samaki na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi tutasaidia na tutaweza kuwapa fursa hata Watanzania ambao wana mitaji ya kuwekeza katika hizi bidhaa, basi wataweza kuwekeza kwa wepesi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie, katika suala la ukusanyaji kodi, Serikali inafanya jitihada kubwa sana kwenye ukusanyaji kodi, lakini, hebu tujiulize kwa kiasi fulani, kwamba kuna kampuni nyingi hasa katika sekta ya utalii, zinatumia hizi *electronic payments*. Kwa mfano, mtu anapolipa kwa kutumia *credit card ya visa au master card, anapo-charge, ile merchant Id,* inaonesha kwamba yeye ni *client* kutoka katika benki fulani ambayo iko nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zile fedha hata kama ile *section* iko hapa, atakapo-charge atatozwa fedha, lakini ile fedha haitaingia katika mapato ambayo yanaonesha ile hoteli, au ile sehemu ya huduma inapoonesha, ile fedha inarudi moja kwa moja katika nchi ambayo ile benki ina-*facilitate* ile *station*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa naishauri Serikali, ni lazima tutunge sheria ya kuweza kudhibiti manunuzi na mauzo haya ya *ki-electronic* ambayo nimeangalia katika Sheria zetu za Kodi, bado hatujafikia katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu kodi ya uchakavu wa magari ambayo yamezidi miaka 10. Naishauri Serikali, hili jambo ilianganalie vizuri sana, kwa maana kwamba, tunaweza tukaongeza kodi kwa maana ya kuzuia labda gari nyingi zisiingie. Najua zipo *effects* nyingine, kwamba gari chakavu zinahitaji *spare parts* nyingi zaidi, lakini tuanganalie pia na kupima mazingira ya nchi yetu yaliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea Serikali ingeshusha zaidi, ili *public transport* itumiwe na watu wachache zaidi kuweza kutanua wigo. zipo kodi nyingi ambazo Serikali wanaweza wakapata kwa kulipa mafuta, *road license* na bidhaa nyingine ambazo zinatumiwa kwenye magari hayo. Kwa hiyo, naishauri Serikali ilianganalie vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabisa, ambalo nataka nilizungumzie, ni suala la kupeleka huduma vijijini. Bajeti ya Serikali mwaka huu ni trioni 18, naishauri Serikali ihimize zaidi, siyo kupeleka fedha nyingi katika maeneo ya mijini ambayo mpaka sasa tumekuwa na *duplication* ya miradi. Miradi mingi ya vijijini ipewe

kipaumbele, wananchi wapate umeme, maji, barabara ili tuweze kuboresha maisha ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu ku-*declare interest* kwa sababu mimi ni mmoja kati wa waagizaji wa bidhaa kutoka nje, kwa hiyo, Kanuni yako ya 61, kwa maana moja au nyingine inaweza ikanihusu, kwa hiyo, hilo naliwasilisha kwako liweze kueleweka.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Ally Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Salim Turkey na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono moja kwa moja bajeti, tena asilimia 200 kwa 200, hakuna cha kupunguza, kama ulivyosema mwongozo; mtu anataka cha kupunguza, atafute pa kupeleka.

Mheshimiwa Spika, wananchi leo tukitoka hapa, Walimu wanataka mishahara, Manesi wanataka mishahara, Wabunge wanataka mishahara. Huyu Waziri wa Fedha atatoa fedha mfukoni kwake! Ukimpunguzia hata senti tano hawezi kupata fedha, tusidanganyane.

Mheshimiwa Spika, kama utakachopata kiongezeke, maana yake bajeti yetu mpaka sasa ni asilimia 70, asilimia 30 siyo zetu, ni tegemezi, je, wasipotuletea hao wajomba? Kwa hiyo, hata tutakazopata sijui kwingine huko, ziongezee ili bajeti yetu ifike asilimia mia moja siyo kuwa tegemezi.

Mheshimiwa Spika, nashangaa baadhi ya Wabunge, wanasema hii habari ya magari kuchakaa miaka 10, sijui wananchi hawana uwezo, ndugu zangu tusidanganyane. Leo mnasema Walimu au Manesi, watanunua magari, Mwalimu gani au nesi gani ana uwezo wa kunua gari milioni 20, tusidanganyane.

Mheshimiwa Spika, mtindo ni huo huo, magari yamezidi kujazana Dar es Salaam, asilimia 80 ya magari yanayoagizwa yote yanaishia Dar es Salaam, ndiyo maana inakuwa foleni kubwa,

hakuna pa kwenda, inakuwa *jam*. Kwa hiyo, lazima tujibane, hakuna kuagiza magari yaliyochakaa chakaa, yaliyokwisha, Tanzania imekuwa ni dampo, tunapata gharama kubwa sana kwa *spare*, hatujijui, fedha nyingi za kigeni nchi yetu inalipa kwa *spares*, watu hawaelewi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo utanunua gari, halijafika Chalinze lilishakufa, *spare* unaagiza, *spares* zenyewe zimekuwa kama mihogo siku hizi, hiyo haikubaliki, mdundo ni huo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima tujikaze, mnataka vizuri, shida yetu sisi ni maji, umeme, barabara na dawa, ndiyo wananchi wanachotaka. Hii kusema tupunguze, hakuna cha kupunguza. Nenda Zambia mafuta ni bei ghali, *DRC*, Kenya, Burundi, mafuta ni ghali. Hii ya kusema sasa mafuta ya taa yashuke, tuanze kuchakachua, tuharibu magari yetu, tuagize tena *spares*, mafuta lazima yalingane bei ili kuharibu habari ya kuchakachua au magari kufa baada ya kuchakachua.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kujua hii *EWURA* na hii rangi kwenye mafuta, vinasaba vya nini? Wakati mafuta yote yalishakuwa bei sawa. Tunapoteza bilioni 12 kwa kampuni ya mtu binafsi, anachukua sh. 6.30 kila lita, hiyo ndiyo tutoe.

Mheshimiwa Spika, hiyo sh. 6.30 iende tena kwenye *REA*, tuongeze ule Mfuko wa Umeme. Siyo kumtajirisha mtu bilioni 12, amekaa na kampuni yake, kampuni hewa na mihuri na rangi anaingiza kwenye mafuta, rangi ya nini? Mafuta yamekuwa bei sawa, rangi ya nini, hiyo haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi ya ng'ombe; imezungumzwa habari ya kodi ya ng'ombe ndugu zangu, kama Serikali Kuu imeshindwa kukusanya, ziende Halmashauri kama zamani, kuzipa uwezo Halmashauri kukusanya kodi ya ng'ombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumza mara ya kwanza hapa, wafuga kuku, mtu anauza *trays* mpaka 30 mpaka 40 za mayai ya kuku, hadaiwi kodi. Anauza kuku 500 mpaka 600 hadaiwi kodi. Lazima tukusanye kodi kwa njia yoyote ile, mtu ana ng'ombe 50 wa maziwa, anauza lita 300 mpaka 400 za maziwa, Dar es Salaam lita

mpaka sh. 1,500/=, lakini halipi kodi. Lazima tuongeze kodi, kila mtu alipe kodi nchi hii. Huwezi kula bila kufanya kazi, hata vitabu vya dini vimeandika, tusifanye ujanja ujanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maghorofa yamekaa Dar es Salaam wanapangisha, Oysterbay Nyumba, dola 2,000 mpaka 3,000 analipa kodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kodi ni lazima, kodi ndiyo inafanya nchi inakwenda. Watu wanazungumza habari ya nchi ndogo, Tanzania ina mtandao mkubwa, barabara ni kilomita za kutosha kuliko Rwanda, kuliko Burundi, tutaziendeshaje barabara zetu, tutajengaje reli bila kujikamua wenyewe.

Ndugu zangu, naona kitu cha ajabu kabisa, anasimama Mbunge kabisa, anajua maana ya bajeti, anasema punguza hiki, punguza hiki, siyo mtindo huo, Serikali itatoa wapi fedha. Waziri hana fedha za mfukoni, fedha ziko kwa wananchi wake hawa milioni 40, lazima tuichangie Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuishi kijanja kijanja, nchi ambayo haikusanyi kodi, haiwezi kufanya maendeleo na tukikaa tunajitetea tetea sijui tufute hiki, tufute hiki, onesha wewe pa kupatia kodi, Mheshimiwa Spika asubuhi amezungumza hapa, ukifuta shilingi mbili, tuoneshe shilingi nne zitatoka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unakuja kusema sijui tutoe kodi, tutoe kodi. Wewe, Rais Kennedy wa Marekani alisema: "Usiulize Marekani imekufanyia nini, sema wewe umeifanyia nini Marekani. Wewe umekuja tu, unadai kila kitu, umeifanyia nini Tanzania? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hadithi ya kizamani ile, wakati ule tukiwa wadogo, kwamba, Serikali inatengeneza hela. Kwa nini isifyatue tu pesa? Sasa Serikali itafyatua pesa kwa namna gani. Fanya kazi kula jasho lako. Wewe unadai, unaogopa wananchi watatucheka kule nje, sijui watachachamaa au watasema kwa vipi, wao wenyewe wameisaidia nini nchi hii. Kuuza vichupi barabarani na maji barabarani, ndiyo wameisaidia nchi hii. Wafanye kazi, wale jasho lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunachotaka ni maji, tunataka barabara, tunataka dawa na dawa haipatikani, maji hayapatikani bila kukamuliwa kodi. Kodi ndiyo chanzo chetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Wazungu wanalipa kodi, ndiyo kodi yao inakuja huku kwetu, je, leo hii wakisema sisi hatulipi kodi, tutaishi vipi? Tulidai uhuru kwa ajili ya kuwategemea Wazungu? Tujitegemee kwa kila kitu, ndiyo faida ya kudai uhuru. Mnakuja mnasema sijui vitu vya ajabu ajabu hapa. Ni wajibu kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna kukwepa. Ukisema utoe hiki, uoneshe pa kulipa kodi. Wewe umekwenda kuoja mke, jenga kwanza nyumba na namna ya kumlisha mke wako. Siyo siku ya kwanza tu, unaomba chumvi kwa jirani, chai kwa jirani, mwisho huyo mke atakukimbia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wazungu wamekuwa wana masharti magumu. Tutakwenda kubaya, wote mnasikia kila siku masharti ya Wazungu yanaongezeka. Mheshimiwa Rais Barack Obama, juzi amesaini kuoana wanaume kwa wanaume amekubali na Jumatatu tarehe 1 Julai, 2013 anakuja hapa Tanzania. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuoneshe mfano. Tujitegemee kwa asilimia mia kwa mia (100%) ili na sisi tuweze kuwakopesha Mataifa mengine majirani zetu. Kwa hiyo, ndugu zangu nawaomba, Bajeti hii iendelee na kama hizo ziada mnazosema ziongezwe, ziongezeke ili tupate maendeleo zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwangu hatuna barabara ndugu zangu, siwezi kukubali mambo ya kupunguza pungua kodi hapa. Tukamuane kodi ili tupate pesa zaidi, tukienda kwa Waziri kuomba barabara, hela inakuwa wazi, tukiomba maji, hela ipo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mmemuonaje leo Mheshimiwa Ally Keisy Mohamed. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa anayefuata ni Mheshimiwa Selemani Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Salim Turkey naye atapata nafasi.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nipende kukupongeza wewe. Kwa sababu mwaka huu Watanzania umetuonesha ni kwa jinsi gani tunaweza tukatengeneza Bajeti ya nchi yetu. Miaka yote toka niingine Bungeni hapa tulikuwa kama *Rubber Stamp*. Serikali inaleta Bajeti yake mara ya kwanza, sisi tunapiga kelele bila kuleta manufaa ya aina yoyote. Hata hivyo, nakushukuru sana busara zako zimesaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tumeona jinsi gani pesa nyingi zimeweza kuingia katika Miradi ya Maji. Ahsante sana. Karibu Shilingi Bilioni 184.6 ni pesa nyingi sana. Hata kule kwangu Kisarawe nasema mwaka huu mmetusaidia, kwa mchakato wako mzuri wa bajeti mmetusaidia sana, lakini busara zako zimetusaidia hata upatikanaji wa umeme Vijijini. Tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote wa Bunge hili, kwa sababu sikupata siku ile nafasi, niwashukuru kwa sababu nimechaguliwa kuwa Mbunge wa *SADC*. Ahsanteni sana Wabunge wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kwenda kama tutakuwa tunaoneana aibu. Nchi yetu tunatakiwa tusimame imara na tuseme *No*. Naomba kwanza upande wa Watendaji wote, wanisikilize vizuri. Tumekuwa na matatizo makubwa sana katika suala zima la ukusanyaji wa kodi. Ndugu zangu hatuwezi kwenda kama tutashindwa kukusanya kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie katika eneo moja. Leo hii Tanzania Wafanyakazi, ukiangalia kumbukumbu ya mwaka 2011/2012 *PAYE* ya Wafanyakazi karibuni imechangia asilimia 17 ya mapato yote. Bahati mbaya sana, kuna Makampuni mengine yanaajiri wafanyakazi wengi. Lakini pesa wanayokata kwa wafanyakazi, pesa zile haziendi katika Mfuko wa Hazina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata ukienda kwenye Makampuni ya Madini, katika Makampuni mbalimbali hapa nchini wanakusanya kodi kutoka kwa wafanyakazi, lakini kodi zile haziendi Serikalini. Ndiyo maana nikawa nina mapendekezo toka muda mrefu sana, kwamba, sasa ikiwezekana kila mfanyakazi apewe *TIN number* yake ili kila kodi ya mfanyakazi iingiapo Serikalini. Mfanyakazi aweze kutumia, Serikali iweze kuweka utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa *TRA*, watumie mfumo wa kiteknolojia. Mfanyakazi atumie simu yake ya mkononi, kwa kutumia nambari yake ya *TIN*, ajue kama kodi yake imepelekwa Serikalini. Naiomba sana Kamati ya Bajeti, kwamba sasa hivi ifanye *Inventory* ya Makampuni yote yaliyokuwepo Tanzania, iangalie idadi ya wafanyakazi walioko Tanzania na iende *TRA*, ikafanye *assessment* kuona kama kweli wafanyakazi hao, kodi zote zimepelekwa Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hapa ndiyo maana, utakuja kuona wakati mwingine kweli tunawaminywa wafanyakazi. Ni kwa sababu tumesema hatuwezi kupunguza hii Bajeti tuliyoipanga, lakini ukiangalia kweli hivi sasa mzigo wanaoubeba wafanyakazi, kodi wanayolipa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ukichunguza kwa mfanyakazi anayelipwa mshahara wa sh. 6,000,000/=, lakini kodi anayokatwa ni ya hatari. Ni kwamba inawezekana tunaona kwamba mianya ya kodi katika ukusanyaji ni midogo, ndiyo maana tunakwenda zaidi kwa wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tuutanue wigo wetu huu wa ukusanyaji wa Kodi ya Mapato, hasa tuangalie jinsi gani Tanzania tumekuwa na Makampuni mengi sana ya Madini.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi tulifanya ziara Botswana. Nchi ya Botswana wanao mgodi mmoja tu wa almasi. Kaka yangu Mheshimiwa Kamani, yeye anajua vizuri zaidi yangu. Mgodi huo wa almasi unachangia kwa kiwango kikubwa sana cha mapato ya nchi ya Botswana. Leo hii Tanzania tunayo migodi mingapi.

Mheshimiwa Spika, tujikite huko, naiomba sana Serikali, tusiwaone aibu watu, watu wamekuja kuchukua pesa katika nchi yetu. Hivi kwa nini watu wanashindwa kukusanya kodi katika Makampuni ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanatanua na kuishi maisha ya anasa. Pesa zinakwenda nchi za nje, mali ni za kwetu sisi wenyewe tukusanye kodi. Naamini tukijipanga vizuri, kwa mfano, ukienda kwa Kaka yangu Christopher Ole-Sendeka, pale Mererani. Mgodini wa Madini wa *Tanzanite* peke yake, ukiambiwa siri ya mafanikio, ni kubwa kweli, nchi yetu tungepeleka mbali kwa kweli. *We are not serious* katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tujipange, tuweze kuangalia hizi rasilimali zetu zinatunufaisha vipi kwa mustakabali wa nchi yetu. Kwa kweli naumia sana. Nilikwenda Mererani kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, *Tanzanite* inayotoka pale kwa kweli ni utajiri wa ajabu sana. Lazima tujipange na kusema *no*.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana ndugu zangu naomba niwaambie, maisha yetu tunayoishi duniani ni machache sana, lakini tutakwenda kujieleza kwa Mwenyezi Mungu. Haya mambo maana yake kuna watu wana manufaa katika haya mambo, siyo bure! Lazima katika nchi hii tukubali kwamba lazima tuumie na uchungu wa nchi yetu. Usinufaike wewe kwa kujenga nyumba yako na kuliacha Taifa la Tanzania linateketea. Hatuwezi kwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yako hasa ya Bajeti, naishukuru sana, lakini ina kazi kubwa ya kufanya. Naomba uiagize Kamati yako iende kwa undani kutafiti katika Sekta ya Migodi ya Madini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumefanya mambo makubwa sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, nchi yetu inaendelea. Lakini tunaposema tunataka tukusanye kodi ni kweli, nasikitika sasa Wizara ya Mifugo, kwamba kuna pesa nyingi zinapotea katika nchi hii, ukianza Mifugo yenyewe mpaka katika *Deep Sea*, Samaki ya Baharini kule. Lakini *we are not serious* kila siku

tunazungumza hapa. Hakuna biashara ya kulialia, tutafute pesa.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani manufaa ya samaki wa Tanzania, wananufaika watu wa nchi nyingine. Hilo jambo haliwezekani! Naamini kama tumejipanga vizuri sisi Watanzania bajeti yetu kwa asilimia mia moja tutai-*support* sisi wenyewe.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ally Keisy Mohamed, amesema hapa hivi punde. Akisisitiza, jamani uchumi sasa hivi unabadilika, tunakokwenda ni kwingine kabisa. Hali tunayo kwenda nayo ni ngumu. Masharti ya Wafadhili, yatakuwa ni ya hatari, mpaka watoto wetu watakuwa katika mazingira magumu kwa kweli. Lazima tuseme *no*, tujipange vizuri kwa kuhakikisha kwamba kodi tunaikusanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuishauri Wizara ya Fedha, kwamba, hapa leo tunazungumza suala zima la fedha zikusanywe. Lakini matumizi ya fedha huko zinakokwenda inakuwa ni changamoto kubwa. Naomba sana na nitaleta hoja binafsi hapa, kwamba ikiwezekana kwa sababu watu wa utendaji peke yake sasa hivi ndiyo wanasimamia pesa.

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana nitaleta hoja binafsi, kuleta utaratibu wa kuweka *Financial Communication Protocol*, kwamba kila mwezi hata Mbunge na Mwenyekiti wa Halmashauri, katika Halmashauri, waweze kupata *transaction* zinaondoka kwa utaratibu maalum. Tuweze ku-*control* pesa, badala ya Kamati za Fedha peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la sivyo, tutasema pesa zikusanywe na hiyo Miradi haitaweza kufika katika malengo tunayokusudia. Hali hiyo sisi inatuuma sana, wananchi wetu wako katika hali ngumu. Kwa kweli hatuwezi kuvumilia. Kama mambo hayaendi vizuri, watakaofanya vibaya tutasema hawa watu wamefanya vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na timu yake, kwamba katika yale maombi ambayo tumeyapeleka Wabunge, katika suala zima la maji, katika suala umeme vijijini,

katika suala zima la vijana na suala zima la Sekta ya Mfugo, Serikali imeweza kuyafanyia kazi. Kwa hiyo tunashukuru sana, isipokuwa ni kwamba, jinsi gani tujipange sasa hivi, tuweze kukusanya vizuri kwa manufaa ya wananchi wetu ili waweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu siwezi kuwa na uwezo wa ku-*move schedule of amendment*, naomba kusema kwamba, Wizara ya Fedha ijipange na kuangalia suala zima la makato ya mishahara kwa wafanyakazi. Kodi imekuwa ni kubwa, lazima tujipange vizuri. Wasipokuwa na uwezo wa ku-*purchase* vizuri, maana yake wafanyakazi wetu wataishi maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana suala la uratibu wa suala zima la kodi ya wafanyakazi inayokatwa ni kubwa sana. Tuangalie katika siku zijazo tufanyeje kuwapunguzia mzigo wafanyakazi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kusema nimehitimisha hapa. Naunga mkono hoja hii, ili mradi zile pesa ziweze kupatikana kwani Jimboni kwangu ninavyo visima 30 vinavyohitaji matengenezo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa John Shibuda Magale, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hassan Abdallah Turkey na Mheshimiwa Kebwe Kebwe atakuwa wa mwisho kwa jioni hii.

MHE. JOHN S. MAGALE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii, nami niwe mshiriki katika fikra za kutafakari na kusemezana kuhusu Sheria inayohusiana na Muswada wa Wizara ya Fedha na Bajeti kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, napenda kukiri kwa dhati kabisa kusema kwamba, Wizara hii imepata muungwana na mstaarabu. Mtu ambaye hana kauli na matendo ya ubinafsi na ya kujikweza, lakini Waungwana husema kila chema hakikosi kasoro.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Bajeti, huu uliouanzisha na kupitia mtazamo wako uliozaa ubunifu mpya wa kujadiliana na

kujenga upatanifu kati ya Bunge na Serikali, napenda kusema kwamba, ni hatua endelevu. Lakini tunapaswa kukubali kwamba watumishi wa Wizara ya Fedha ni vema wakajiona kwamba ulipoanzisha Kamati ya Bajeti ya Bunge, siyo tunakosoa na kufedhuli uwezo wao wa taaluma, maarifa na ujuzi wao. Ni vema wakakubali kwamba Tanzania itajengwa na umoja wa ukuni na ukuni huivisha chungu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni hasara sana ikiwa Wizara ya Fedha, watakuwa na nongwa pale wanapopokea ushauri kutoka Kamati ya Bajeti ya Bunge, wakajihisi kwamba tunawashutumu kwamba labda hawakuweza kuwa na maono ya kutafakari na kuleta maslahi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kila jambo na wakati wake. Sasa wakati umepevuka Watanzania tujenge mshikamano wa kuendeleza dhana ya kwamba, Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko makubwa sana, tusipoenzi kwamba, mtu aliye na hekima, aliye na busara, anayetanguliwa na hekima huwa hana tabia ya kifuniko kwa maovu. Leo napenda kushukuru kwamba, tumeenzi na tunathamini sana msemo wa Wakongwe kwamba anayekosoa ni mstaratibu kuliko msengenyaji anayekaa kichinichini. Hata Mheshimiwa Tundu Lissu, leo nakupongeza kwa kutoa ya nafsini mwako. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya kwa sababu tukubaliane kwamba, kama tutakuwa na uhafifu wa kutafakari na kuona kwamba dhana ya utozaji kodi, inaweza ikawa ni dhana isiyo kuwa na machungu kwa tabaka la kati la uchumi, basi tuelewe kwamba, Tanzania tumepotea njia.

Mheshimiwa Spika, tukubaliane makato yatakayozaa ada, yatakuwa na mashinikizo makubwa sana kwa tabaka ambao halipokei mshahara kila mwezi. Tukubaliane watu wa vijijini, wakulima wa pamba wanategemea pamba kwa msimu mmoja kwa mwaka. Je, wanavijiji hao ambao hawana mshahara wa kupokea kila mwezi, Wasukuma wangu hao na watani zangu ambao wanalima pamba, wanayo masikitiko makubwa kwamba, tozo ambazo zitaibua ada mbalimbali kwenye simu na mahali pa

huduma zinazohitajika kulipiwa nyongeza, tujiulize kwamba, zinakwenda sambamba na uhai wa uchumi wa jamii wa familia kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaasa Wizara ya Fedha, timizeni haya ambayo tumeyapitisha hapa. Sasa kuweni na ufunguo wa fikra, muwe kiona mbali. Bajeti ijayo mtambue kwamba, kuna tabaka la Watanzania ambao maisha yao na kipato chao ni goigoi.

Mheshimiwa Spika, tuna tabaka la watu wa utumishi Serikalini na Makampuni na Taasisi, mishahara yao ni mikubwa na *Alhamdulillah*. Lakini unapokuja kwa mtu wa kijijini, kauka nikuvae, tunapoanza kumfikiria tunampa tozo ambazo anashindwa hata kuzimudu, mnajenga machukizo dhidi ya utumishi wa Serikali, mnajenga machukizo dhidi ya utumishi wa CCM, mnajenga machukizo dhidi ya kumuenzi Baba wa Taifa aliyewapenda Watanzania wake maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ndiye Mshenga wa kujenga mahusiano baina ya jamii, lakini napenda kusema kwamba, naomba niwaulize ndugu zangu, je, Wizara ya Fedha haya ambayo tumeyapitisha hapa, ni bima kwa ustawi wa maendeleo ya jamii? Yanamsaidia vipi Mtanzania mlalahoi, makabwela, wavuja jasho. Je, Bajeti hii kwa kiasi gani itakuwa ni MKUKUTA kwa walalahoi? Je, tozo hizi za kodi, zina mnyumbuliko wa mrejesho, mtoko mrejeo wa aina gani, kwa mlalahoi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu, lindo la utawala bora ni kujali watu fukara na kulinda watu maskini. Maandamano katika nchi mbalimbali tunazoziona ni kwa sababu watu wameona kwamba, wanakamuliwa bila kujua watakula wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri alitazame sana, ni mfumo wa *TRA*, wa kuwekewa malengo ya kutoza kodi. Kwa hiyo, Watumishi wanakamua wananchi bila kujali kwamba huyu mwananchi hakutengeneza faida. *TRA*, wanakuwa ni watu ambao wanataka kulinda maslahi yao na ajira zao. Hebu mlitazame hilo.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ni la sare ya CCM na Serikali ni ya CCM, ninyi ni mapacha wa siasa ya CCM na Itikadi ya CCM, lakini jiulizeni na mjitambulisha, mbele ya jamii, tunataka kutekwa na kada ya utajiri wa kati.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatekwa, tunawasahau watu wa chini, walalahoi, kila siku mnazungumzia maslahi ya tabaka la kati. Kwa sababu wasomi ambao mna mishahara hivi sasa mikubwa mikubwa, mnaona kwamba tozo za kodi hizi hata kwenye simu mnapotuma pesa hazina kero yoyote, hazina ghadhabu yoyote. Lakini kwa mtu maskini ni kero na mmejenga fitna.

Mheshimiwa Spika, napenda niwaambie hamtakwepa machapio ya kisiasa. Hamtakwepa mang'amuzi ya kisiasa ya kushutumiana kwa sababu mtu wa chini, rufaa yake ya ni Bunge na mtu wa chini rufaa yake ni siasa.

Mheshimiwa Spika, kama hamtoweza kukaa mkatafakari, kupitia vikao vyenu, mkaja na hoja ya kwamba, pale ambapo kuna mserereko wa kudidimiza ustawi na maendeleo ya Mtanzania wa hali ya chini, basi mjitambue mnaweza mkakaa, mkajiuliza mazalia ya makusanyo mengine mnaweza mkakokotoa wapi? Msiogope kuleta *Supplementary* ya kutoa tuzo la uwajibikaji kwa maslahi ya walalahoi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hivi sasa tumekuwa na kiwewe na tabaka la kati. Watu wa chini hawana sikio. Nasikitika kusema kwamba, watu wamekuwa vipofu, wamekuwa viziwi na hawana mahali pa kusema kwamba ni sauti ya maslahi ya kijamii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. JOHN S. MAGALE: Wakumbuke...

MBUNGE FULANI: Kengele ya pili.

MHE. JOHN S. MAGALE: Kengele ya kwanza hiyo. Usiwe na hila.

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa ni ya kwanza.

SPIKA: Ni kengele ya pili, bwana wewe tumeshamaliza. Sasa namwita Mheshimiwa Salim Hassan Abdullah Turkey na atamalizia Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe.

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nichukue fursa hii, kuwapongeza Waziri wa Fedha na Manaibu Waziri wake na Kamati zote waliochangia katika Bajeti hii. Kwa kweli naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nishirikiane na wenzangu, kwamba nchi yenye amani ndiyo nchi ambayo inaendelea. Leo hii bila ya amani, nchi hii haiwezi kwenda mbele. Kwa hiyo, nasaha zangu kwa Watanzania wote na hasa Wabunge kwamba, tujitahidi kudumisha amani ya nchi hii, kwani ndiyo itakayofanya nchi hii iendelee na kodi zipatikane nchi iendelee mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba ku-*declare interest*, toka kuzaliwa kwangu mimi ni mfanyabiashara. Mwenyezi Mungu amenijalia nimekuwa mtu wa viwanda, *Alhamdulillah* akanijalia nimekuwa mtu wa viwanda na *Alhamdulillah* nashukuru kanijalia na sasa nimekuwa Mbunge, nimeingia katika siasa. Kwa hilo, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaingia katika mada ambayo ndiyo naielewa na ndiyo fani yangu. Nchi yoyote ili iendelee katika dunia ni lazima tuwekeze katika viwanda na ili viwanda viwe vya uhakika, basi Serikali nayo iwe imejipanga kulinda viwanda hivyo. Ni sera ya Serikali ambayo imefanya watu wavutike kuwekeza katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna viwanda vinaitwa *Integration, integration* maana yake kiwanda ambacho kinaanza na *raw material*, inakuja inafikia mahali unapata *semi finish product* na baadaye unapata *finish product*. Sasa jambo la kushangaza sana Serikali yetu inachezea sana hizi Sheria na hivi vivutio walivyoviweka kwa ajili ya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unashangaa kwamba, Serikali imetoa kauli na katika uwekezaji Sheria hiyo ipo kwamba *any semi finish product* ikiingia nchini, lazima ilipishwe *ten percent*, hiyo ndiyo Sheria na mtu yeyote ambaye ataweka kiwanda kwa kutumia *raw material* basi lazima apewe *zero* bila ya kutazama kwamba, kiwanda kile kitamtosheleza mlaji au hakimtoshelezi mlaji. Ni kiwanda chenyewe kikiwekeza tu na mifano hai tunayo.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vya Saruji tunavyo vitatu tulivyorithi kwa maana ya Tanga, Mbeya pamoja na Dar es Salaam. Viwanda hivi vina uwezo mkubwa sana wa kuunguza mawe ndiyo *raw material* zenyewe, wanapata kitu kinaitwa *clinker* ambayo ndiyo *semi finish product*. *Semi finish product* ile ndiyo wanatengeneza saruji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchini hapa kuna viwanda vinne vimeshakuja vina-*invest* katika *semi finish product* kwa maana wao wata-*import clinker* na hivi viwanda vya nchini wanatengeneza *clinker* wanajitosheleza wenyewe, hawawezi kutupa sisi wenye viwanda vidogo vidogo. Kwa sababu na mimi mwenyewe karibuni nitaanza kiwanda changu cha saruji Kisarawe. Kwa hiyo, hawana uwezo wa kutupa sisi. Sasa je, tuiambie Serikali *clinker* ile ambayo wale viwanda wanaizalisha ni kwa ajili yao tu, sisi viwanda vidogo vidogo hawawezi kutupa, kwa hiyo, Serikali ifanye *zero*. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, sasa tunakuja katika mada yetu kuu ambayo hiyo ndiyo yangu mimi hasa ni *LABSA*. Kiwanda cha *LABSA* hali kadhalika miaka miwili iliyopita Serikali hii iliweka kodi ya asilimia 10 kwenye *LABSA* inayoagiza kutoka nje ya nchi na hicho ndiyo kikawa kivutio kwetu sisi tuwekeze kiwanda ili ile asilimia 10 tupate *zero*, tukawekeza kiwanda cha kutengenezea *LABSA* kwa kuiona ile kodi ya asilimia kumi ndiyo *protection*.

Mheshimiwa Spika, leo tusifichane uzalishaji wowote utakaofanyika ikiwa China, ikiwa India na nchi za nje zozote hatuwezi tukalinganisha uzalishaji wa nchi zile na uzalishaji wa nchi yetu haiwezekani ni vitu viwili tofauti kabisa, gharama zetu sisi zipo juu ukilinganisha na wale, maana *raw material* wanazo wao, umeme kwao ni wa uhakika, teknolojia wanayo, mashine zenyewe

wanatengeneza wao, sisi tunanunua kwao. Kwa maana ile *ten percent* ndiyo inayo-*complement* mambo haya mengine yote.

Mheshimiwa Spika, sasa unapokuja ukasema kwamba, unataka kiwanda hiki lazima tuwalishe wote, hiyo siyo Sheria tuliyoambiwa ndani ya nchi. Ndani ya nchi tumeambiwa *integration plant* yoyote itakayoanza na *raw material* iwe *zero*, ndiyo maana tukawekeza. Sasa leo Serikali yetu sikivu, inakuja inasema kwamba sisi tunaweka *zero*, sawa wekeni kwa sababu nyie ndiyo wenyewe ubavu, lakini sisi watu ambao tumekwenda mabenki, tukakopa, tukaweka viwanda hivi na baada ya kuweka sisi pia kuna Kiwanda cha *Royal* kimeanza kutengeneza *LABSA*.

Mheshimiwa Spika, leo viwanda hivi vimewekwa kwa sababu ile *ten percent projection* ipo. Sasa unapoondoa *ten percent* ile, mtu aagize kama soko, *raw material*, *semi finish product* ambayo Serikali imesema lazima ilipiwe *ten percent*, inakuja kwa *zero* na huku *raw material* watu wamewekeza milioni karibu milioni 14 katika viwanda hivi, tunawekaje, tutalipa vipi madeni ya watu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Serikali inaweka ziro, basi itusaidie na sisi tukapate njia ya kuweza kulipa hizi *interest* za watu. La kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna usemi kwamba kuna viwanda vidogo vidogo vinavyotengeneza sabuni ya unga, sisi hapa sote ni Wabunge, kila mmoja anatoka katika katika Jimbo la Tanzania na kila mtu ana Jimbo lake. Swali langu kwa ndugu zangu, ni kwamba nani ana kiwanda cha sabuni ya unga ndani ya Jimbo lake. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako ikiwezekana basi, waoneshe mikono kwa sababu kuna usemi wa uongo unasema kwamba, nchi hii ina viwanda vya kutengeneza sabuni ya unga, hakuna. Tunavyo viwanda vitatu tu hapa vinavyotengeneza sabuni ya unga; *Murzah Oil*, *Royal* pamoja na *Family*. Sasa huyu *Family* yeye ana kiwanda kikubwa sana, kiwanja chake tu ni *dollar* milioni mbili, mashine na nini na kila kitu karibu *dollar* milioni saba. Leo kiwanda hiki unakithamini kiwe kidogo kwa misingi gani, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tunaomba sana na nimesema Mheshimiwa Waziri ananisikia, Wabunge wote tupu, tuna Majimbo yetu, wathibitisha, nani anatengeneza sabuni ya unga, tunadanganya. Kwa hiyo, hii kodi ya asilimia kumi, wapo Wabunge wanasema kwamba wafanyabiashara hawawezi wakalipa kodi, basi mimi wa kwanza leo nasema na kama kuna usemi kwamba sisi ndiyo tunaoagiza LABSA nyingi, sasa sisi ndiyo tunaokubali tulipe asilimia 10 Serikali ipate. Lakini hilo nalo ni la uongo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati tunaanza kiwanda hiki, tuliagiza *container* karibu sitini kwa sababu kila mwezi tunatumia *container* moja ya LABSA, sasa huwezi ukaanza kiwanda usiwe na *raw material* ya *backing*, mashine mpya inaweza ikagoma kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati ule walipotembelea Waheshimiwa Wabunge na Wenyeviti wakaona kwamba ile *material* ipo, wakafikiri sisi tunaagiza, lakini ile ilikuwa ni *stock* yetu. Kuanzia Januari mwaka huu mpaka leo hakuna LABSA iliyoagizwa kutoka nje na hivi kwa taarifa zetu Wabunge tunaumia, kiwanda tunaendesha siku 12, 13 *raw material* hatuna pa kuuza. Kwa sababu *material* ukienda kununua nje tunawanufaisha Wachina na Wahindi, wao wanatengeneza kwa rahisi lakini ikija hapa inapita bure. Hivi viwanda vitaishi vipi na madeni ya watu tutalipa vipi? Huo ndiyo ukweli wenyewe na uwazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwasilishe hili na ndugu zangu Wabunge mlifahamu. Hapa siyo mahali pa kupiga debe la bure, tuwe na hoja za nguvu jamani, tusiwe na upendeleo wa kipuuzi puuzi tu. Tuongee vitu vya ukweli na uhakika na hili nasema ni ukweli na niko tayari kama kuna Kamati inataka kuundwa kuja kuangalia kiwanda, ije kesho waangalie kama hakuna *fifty tones per day* na tunatumia tani ngapi na *material* inayobaki ni ngapi.

Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la Tanzania na nasema kwa mdomo mpana na ukweli mtupu na anayeweza kubisha aje na mimi ninatoa *challenge* kwamba hiyo ripoti iliyoletwa katika BACHET pamoja na Baraza la Viwanda Biashara ni uongo tupu, hakuna

demand ya sixty thousand tones ya LABSA katika nchi hii haipo, tunadanganya.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna kitu kinasema kwamba, tunazalisha tani 27 katika nchi hii ni uongo. Sisi tunazalisha tani 18 na tunatumia tani 7,200, ziada tunayo, tunataka tuuze ndani ya nchi yetu, hili ndiyo tunalopigania. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aitazame kwa moyo mkunjufu na huruma sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER OLE- SENDEKA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Huyu amekwisha *declare* kwamba anayosema ni ya kwake, amesema, hukuwepo ndiyo maana nikanyamaza. Amesema ni ya kwake na yeye yumo katika hiyo shughuli. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

MHE. CHRISTOPHER OLE- SENDEKA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Naona muda haunitoshi. Mheshimiwa Dkt. Kebwe!

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika Muswada huu wa Matumizi ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani kwa aliye juu kwa Watanzania wote ambao walipigia kura Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa Kata na kunyanyua ushindi wa kishindo ikiwemo Kata ya Machila pale Serengeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati ya Bajeti hayajawekwa wazi ili kusudi pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wana mawazo mengine ya ziada kuchangia katika njia zingine za kuongeza mapato, waweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, hili litaleta siha na afya katika masuala ya mapato ya nchi yetu. Nikijaribu kuangalia suala zima la utalii wa ndani halijazungumzwa sana katika bajeti na katika maeneo ya tozo ili kusudi eneo hili liongeze mapato.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia ni asilimia mbili ya mapato ya utalii yanayotokana na utalii wa ndani ni kiasi kidogo sana. Hata ndugu yetu jirani Mheshimiwa Kagame anatutania, anasema hivi Watanzania mmekuwaje nyie, mie ningepewa Tanzania vyanzo vingine vyote ningevifunga nishughulike na utalii pekee yake, ningeweza kuendesha nchi bila kutetereka na bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, mfano, tuliiona wakati ule wa kwenda kufanya *medical tourism* kule Loliondo kwe Mzee wa Loliondo wanamwita Babu, mbona mapato mengi sana yaliingia na wale walikuwa wanakwenda kwa ajili ya tiba, lakini walikuwa wakifika getini wanatozwa, fedha nyingi sana TANAPA walipata. Hii ni njia mojawapo ya utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la utalii wa ndani asilimia mbili hii haikubaliki. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ijipange, ni njia nzuri ya kuongeza mapato. Hatuwezi kusema katika dunia sisi ni wa pili baada ya Brazil kwamba, tuna vivutio vingi vya kitalii, halafu hatukusanyi, siyo nzuri. Wenzetu wa Japan, ukizaliwa sehemu yoyote ile ya Japan lazima uende sehemu nyingine ya Japan, ku-*encourage* utalii wa ndani kwa ajili ya kuongeza mapato. Kwa hiyo, suala hili litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, lakini mafuta ya kula haiwezekani sisi tuna maeneo mengi, tuboreshe viwanda haya mafuta ya kula yapatikane nchini. Mafuta ya kula ambayo yanaingia nchini asilimia 60 ni fursa ambayo kwanza tunawanyima Watanzania kwa sababu alizeti yetu ingeweza ikaboreshwa na katika maeneo mengine ufuta tungeuboresha, tukainua kipato.

Mheshimiwa Spika, mafuta haya ya mimea ni namba moja, hayana *cholesterol*, kwa hiyo masuala ya magonjwa sijui ya *pressure*, moyo kadhalika haviwezi kuwepo kwa kutumia mafuta ya aina ya mimea. Kwa hiyo, ni vizuri fursa hii nzuri tuitumie kwa kuongeza kodi kwa haya mafuta ambayo yanatoka nje. Kwa ajili ya ku-*encourage* uzalishaji wa mafuta ya ndani ya mimea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo nchi zingine wanavyofanya kwa kuongeza kodi na ndiyo sababu unaona hata maji tunashindwa, maji ya Rwezori kutoka Uganda yapo mengi sana Tanzania, lakini ukienda Uganda huwezi kukuta kuna maji ambayo yanatoka Tanzania. *Famous* maji ya Kilimanjaro, lakini huyakuti Uganda. Kwa hiyo, mbinu kama hizi ni njia nzuri za kusaidia kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikijaribu kuangalia katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri amezungumza suala la VAT. Kuongeza kodi hii ya ongezeko la thamani katika utalii, maana yake unasema gharama za utalii ziongezoke. Sasa wenzetu wanatumia fursa hiyo, gharama zikiongezeka kwetu sisi wao wanapunguza halafu watalii wote wanakwenda katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya imekwenda mpaka inagusa na wakazi hususan wa Kanda ya Ziwa wakiwemo wa Wilaya ya Serengeti, kwa sababu ukisema unapandisha gharama za usafiri toka sh. 1,500 ya ongezeko lile kwenda sh. 10,000 mzigo huu unakwenda kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali iangalie suala hili isiongeze adha na kuongeza mzigo kwa wananchi. Mathalani magari yale ambayo ni malori kutoka Kanda ya Ziwa wanavyokatisha Serengeti wanapita Ngorongoro kwenda Arusha kwa ajili ya kuchukua bidhaa za viwandani. Unakuta lori wana-charge sh. 25,000/=, lakini mwelekeo ni kwamba watakwenda ku-charge sasa sh. 100,000/=. Kwa hiyo, lori hilo litoke Kanda ya Ziwa ikiwemo Serengeti kwenda Arusha na kurudi ina maana ni 400,000/= kwa lori moja hilo. Sasa mzigo huo utakwenda wapi? Unakwenda kwa mlaji ambaye ni mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaishauri Serikali katika maeneo mengine ambayo tumeshauri waangalie vyanzo vizuri vya mapato, lakini kodi hizi ambazo wanaongeza ni vizuri kuongeza kodi, ni kitu kizuri hatukatai, lakini ongezeko hilo ni kubwa, linatisha na ni mzigo na ni mzigo kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, hakuna Serikali hata moja duniani ambayo haitozi kodi na kwa njia hii kama kodi inatozwa, ambayo inakwenda

katika uwezo wa mlaji, hiyo inakubalika, lakini siyo kuweka mzigo mzito ambao unakuwa ni adha kwa Mtanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikijaribu kuangalia ile kodi katika ushuru wa bidhaa, ile Sura 148 imezungumzia eneo hilo. Kwa hiyo, ni vizuri mabadiliko yale yafanyike ili kusudi kupunguza hiyo adha. Lakini ongezeko limepitia katika Muswada ule ushuru wa bidhaa katika sigara wameongeza kodi vizuri. Lakini katika sehemu ile ya *cigar* ni *zero*, *cigar* nayo iongezwe kodi, ni sehemu vile vile ya kudhibiti matumizi ya tumbaku na nchi zingine ndivyo wanavyofanya wanaongeza kodi kwa ajili ya kuongeza mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia maeneo mengine, sambamba na sigara kuna mabango ambayo yanatangaza sigara, kwa hiyo, mabango yale mbali na ukubwa, mbali na idadi waongeze kodi pale katika kuchaji maeneo hayo ya sigara ili kusudi matangazo yote ambayo yanahusu sigara yaongezeke vile vile siyo tu kwa ajili ya bei ya kununua sigara, ni njia nzuri ya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, lakini katika historia ya nchi yetu kwa Sheria ile ya Manunuzi ya mwaka 2004 na kufanyiwa mabadiliko mwaka 2005. Ni wakati muafaka Sheria ile ipitiwe upya, kwani kuna maeneo mengi ambayo inabidi yaboreshwe vizuri. Kwa mfano, unavyosema unachukua *bidder* ambaye ame-*tender the lowest*, lakini *the lowest* mwingine anaweza akachukua *the highest* lakini *reasons* zinakuwa ni tofauti, inaweza ikawa ni *restricted tendering*. Halafu ni uchochoro ambako fedha nyingi za Serikali zinapotea.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, asilimia 30 ya mapato ya Serikali yanapotea kutokana na kutokuwa na uaminifu katika eneo la manunuzi. Kwa hiyo, Sheria hii ije hapa Bungeni tuijadili ikae vizuri kwa ajili ya kuziba na kupunguza mianya hii ambayo wengine ambao siyo waaminifu wanapitia katika uchochoro huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza mapato kupitia Kamati hii ya Bajeti, tunashukuru sana imeanza na ni mwanzo mzuri na Kamati imeanza vizuri, lakini mapato haya na matumizi hivi kuna uwiano gani? Tusizungumzie sana kuhusu masuala ya mapato, lakini

usimamizi wa matumizi bado ni tatizo kubwa na ndiyo sababu katika bajeti tuna-*operate the lowest* katika nchi za Afrika Mashariki. Ukija kuangalia ile *historical background* ya Kenya, Uganda na Tanzania, katika bajeti wao mwaka jana kwa mfano, Kenya walikwenda kwa *conversion* ya fedha zao zilikuwa ni trilioni 26. Bajeti hii ambayo imesomwa juzi wapo trilioni 28.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaweza kuona ni kiasi gani bado tuna-*operate the low*. Wenzetu Waganda na idadi yao bilioni 34, bajeti yao mwaka jana ilikuwa trilioni 10, mwaka huu wamesoma bajeti juzi ni trilioni 16. Sasa tofauti ya Uganda na sisi trilioni mbili ni dhahiri bado tuna kazi kubwa ya kujipanga. Bajeti yetu bado ipo chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la msingi la kuangalia ni hili ongezeko la bei ya mafuta yakiwemo mafuta ya taa. Hivi ina- *sound* vipi kule kijijini kwetu kwa sisi ambao tumezaliwa vijijini, tunaishi vijijini, nishati yetu kubwa pale ni mafuta ya taa. Sasa unapopandisha mafuta ya taa hivi itakuwaje?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, fedha iende ikafanye kazi Majimboni. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa mara ya kwanza, wengi mmejadili Muswada uliopo na kwa kweli mmeujadili vizuri. Kwa hiyo, mmezingatia kwa mujibu Muswada ulivyoletwa na ushauri wenu na kwa sababu tutakuwa na kazi nzito kesho, nimeshafunga orodha ya wachangiaji na wote walioomba na waliokuwa kwenye orodha wameshachangia wote.

Kwa hiyo, kesho asubuhi baada ya kipindi cha maswali, tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, nategemea kama nilivyosema kwa maagizo yangu kwamba, wale waliokuwa na majedwali ya mabadiliko wawe wameshiriki kule kwenye Kamati ya Bajeti, hapa hatuta-entertain *anything*. Kwa sababu maamuzi

yangu ni kwamba, mabadiliko yoyote yatapelekwa kwenye Kamati. Kwa hiyo, Kamati ndiyo itakuja kuripoti walichokubaliana kuhusiana na mambo mengi.

Halafu lingine Waheshimiwa Wabunge, unapojadili usidhani kama wewe ndiyo una uwezo wa kujua vizuri sana, wewe upo tu hapa, lakini kuna watu wanaojua kwamba hili ndiyo, lakini lina matatizo yake. Kwa hiyo, katika Muswada mmoja mgumu sana kuujadili kwa kweli ni huu. Maana si suala la maneno ni suala la hesabu, si maneno mazuri, ni suala la hesabu. Sasa kama ni suala la hesabu basi tena mtaona ugumu ulivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ndugu zangu naomba tuwe pamoja, tuelewane. Kitu kingine pia sijui labda nyie siyo Bunge lililopitisha ile Sheria ya *Mortgage Finance*. Tulipitisha *Mortgage Finance Bill* hapa, hao mnaosema watu wadogo wadogo wa pikipiki hawa kama Wabunge mngeweza kuwa-*organize* wakakopa hizo pikipiki kwa *Mortgage Finance* zingekuwa za kwao. (*Makofi*)

The Mortgage Finance hata *fridge*, kama mama anafanya kazi yake ya kuuza *juice* anakwenda kukopa *fridge under Mortgage Finance*, kule wanakotoa ma-*fridge* wanampa friji, benki inayohusika itawalipa wale wanaohusika, yeye anaendelea kulipa, hii *Mortgage Finance* ilikuwa kwa watu wadogo wadogo. Kwa hiyo, hizo pikipiki kama hawa matajiri wanakuwa na pikipiki 1,000, halafu watu wanaendelea kuendesha tu mpaka wanaumia, lakini wanaweza kukopa kwa *Mortgage Finance*, Sheria tuliyotunga hapa.

Waheshimiwa Wabunge someni mkawasaidie wananchi waweze ku-*generate income* na walipe haki za Serikali.

Baada ya kusema hivyo, sina matangazo mengine, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho Tatu Asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 28 Juni, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)